**BUNGE LA TANZANIA**

_____

**MAJADILIANO YA BUNGE**

_____

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Nne – Tarehe 10 Aprili, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 24

**Serikali Kuongeza Fedha za Ujenzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Chemba**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni alipotembelea Wilaya ya Chemba aliahidi kuongeza fedha za ujenzi wa Jengo la Halmashauri mpya ya Wilaya:-

Je, katika mwaka huu wa fedha, Serikali imetenga kiasi gani kuendeleza ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Seleman Nkamia, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Halmashauri ilitengewa jumla shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba. Hadi Machi, 2017 fedha zote zimepokelewa na kazi inaendelea vizuri. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkamia, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imekuwa ikipeleka fedha kidogo kidogo kwenye Halmashauri hizi ambazo ni mpya. Je, haioni kwamba sasa hakuna sababu ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala kabla ya kumaliza maeneo ambayo tayari yameshaanzishwa na uendeshaji wake unasuasua?

Swali la pili, kuendesha Halmashauri ni gharama kubwa; kunahitaji huduma za afya, miundombinu na vinginevyo. Je, Serikali iko tayari sasa kuongeza bajeti kwenye Halmashauri mpya zote nchini ili kuziondoa kabisa katika hali ambayo sio nzuri sana kwa sasa na kuacha kabisa zoezi la kuanzisha maeneo mapya ya utawala? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Suleiman Jaffo, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *concern* ya

Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia tumeipata lakini nikujua uanzishwaji wa Halmashauri hizi mara nyingi sana unaanzia humu Bungeni. Hapa nimekuwa nikijibu maswali kadhaa kwa baadhi ya Wabunge na hasa Malocha anaeniangalia kwa jicho la karibu sana hapa; kila Mbunge kutokana na jiografia jinsi ilivyo anapenda Halmashauri yake iweze kugawanywa au kwa mfano Halmashauri ya Sikonge kule nilikofika ina *square* kilometa karibuni 27,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiangalia kweli kuna maeneo mengine ni kweli kulikuwa kuna haja ya kugawanya lakini vilevile na suala la kuhudumia hizi Halmashauri imekuwa ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tutaangalia kwa kina jinsi gani tutafanya; lengo kubwa ni wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili jinsi gani hizi Halmashauri ziweze kuongezewa mgao wa fedha. Naomba niseme jambo hili kwamba, kama Serikali tunalichukua ndio maana hata ukiangalia suala la bajeti kidogo linaongezeka. Changamoto kubwa ni kutokana na mapato yetu tunayoyapata kama Serikali kwa ujumla. Kikubwa zaidi naomba kuzihamasisha Halmashauri sasa ziweze kuweka mipango mizuri ya jinsi gani itakusanya mapato yake ya ndani kwa sababu mpaka leo hii ukija kuangalia Halmashauri mbalimbali hata ile bajeti tuliyoitengea mwaka huu zimesua sua katika ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, naomba nizihamasishe Halmashauri zihakikishe japokuwa tunazigawanya, lakini lazima *commitment* ya kukusanya mapato iwe ni kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *concern* yake Mheshimiwa Nkamia naomba tuipokee kama Serikali, kama ni ushauri mpana ili Serikali yetu iweze kwenda vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kuna Halmashauri nyingi zilianzishwa kwa

misingi ya kisiasa na kuacha Halmashauri ambazo zina hadhi kabisa ya Halmashauri. Vipi Serikali inaonaje kuzifuta mara moja Halmashauri ambazo zilianzishwa hazina vigezo na kuzipa Halmashauri zenye vigezo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Keissy ndio hoja ile ile ya Mheshimiwa Juma Nkamia. Ndio maana nimesema tukisema kuanzia leo hakuna kugawanya Halmashauri zingine, kuna Halmashauri zingine zina mzigo mkubwa kutokana na jiografia yake ilivyo kubwa kwelikweli. Kwa hiyo, tukisema kuanzia leo ni marufuku nadhani kuna baadhi ya Halmashauri hatutazitendea haki. Hata hivyo, ni kweli kuna Halmashauri zingine sasa hivi ukiziangalia kweli kama inawezekana tuzifute kwa sababu jiografia yake na hata *population* ya watu bado ni ndogo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya yote ni mawazo ya Waheshimiwa Wabunge lakini jambo kubwa ni kuijenga vizuri Serikali yetu. Nadhani mawazo yao ngoja tuyachukue na tuone kwa pamoja *way forward* ni nini, lengo likiwa hapo baadaye Serikali yetu iweze kuendeshwa vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea, Mheshimiwa Esther Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa n iaba na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

Na. 25

**Upunguzi wa Dawa Katika Hospitali za Wilaya**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY (K.n.y MHE. ESTHER A. MAHAWE)** aliuliza:-

Vituo vya Afya na Zahanati zilizo karibu na Hospitali za Wilaya zina changamoto ya utoaji huduma bora kwa

sababu ya upungufu wa dawa na watumishi wa kada ya afya hivyo kusababisha kuhudumiwa na Hospitali za Wilaya ambazo bajeti za dawa hazikidhi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza bajeti ya Hospitali za Wilaya zilizoko katika Mkoa wa Manyara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rai, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Manyara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2016/2017, Halmashauri za Mkoa wa Manyara zimetengewa bajeti ya shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kati ya fedha hizo, fedha zilizopokelewa hadi Machi, 2017 ni shilingi bilioni 1.07 sawa na asilimia 75%. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri za Mkoa huo zimepanga kutumia shilingi 1.58 kwa ajili ya dawa sawa na ongezeko la asilimia 9.7 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuanza kutumia mfumo wa kupeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa moja kwa moja katika vituo vya tiba yaani *Direct Facility Financing (DFF),* hali itakayosaidia vituo vya kutolea huduma kuboresha upatikanaji wa dawa kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati. Halmashauri zitabaki na jukumu la kusimamia taratibu zote na kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri niwashukuru Naibu Waziri wa Afya na Naibu

Waziri wa TAMISEMI kwa kuja Mbulu na kutembelea baadhi ya Halmashauri za Wilaya ya Mbulu na vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika swali la msingi muuliza swali alitaka pia mpango mkakati wa Serikali kuajiri kada za afya kwa maelezo ya swali la msingi. Je, Serikali ina mkakati gani na ajira ya kada za afya ili kupunguza tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ongezeko la asilimia 9.7 ni dogo sana ukilinganisha na tatizo la huduma ya afya hususan dawa na vifaa tiba katika nchi yetu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kukaa chini na kwenda katika Halmashauri zote nchini kufanya tafiti ili waweze kuleta mpango mkakati wa kuondoa tatizo la upungufu wa dawa na vifaa tiba katika nchi yetu*? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri , majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mpango mkakati wa Serikali ni suala zima la ajira kama tulivyosema. Niseme wazi kwamba ajira zilisimama kwa lengo mahususi kutokana na mipango ya Serikali na hapa juzi mnaona kwamba mchakato wa ajira za elimu hasa walimu wa sayansi umeanza lakini sio muda mrefu kwa kadri Ofisi ya Rais, Utumishi itakavyokuwa imejipanga itatoa vibali vya ajira kwa ajili ya sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuondoe hofu katika suala hilo kwa sababu tunajua wazi kwamba kweli tuna changamoto ya wahudumu mbalimbali hasa katika sekta ya afya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la mpango mkakati ni kweli, kwanza naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge leo hii ukifanya *reference* katika Halmashauri zetu kuna ma-*DMO* wengi sana walikuwepo hapa Mkoani Dodoma. Lengo ni kuhakikisha sasa tunatengeneza mipango mizuri na sio ile mipango ya mezani

peke yake; tunatengeneza mipango mizuri ya kwenda kujibu matatizo ya afya katika maeneo yetu. Leo hii tumesema fedha zitakwenda moja kwa moja mpaka katika kituo cha afya na zahanati; tumepata akaunti zote za vituo vya afya katika nchi yetu; huo ni mpango mkubwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo naomba niwaeleze ndugu zangu wakati mwingine tuna tatizo kubwa la usimamizi wa rasilimali fedha. Katika mwaka 2016/2017, mpaka mwezi Julai kuna *outstanding* fedha ambazo ni za *Basket Fund* hazijatumika karibu bilioni 20. Katika Mkoa wa Manyara peke yake kuna karibu milioni 500 mpaka mwezi Julai zilikuwa hazijatumika. Mpaka tunapozungumza leo hii bajeti yetu ya mwaka huu *Basket Fund* ni zaidi ya shilingi bilioni 106.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpaka mwezi Desemba fedha zile ambazo zimekuwa *accrued* ambazo hazijatumika na fedha zilizoingia ni takriban shilingi bilioni 71; kati ya fedha hizo 71, fedha ambazo zimetumika mpaka hivi sasa ni asilimia 55 tu mpaka mwezi Desemba, nini maana yake? Fedha zipo katika Halmashauri yetu lakini dawa hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwasihi Waheshimiwa Wabunge kwamba tuhakikishe katika Halmashauri zetu fedha za *Basket Fund* tuwabane ma-*DMOs* na wahasibu wetu tuweze kuzibainisha ziende zikanunue dawa na vifaa tiba; lengo kubwa ni kumwokoa mwananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Bilago, swali la nyongeza.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tatizo lililopo Manyara linafanana kabisa na tatizo lililopo Wilaya ya Kakonko. Tatizo ambalo lipo Hospitali ya Wilaya ya Kakonko ambayo ni kituo cha afya haijapata

hadhi ya Wilaya ni kupata dawa zenye hadhi ya kituo cha afya lakini zinatumiwa na wananchi wa Wilaya nzima kama Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Kakonko akaona hali ya kituo cha afya ilivyo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilago uliza swali, muda wetu unakimbia sana.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Ndiyo nauliza hivyo; ni lini sasa Kituo cha Afya Kakonko kitabakia kuwa kituo cha Afya ili iweze kujengwa Hospitali ya Wilaya ya Kakonko?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kweli nikiri kwamba, nimefika pale Kakonko na nimetembelea kile kituo cha afya tukiwa pamoja na Mbunge ni kweli kuna changamoto hizo kubwa lakini tubaini kwamba vipaumbele hivi mchakato wake unaanza kiwilaya. Hata hivyo, Mheshimiwa Bilago anafahamu kwamba pale alikuwa hana *ambulance;* Serikali imepeleka tayari *ambulance* kipindi hiki kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika mpango wa bajeti katika *Basket Fund* yake ana milioni 395, fedha ambayo nimpe taarifa mpaka mwezi wa Saba Halmashauri yake zaidi ya shilingi 197 zilikuwa hazijatumika zimevuka mwaka wakati wananchi wana matatizo. Kwa hiyo, naomba niseme sisi kama Serikali tutaangalia jinsi gani tutafanya katika mchakato huu ili kwenda pamoja na wenzetu wa Halmashauri, lakini jambo la msingi ni lazima tuwasimamie watendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine kuna baadhi ya wengine wanafanya mambo ya hovyo na wananchi wanaendelea kupata shida wakati fedha zipo; Mbunge na watu wengine wanapata matatizo kumbe fedha

zipo watendaji wetu wameshindwa kutimiza wajibu wao. Kwa hiyo, tupo pamoja kuhakikisha mambo yanaenda vizuri katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa leo tuna saa moja tu ya maswali kwa hiyo tuvumiliane, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa GoodlucK Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga sasa aulize swali lake.

Na. 26

**Mashirika na Taasisi za Umma Kujiunga na Mfuko wa Bima wa Taifa**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA** aliuliza:-

Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa ulianzishwa kwa ajili ya kuratibu na kusimamia matibabu kwa watumishi wa Serikali, taasisi na mashirika ya umma nchini:-

(a) Je, hadi sasa ni Taasisi na Mashirika ya umma mangapi yamejiunga na mfuko huo?

(b) Je, ni Taasisi na mashirika ya umma mangapi hayajajiunga na mfuko huo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulianzishwa kwa ajili ya kuratibu na kusimamia matibabu kwa watumishi wa Serikali, taasisi na mashirika ya umma nchini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 idadi ya wanachama katika mfuko ni 792,987 kutoka wanachama 474,760 mwaka 2012. Tangu kuanzishwa kwake

mwaka 2001, mfuko umefanya maboresho mbalimbali ya vitita vya mafao na namna ya kuchangia kwa makundi mbalimbali ya jamii. Maboresho haya yamewezesha kwa kiasi kikubwa kuongeza idadi ya wanachama walio katika mfumo huu wa bima ya afya nchini na kufanya wanufaika kufikia asilimia nane. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2016 idara za Serikali, taasisi na mashirika ya umma zilizotumia huduma za bima ya afya za *NHIF* zimefika 307. Idadi hii imetokana na jitihada za makusudi za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuwa na Bima kwa watumishi wa umma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika, taasisi na idara za Serikali ambayo hayajajiunga na mfuko yapo 23 yakiwemo *TRA, BOT, TANESCO, NHC, TPA, PSPF, LAPF, PPF, EWURA, NCA* na *GEPF.* Mfuko unaendelea na jitihada za kukutana na uongozi wa mashirika haya ya umma kwa lengo la kutoa elimu na kuwahimiza juu ya umuhimu wa kujiunga kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mfuko.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, swali la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; kwanza naomba nioneshe masikitiko yangu kwa kiwango cha juu kwa Waziri kijana kujibu majibu ambayo hayaendani na kasi ya Serikali kwa sasa hivi. Haya mashirika ambayo ameyataja *TRA, BOT, TANESCO, NHC* na *TPA* mimi mwenyewe binafsi nilitembelea wakati nipo *NHIF* lakini ni tofauti ya anavyosema Waziri sasa hivi. Je, katika michakato ambayo imeshawahi kutokea nchini kwetu mchakato mgumu ulikuwa wa kuhamia Dodoma, Rais alisema mwaka jana mwezi wa Saba lakini sasa hivi Mawaziri wote wamehamia Dodoma.

Swali la kwanza; je, ni nini kinashindikana mashirika haya ya umma kuhamia *NHIF* wakati ni kitendo cha muda mfupi tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ofisi yako ni shahidi Wabunge tulipotoka mashirika ya *private insurance*

kwenda *NHIF* tuliweza ku-*save* kiwango kikubwa cha pesa mpaka tukanunua madawati nchi nzima. Kumekuwepo na ubadhirifu mkubwa wa pesa za Serikali kwa haya mashirika ya umma *through private health insurance.* Je, Serikali itakubaliana na mimi sasa hivi kufanya mchakato wa kuangalia kiwango gani cha pesa kinachopotea iwapo mashirika ya umma yataendelea kutumia *private health insurance* badala ya *NHIF? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Kigwangalla, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naweka sawa, mimi sio Naibu Waziri kijana, mimi nimeshavuka umri wa ujana mimi ni mtu mzima na yeye bado kijana mdogo wangu lakini mimi sio kijana, mimi ni Naibu Waziri. Kumjibu ni kwamba, hakuna kinachoshindikana kwa mashirika kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa na kinachofanyika sasa hivi ndani ya Serikali ni mapatano baina ya shirika letu la *NHIF* na haya mashirika mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambapo tunatarajia watakapokubaliana kama ambavyo Katibu wa Bunge amekubaliana na Shirika letu la *NHIF* kuliingiza Bunge huko na haya mashirika mengine taratibu yataendelea kufanyiwa kazi kama ambavyo alikuwa akifanya yeye wakati ameajiriwa na *NHIF*. Aliendelea kuwashawishi kwa sababu sio suala la kulazimishana. Yeye amekuwa akienda kule kuwashawishi miaka yote ambayo amekuwa akifanya kazi kule hakufanikiwa kuwa-*convince* wakajiunga na mfuko; leo hii anataka tu hii miezi miwili, mitatu tuwe tumeshawa-*convince* sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo pengine mfupa uliomshinda yeye anatarajia sisi tutauweza kwa haraka zaidi wakati yeye mwenyewe ulishamshinda. Kwa hiyo wataalam wetu, kama alivyokuwa yeye mtaalam wa *NHIF* – wanaendelea kupatana na haya mashirika taratibu kuyashawishi yajiunge na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu yake ya pili; mpaka sasa hatujajua ni kiasi gani cha pesa ambacho pengine kinapotea kwa mashirika mbalimbali ya umma kuwa yamejiunga kwenye mifuko ya *private health insurance* na sio kujiunga katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hata hivyo, natoa rai kwa mashirika haya na Mawaziri ambao wanayasimamia mashirika haya kutoa maelekezo kwenye mashirika haya ili huu mchakato wa *negotiations* ambao unaendelea uweze kuongezwa kasi ili mashirika yote ya Serikali hatimaye yajiunge na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya badala ya kuwa kwenye mifuko hiyo mingine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naona umesimama lakini pia utusaidie sasa kama Mheshimiwa Mlinga alivyoshindwa yeye kufanya na Serikali sasa imeshindwa kuyaleta hayo mashirika kwenye *National Health Insurance Fund?* Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nimshukuru sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga kwa maswali yake mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwathibitishia suala la mashirika ya umma kujiunga na *NHIF* sio suala la hiari. Tayari kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanatumia *NHIF* kwa hiyo hatuoni kisingizio kwa mashirika ya umma kutumia *NHIF.* Nimetoka kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha na yeye alipowasilisha mpango wa bajeti na mwongozo wa sera za matumizi, Serikali imetoa maelekezo tutumie huduma na bidhaa zinazozalishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutakaa na mashirika haya tuweze kuona, wengi tumeongea nao wana mikataba na mashirika haya ya bima binafsi kwa hiyo hatuwezi kukatisha lakini nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mlinga, tutafanya kazi pamoja kuhakikisha mashirika yetu haya yote yanajiunga na

bima ya afya *NHIF.* Nitoe wasiwasi, *NHIF* sasa hivi inakubalika katika hospitali kubwa zote, kama Wabunge wanatumia sioni ni sababu gani mtumishi wa *TRA* na *BoT* asitumie huduma za *NHIF.* Mheshimiwa Mlinga, nakushukuru sana na tutafanya kazi pamoja kuhakikisha tunalitatua suala hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri na ile mikataba ambayo ni ya muda mrefu kuanzia sasa na yenyewe muiangalie kwa sababu mikataba huwa ina vifungu vya kukatikia njiani, muiangalie na hiyo. Mheshimiwa Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Hapo mwanzo Mfuko huu wa Bima ya Afya ulikuwa unatoa mikopo mbalimbali katika vituo vyetu vya afya, hospitali, kwa ajili ya ku-*support* matibabu kwa wateja wao, lakini tangu mwaka jana utaratibu huu wa kutoa mikopo katika hospitali zetu umekuwa sasa na urasimu kwa kupitia Hazina na tangu mwaka jana mwezi wa Tatu mikopo mingi imekwama Hazina.

Naomba nifahamu, Serikali ina mpango gani kurudisha utaratibu huu wa Mfuko wa Bima ya Afya katika Wizara husika ili hospitali zetu zipate mikopo ikiwemo Hospitali ya Mrara, Babati ambayo tumeomba mkopo tangu mwaka jana na hatujajibiwa? Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Utaratibu wa mikopo ni kwamba ni lazima taasisi za Serikali zinapokopa ziwe zimepata kibali cha kutoka kwa Msajili wa Hazina *(Treasury Registrar)* na huo ni utaratibu wa kawaida wa ndani ya Serikali. Kama ilikuwa ikifanyika hivyo huko nyuma maana yake taratibu zilikuwa haziko sawa lakini kwa mujibu wa *circular* ambayo ilitolewa na Msajili wa Hazina miezi takribani 24 iliyopita, utaratibu uliwekwa kwamba taasisi yoyote ile ya Serikali haitaruhusiwa kuchukua mkopo ama kutoa mkopo kwenye taasisi nyingine bila kuwa kuna kibali cha mwenye mali kwa maana ya *Treasury Registrar* ambaye

anazishikilia mali zote za mashirika ya umma, kwa hiyo ni utaratibu wa kawaida wa kisheria ambao ni lazima ufuatwe.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Lolesia Jeremia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Mapambano Dhidi ya Kifua Kikuu na *Silicosis***

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Katika Mkutano wa *SADC* uliofanyika Nchini Swaziland pamoja na mambo mengine suala zima la kupambana na Ugonjwa wa Kifua Kikuu na *Silicosis* lilijadiliwa. Ugonjwa huo unaathiri sana watu wanaojihusisha na shughuli za uchimbaji wa madini na wale wanaoishi kandokando na maeneo ya uchimbaji:-

(a) Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi wanachama wa *SADC;* je, inalifahamu tatizo hilo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kupambana na Ugonjwa huo wa Kifua Kikuu na *Silicosis,* hasa katika maeneo yenye shughuli za uchimbaji wa madini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inafahamu changamoto ya uwepo wa Magonjwa ya Kifua Kikuu na *Silicosis* katika maeneo ya wachimbaji. Kwa upande wa Kifua Kikuu inakadiriwa kuwa ukubwa wa tatizo hili ni kubwa zaidi

ikilinganishwa na hali halisi katika maeneo mengine na kwa upande wa *Silicosis* kumekuwepo na ripoti za wagonjwa wachache katika hospitali za Serikali ikiwemo Kibong'oto kuhusu wachimbaji wadogowadogo kutoka maeneo ya migodi. Kupitia ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria *(Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria),* nchi kumi wanachama wa Jumuiya ya *SADC* ikiwemo Tanzania zipo katika utekelezaji wa mpango wa kudhibiti kifua kikuu na magonjwa ya mfumo wa hewa yatokanayo na uchimbaji madini ikiwemo *Silicosis.*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia halmashauri zilizo katika maeneo ya migodi imeanza kuweka mikakati ya kudhibiti magonjwa haya kama vile kutoa elimu kwa wachimbaji ya namna ya kujikinga na vumbi na kutumia njia sahihi za uchimbaji. Vilevile, katika mpango huu wa *Global Fund to Fight HIV AIDS, Malaria and Tuberculosis* kuna afua *(intervention)* itakayoshughulika na Sera za Udhibiti wa Vumbi katika Maeneo ya Wachimbaji *(The Dust Control Policy)* ambayo itawabana wachimbaji kudhibiti vumbi wakati wa shughuli za uchimbaji. Aidha, Serikali itaongeza wigo wa huduma katika vituo vya afya kwenye maeneo yaliyoathirika ikiwemo Mkoa wa Geita ili vituo viwe na uwezo wa kuchunguza na kutibu magonjwa hayo na kuwajengea uwezo wataalam wa afya katika kuhudumia wagonjwa katika maeneo ya migodi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Losesia Bukwimba, swali la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kabisa kwamba tatizo hili la Kifua Kikuu ni kubwa sana na hasa katika maeneo ya wachimbaji wa madini ikiwemo Geita. Ningependa kujua sasa kwamba Serikali ni lini itaweza kufanya utafiti wa kina hasa katika maeneo ya wachimbaji ili kubaini ukubwa wa tatizo hili katika maeneo haya na hatimaye kuweza kupatiwa ufumbuzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa nchini Tanzania tatizo hili la kifua kikuu ni kubwa sana, katika takwimu za dunia inaonesha kwamba mwaka 2015 watu 160,000 waliweza kupata tatizo hili la kifua kikuu. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwa na sera pamoja na mikakati ili kuweza kupambana kutokomeza ugonjwa huu wa kifua kikuu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Kigwangalla, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kwamba ni lini Serikali itafanya utafiti kwenye maeneo haya, naomba nimuahidi tu kwamba, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati hii kama ambavyo imeweka mpango wake wa bajeti wa kila mwaka na tutakapopata pesa mahususi kwa ajili ya tafiti mbalimbali, tutahakikisha tunatoa kipaumbele kwenye eneo hili la maeneo ya migodi kwenye magonjwa haya ya kifua kikuu pamoja na magonjwa ya *silicosis.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tarehe mahususi kwamba ni lini tunaweza tukafanya hivyo lakini dhamira yetu ni njema na kwamba tutakapopata pesa basi tutazielekeza kwenye tafiti kwenye maeneo haya ya migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwamba kwa nini Serikali isilete sera kwa ajili ya Kifua Kikuu; naomba nimjulishe tu kwamba sera tunayo na *infact* mapitio ya sera yanatuelekeza sasa hivi ndani ya Serikali kutekeleza miradi ya Kifua Kikuu, uchunguzi pamoja *(case detection)* mpaka kwenye ngazi ya jamii, kwenye ngazi ya kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ufuatiliaji wa kesi mbalimbali za kifua kikuu kwa sera hii tuliyonayo sasa unafanyika mpaka kwenye ngazi ya *community* kwa maana ya kwamba tunakwenda mpaka kwenye kaya, kwenye

*household.* Kwa hiyo sera tunayo na tunaendelea kuitekeleza na kwa kiasi kikubwa katika miaka ya karibuni maambukizi ya kifua kikuu yameendelea kupungua.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, samahani, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nimesimama kutoa msisitizo kwa swali la Mheshimia Lolesia Bukwimba, ni kweli tuna wagonjwa takribani 160,000 wa kifua kikuu nchini lakini changamoto yetu kubwa ni kuwafikia wagonjwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kuwafikia wagonjwa takribani 62,000 tu, kwa hiyo nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge, tunapokwenda katika majimbo yetu tuwahamasishe wananchi kupima kifua kikuu, takribani wananchi 100,000 tunao katika majumba yetu, katika kaya zetu, katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo tumelifanya, kila mama mjamzito na mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano anayekwenda hospitali sasa hivi atapimwa kifua kikuu na watu ambao pia wana maambukizi wa VVU. Kwa hiyo, nawaomba sana kifua kikuu kiwe ni agenda yenu ya kila siku mnapokuwa katika majimbo yenu. Mtu ambaye hajapata matibabu ana uwezo wa kuambukiza mpaka watu 20 kwa mwaka mmoja, tusipochukua hatua Kifua Kikuu kitakuwa ndicho kinachoongoza kuua kuliko Malaria au *HIV/AIDS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona nisimame ili kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge kushiriki katika mapambano ya kifua kikuu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiawa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Ukonga, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Na. 28

**Uingizaji wa Mayai Kutoka Nje**

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. MWITA M. WAITARA)** aliuliza:-

Baadhi ya wakazi wa Ukonga wanafuga kuku wa mayai na wengine wanatengeneza chakula cha mifugo, shughuli zinazowainulia kipato na kuweza kupata mahitaji muhimu ya kimaisha, lakini shughuli zao zimeathiriwa na watu wanaoingiza mayai toka nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia uingizaji wa mayai toka nje kwa sababu unaharibu soko la ndani la bidhaa hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia malighafi ili chakula cha mifugo kiendane na bei ya mayai na kuku?

(c) Je, Serikali ipo tayari kusimamia wananchi walipwe fidia kutoka kwa wawekezaji wanaoingiza vifaranga wasio na chanjo toka nje ambao wengi wao hufa na kusababisha hasara kwa wananchi wafugaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2006, Serikali iliweka katazo la kuingiza kuku na mazao yake nchini ili kudhibiti Ugonjwa hatari wa Mafua ya Ndege. Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za Mwaka 2007 na 2010 zinatumika kudhibiti na kukagua uingizwaji katika maeneo ya mpakani, bandari na viwanja vya ndege. Hakuna mwekezaji yeyote anayeruhusiwa

kupewa kibali cha kuingiza vifaranga au mayai nchini kwa ajili ya biashara na katika kusimamia hili kuanzia mwaka 2013 hadi 2017, vifaranga 67,500 vilivyoingizwa nchini kinyume na sheria viliteketezwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasimamia ubora wa malighafi za kusindika vyakula vya mifugo kupitia Sheria ya Maeneo ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Na. 13 ya Mwaka 2010. Changamoto katika kusindika vyakula hivyo ni gharama kubwa ya viinilishe vya protini kutokana na matumizi ya maharage aina ya soya. Maharage haya huagizwa kutoka nje ya nchi hususan Zambia na India. Wizara inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa soya hapa nchini katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wawekezaji wachache ambao hupewa vibali maalum vya kuingiza nchini mayai au vifaranga wa kuku wazazi *(parent stock)* tu. Ukaguzi kwa ajili ya kudhibiti uingizaji wa vifaranga na mayai unaendelea na hatua kali zinachukuliwa kwa yeyote atakayekamatwa kwa kukiuka utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kadri ya muuliza maswali, kipengele namba (c) kinasema je, Serikali ipo tayari kusimamia wananchi walipwe fidia kutoka kwa wawekezaji wanaoingiza vifaranga wasio na chanjo toka nchi za nje? Kimsingi kwenye jibu lake haja-*commit,* hajasema kama Serikali sasa hivi iko tayari kuhakikisha wafugaji wale wanaopata hasara wanalipwa fidia yao, kwa hiyo tunaomba Serikali itoe neno kwenye hili. Pia itueleze kama hali ni hii basi izuie kabisa watu wasiingize vifaranga ambavyo havina chanjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji hasa wa chakula kama alivyosema yeye mwenyewe na tumeona gharama kubwa sana kwenye chakula cha mifugo. Kwa kipindi hiki ambapo kuna tatizo kubwa la chakula na njaa, Serikali haioni sasa umefika wakati iondoe angalau kodi fulani ili kuweza ku-*compensate* wakulima katika kupata chakula chenye bei nafuu na wananchi waweze kununua kuku kwa bei nafuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia, kimsingi suala la fidia halitokei kwa sababu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, kimsingi ni kinyume cha sheria na taratibu kuingiza kuku na mayai kutoka nje, kwa hiyo wale ambao wanaingizwa kwa taratibu ambazo sio rasmi, wanaingizwa kwa utaratibu wa njia za panya. Kwa hiyo, kimsingi Serikali imeweka utaratibu kuhakikisha kwamba hairuhusu uingizwaji, hivyo kutokea na ndiyo maana tumesema tayari katika kipindi cha miaka minne tumeteketeza vifaranga zaidi ya 67,000. Hata hivyo, tunachotaka kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge ni kuonesha ushirikiano kama wanaweza wakatuonesha watu ambao wanaingiza vifaranga na mayai kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na gharama ya vyakula vya mifugo, hasa kuku, kama nilivyosema vilevile ni kweli kwamba kuna gharama kubwa sana katika kutengeneza vyakula vya kuku kwa sababu kiinilishe kinachotumika ni maharage ya soya ambayo hatuzalishi hapa nchini. Kwa hiyo, hatua ambazo tunazichukua ni pamoja na kuhamasisha wananchi walime zao la soya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kupitia hotuba ya bajeti ya Wizara yetu kwa ajili ya mwaka wa fedha unaokuja, Serikali imechukua hatua kadhaa kupunguza kodi na tozo

za mazao na bidhaa mbalimbali ili basi vyakula vya kuku na mazao mengine viweze kupatikana kwa bei nafuu. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la kodi na tozo litashughulikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 29

**Changamoto Zinazokabili Kilimo cha Viazi – Njombe**

**MHE. LUCIA M. MLOWE** aliuliza:-

Kilimo cha viazi katika Mkoa wa Njombe kimekuwa ni ukombozi kwa wananchi wa mkoa huo. Zao hilo ni la biashara lakini wananchi wameanza kukata tamaa kutokana na kupanda kwa bei za pembejeo, pembejeo kutokufika kwa wakati na kukosa soko la uhakika:-

Je, Serikali ipo tayari kuwaunganisha wakulima hao na kuwa na chama chao kitakachoweza kupigania haki za wakulima hao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikihimiza makampuni na mawakala wanaosambaza pembejeo za kilimo kuwafikishia pembejeo wakulima kwa wakati kabla ya msimu wa kilimo kuanza. Kutokana na juhudi ya Serikali kwa kushirikiana na makampuni yanayosambaza pembejeo, imewezesha ufikishwaji wa pembejeo ikiwemo mbolea na mbegu bora kwa bei ya soko kwa wakulima kwa wakati. Aidha, changamoto ya kupanda bei ya pembejeo

inafanyiwa kazi kwa kuondoa tozo mbalimbali ili kupunguza bei ya pembejeo na kuwezesha wakulima kumudu kununua na kutumia pembejeo hizo. Vilevile Serikali inakamilisha mchakato wa manunuzi ya pamoja *(bulk procurement)*, uondoaji au kupunguza tozo mbalimbali na gharama za usafirishwaji katika mbolea ambao utasaidia kuongeza upatikanaji na kupunguza bei ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuhimiza uzalishaji wa mbegu za viazi kupitia vikundi katika ngazi ya mkulima. Kupitia utaratibu huu wakulima wengi watamudu kununua mbegu za viazi kwa bei nafuu kwa vile zinazalishwa ndani ya kijiji. Pia kupitia *SAGCOT* wakulima nane wamepata mafunzo ya kuzalisha mbegu za viazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambazo zitauzwa ndani ya mkoa na hivyo kuchangia upatikanaji wa mbegu za viazi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari kuwaunganisha wakulima wa zao la viazi kwa kutumia taasisi zake katika kuunda ushirika ambao utasaidia kuanzisha chama chao kulingana na taratibu za uanzishwaji wa vyama vya ushirika. Jukumu hili litatekelezwa kupitia tume ya ushirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri husika katika Mkoa wa Njombe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucia Mlowe, swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Swali la kwanza, kwa kuwa tatizo la pembejeo limekuwa la muda mrefu na ni sugu katika Mkoa wetu wa Njombe. Je, Serikali iko tayari sasa kuanzisha Kiwanda cha kutengenezea mbolea katika Mkoa wa Njombe?

Swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Njombe ni kati ya Mikoa inayotoa viazi au inayolima viazi kwa wingi; Njombe peke yake inalima au inatoa viazi tani 900,000 kwa mwaka,

lakini tatizo ni kwamba soko limeingiliwa na watu wa Kenya. Je, Serikali iko tayari sasa kuwazuia watu wa Kenya wasilete viazi nchini Tanzania ili wakulima wetu wa viazi waweze kuwa na soko zuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Serikali kujenga Kiwanda cha Mbolea Njombe; Serikali ya Awamu ya Tano inahamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda, kwa hiyo, tuko tayari kushirikiana na Mbunge pamoja na wadau wengine wowote ambao wanataka kuanzisha Kiwanda cha Mbolea-Njombe. Vilevile ni lazima niseme kama nilivyosema, tunategemea bei ya pembejeo ishuke kuanzia mwaka unaokuja kwa sababu karibuni tutaanza utaratibu wa kuagiza mbolea kwa pamoja *(Bulk Procurement).*

Kuhusiana na suala la ushindani wa Wafanyabiashara kutoka Kenya; kimsingi tunabanwa na itifaki za Kikanda kuhusiana na biashara, kwa hiyo ni vigumu moja kwa moja kuwazuia wakulima wa Kenya isipokuwa tunachofanya ni kujenga mazingira ambayo wakulima wetu wanaweza wakazalisha kwa tija ili waweze kushindana na wafanyabiashara wengine kutoka Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nipende tu kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba ushindani siyo mbaya na mara nyingi Wakenya wanapokuja kununua viazi kutoka kwetu ni kwa sababu kuna tofauti kati ya msimu wa viazi kuzalishwa Njombe na Kenya, kwa hiyo tusiogope ushindani lakini tujizatiti zaidi tuweze kuzalisha kwa tija ili tuweze kushindana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlowe naona Waziri wa Viwanda hapa anapiga sana makofi kwa hiyo nadhani utamwona ili akukabidhi kiwanda kimoja.

Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 30

**Serikali Kuliongezea Bunge Bajeti**

**MHE. LUCY S. MAGERELI** alililiza:-

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano kumekuwa na mabadiliko makubwa ya uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kupunguza muda. Bunge sasa hukaa kwa siku 10 hadi 12 tu jambo ambalo linasababisha muda wa kuchangia na Mawaziri kujibu hoja kuendelea kupunguzwa hadi kufika dakika tano tu kitu ambacho kimepunguza kabisa ufanisi wa chombo hiki muhimu chenye majukumu muhimu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliwezesha Bunge kufanya shughuli zake kwa ufanisi kwa kuliongezea bajeti?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali kuliwezesha Bunge kufanya shughuli zake kwa ufanisi ni kwa kutoa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwenda kwenye Mfuko wa Bunge Fungu namba 42 kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, taarifa ya utekelezaji ya Mfuko wa Bunge na hali ya upatikanaji wa fedha. Kifungu cha 45(b) cha Sheria ya Bajeti kinatuelekeza tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 99 na hadi Februari, 2017 jumla ya shilingi bilioni 62.6 sawa na asilimia 68 ya bajeti ya mfuko huo

zilitolewa. Serikali inaahidi kutoa fedha zote zilizobaki kwenye bajeti ya fungu hili yaani shilingi bilioni 8.3 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 6.7 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali imeongeza bajeti ya Mfuko wa Bunge kutoka shilingi bilioni 99 mwaka 2016/2017 mpaka shilingi bilioni 121 mwaka ujao wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Magereli swali la nyongeza.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Hata hivyo, nieleze masikitiko yangu tu kwamba eti unapata majibu ya Serikali, yanakwambia Mpango wa Serikali kuliwezesha Bunge kufanya shughuli zake kwa ufanisi ni kutoa fedha toka Mfuko Mkuu wa Serikali kupeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Bunge, Fungu 42 eti huo ndiyo mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu najua sisi wote hapa katika Bunge hili ni mashahidi, majukumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muhimu na nyeti sana kuliko hiki ambacho Serikali inataka kutuambia kwamba mpango wake ni kutoa fedha Mfuko Mkuu wa Serikali na kupeleka Mfuko wa Bunge. Ninyi wote ni mashahidi kwamba kwa mujibu wa kanuni, muda wa Kamati za kuelekea bajeti ni wiki tatu lakini *this time* wiki moja imeondoshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye swali langu la msingi nilichouliza ni kwamba, muda wa uendeshaji wa shughuli za Bunge umepunguzwa mno kiasi cha kufikia siku 10 hadi 12, lakini hata muda wanaopewa Mawaziri kujibu hoja za Wabunge na wananchi wa Tanzania nao umepunguzwa kufikia kiasi cha dakika tano. Kwa hiyo, hatutekelezi wajibu wetu kama Bunge kwa sababu tunakimbizana na muda ingawa hili la muda naona halikuzingatiwa, lakini bado hoja ya bajeti mpaka mwezi

wa Pili mmetupa asilimia 68, tu kwa hiyo bado hata hilo ambalo mlifikiri ni kazi rahisi tu kutoa Mfuko wa Serikali kuweka Mfuko wa Bunge bado hamjatoa kiasi kinachokidhi, bado mnatusafirisha kwenye *Hiace*, bado...*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli naomba uulize swali yaani muda wetu umekimbia, uliza swali tafadhali.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa binafsi yangu, naomba nielezwe kabisa *straight forward* kama hili ndiyo jibu la Serikali basi swali hili halijajibiwa naomba lijibiwe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli kwa sababu hujauliza sasa swali la nyongeza unaomba lijibiwe, nadhani utatumia kanuni mahususi inayohusu swali kujibiwa kikamilifu kwa hiyo wakati utakapofika, Waziri nadhani hujaulizwa swali la nyongeza. Kwa hiyo, tunaendelea. Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 31

**Ongezeko la Taasisi Zinazotoa Huduma za Kibenki**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Hapa nchini pamekuwepo na ongezeko kubwa la Taasisi mbalimbali zinazotoa huduma za kifedha kama vile Benki, Vikundi mbalimbali kama *VICOBA*, Taasisi za Kukopesha Watumishi, Taasisi za kukopesha wafanyabiashara na wakati mwingine watu na mitaji yao wanakopesha watumishi (kienyeji) kwa kificho ficho:-

(a) Je, ni chombo kipi hasa chenye wajibu wa kufuatia kodi zinazotozwa na wananchi?

(b) Je, kodi zinazotozwa ni halali?

(c) Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wananchi wake hawaibiwi kwa njia hiyo?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, Toleo la 2005, Ibara ya 138(1) inaelekeza kuwa, hakuna kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge au kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa Kisheria na uliotiwa nguvu Kisheria na Sheria iliyotungwa na Bunge

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399(5) imeipatia Mamlaka ya mapato wajibu wa kukadiria, kutoza na kutoa hesabu za mapato yote ya umma. Aidha, Sheria ya bajeti kifungu cha 58(b) inaelekeza kuwa mtu yeyote aliyepewa Mamlaka ya kukusanya mapato ya Serikali atawajibika kukusanya kwa ufanisi, kutoa hesabu za mapato, kuyawasilisha na kuyatolea taarifa kwa kuzingatia Sheria husika na kuchukua tahadhari kuzuia usimamizi mbovu wa mapato na pale inapolazimu, mfano; katika operesheni maalum dhidi ya wakwepa kodi sugu au mazingira hatarishi, *TRA* inaweza kuomba msaada wa vyombo vingine vya dola.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kodi halali zinazotozwa kwenye huduma za kifedha kwa mujibu wa Sheria ni zifuatazo:- Kodi ya zuio kwenye faida inayolipwa kwa Mwekezaji ambayo ni pamoja na amana za Benki, dhamana za Makampuni au Serikali na hisa; Kodi za ongezeko la thamani kwenye ada zinazotozwa kwenye huduma za kifedha na ushuru wa bidhaa kwenye ada inayotolewa kwenye kutuma au kupokea fedha kwa njia za kielektroniki na hususani simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo mtu binafsi ama Taasisi itatoza ama kukusanya kodi yoyote kinyume na matakwa ya Sheria, anakuwa ametenda kosa na hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa mara moja dhidi yake.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa wananchi hawaibiwi kutokana na taasisi zinazotoa huduma ya ukopeshaji kwa kificho ama kienyeji, Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogondogo za Fedha ya mwaka 2000 kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Taasisi ndogo za fedha zinasimamiwa ipasavyo. Kwa sasa Serikali inakamilisha mapendekezo ya kuwa na Sheria ya kusimamia taasisi ndogo za huduma za fedha ambazo zitawezesha kuondokana na hali hiyo iliyopo sasa. Vilevile Serikali imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara kwa wananchi na jamii kwa ujumla ili kuhakikisha kuwa taasisi zinazoingia nazo mikataba ya ukopeshaji wa fedha na shughuli nyingine zinakuwa zimesajiliwa na kutambuliwa kisheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Desderius Mipata swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza:-

La kwanza; kwa kuwa wapo watu wanaokopesha kienyeji na hutoza riba kubwa inayofikia asilimia 30 kwa mwezi na inapotokea mkopaji akakosa kulipa maana yake mwezi unaohusika gharama hiyo hupanda kwa maana ya *compound interest* kwamba mtaji pamoja na asilimia iliyopaswa kutozwa hufuata kwa mwezi mwingine na hali hii huacha wananchi katika hali ngumu sana. Je, Serikali inawajua vizuri hawa watu na ina mpango gani wa kutafuta njia ya kuimaliza kadhia hii? *(Makofi)*

Swali la pili; kwa kuwa watumishi ndiyo walengwa wakuu katika jambo hili pamoja na wastaafu ambao wako karibu kustaafu na kadhia hii huwafanya wapoteze hata ufanisi kazini; je, Serikali haioni umuhimu wa kulichukulia hili jambo kama vita ya madawa ya kulevya kwa sababu watumishi wengi wanastaafu wakiwa hawana kitu chochote na familia zao zinasambaratika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, ni kweli kabisa riba hizi kwa hawa wakopeshaji wa mitaani ni mzigo mkubwa kwa wale wanaolazimika kwenda kukopa huko na ndiyo maana Serikali imekuwa inasisitiza kwamba kadri inavyowezekana wasiende huko, lakini jibu langu la msingi ni kwamba; sasa hivi Serikali tunafanya jitihada kubwa na tayari tumeshaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri ili jambo hili baada ya kulifanyia kazi kwa mapana yake liweze kushughulikiwa kwa ukamilifu na maagizo maalum ya Serikali baada ya kuwa waraka huu umepitiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile la kusema kwamba tuichukulie kama vita nafikiri tusiende huko kwa sasa kwa sababu waraka umeandaliwa, ni vizuri tupate nafasi ya kulichukulia maamuzi tukiwa tumetulia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje sasa aulize swali lake.

Na. 32

**Umuhimu wa Kujenga Kituo cha Forodha na Ukaguzi-Ileje**

**MHE. JANET Z. MBENE** aliuliza:-

Jumuiya za kiuchumi za Kikanda zimekuwa sehemu ya mkakati mkubwa katika kuratibu masuala ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kimazingira. Ileje ni Wilaya ya mpakani mwa Nchi za Malawi na Zambia lakini haina kituo cha forodha. Hakuna miundombinu ya soko la Kimataifa, hakuna kituo cha uhamiaji, hakuna kituo cha kudhibiti mazao, mifugo wala silaha. Hii inasababisha wahamiaji haramu na wahalifu kutumia mipaka kinyume cha sheria na taratibu:-

Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha forodha, kituo cha uhamiaji, soko la Kimataifa na kituo cha kukagua mifugo na silaha kwa ufanisi na maendeleo ya lleje?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu**:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa lleje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kabisa kuwa katika Wilaya ya lleje hakuna kituo cha forodha na uhamiaji wala soko la Kimataifa na vituo vya kukagua mifugo na silaha. Namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge ambaye ameendelea kufuatilia jambo hili kwa nguvu sana na kwa kutambua umuhimu huo, Mamlaka ya Mapato na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tayari tumefanya jitihada tumepata kiwanja kwa ajili hiyo lakini bado tunafanya mashauriano na nchi jirani na hususani Zambia na Malawi kwa sababu ya utaratibu wa kujenga kituo cha pamoja lakini pia tutahitaji maandalizi kwa ajili ya kuamua jengo lenyewe hilo la kituo cha pamoja liweje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kazi hizo kukamilika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaanza utekelezaji wa ujenzi wa kituo hicho mara baada ya kuwa shughuli hiyo imekamilika, lakini kwa sasa natoa rai kwa niaba ya Serikali kwa wananchi wa Wilaya ya lleje na Wilaya zinazofanana na hizo kuendelea kutumia huduma zilizo katika Wilaya na Mikoa jirani wakati tunafanya utaratibu wa kujenga vituo hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janet Mbene, swali la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutupa moyo na kutuhakikishia kuwa tayari mikakati ya kutuwekea kituo cha forodha iko njiani. Hata hivyo, nataka vilevile nimtake Mheshimiwa Waziri na Serikali kuharakisha mipango hiyo kwa

sababu hivyo vituo vya jirani anavyovizungumza bila shaka anazungumzia Kasumulo iliyopo Kyela, anazungumzia Tunduma ambavyo vyote viko mbali sana na lleje na lleje kama inavyofahamika hakuna barabara hata moja inayopitika vizuri, kwa hiyo kutuambia sisi twende tukatumie vituo vile ni kama kutudhihaki. Pamoja na hayo, tayari ardhi imeshaanza kupimwa na inamaliziwa, tayari maeneo yameshaainishwa, tayari wahusika wameshakuja kukagua maeneo, namwomba sasa Mheshimiwa Waziri anihakikishie kuwa sasa hatua itakayofuata ni ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Malawi; Malawi tayari wana kituo, wanatungojea sisi. Miundombinu yetu sisi ndiyo inachelewesha kile kituo cha Malawi kushirikiana na cha kwetu. Kwa hiyo, naomba sana hilo lifahamike na atuhakikishie hapa ni lini sasa hatua hizo zitafanyika? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa lleje kwamba maoni yake yatazingatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani sasa aulize swali lake

Na. 33

**Ajali ya Bodaboda**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS (K.n.y MHE. ABDALLAH HAJI ALI)** aliuliza:-

Usafiri wa bodaboda unatoa ajira kwa vijana walio wengi na kurahisisha usafiri, lakini zimekuwa zikisabaisha ajali nyingi mara kwa mara:-

Je, ni watu wangapi wamepoteza maisha na wangapi wamejeruhiwa na ajali za pikipiki kuanzia mwaka 2010 hadi 2017?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu ndugu yangu Abdallah Haji Ali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pikipiki za matairi mawili yaani bodaboda na matairi matatu yaani bajaji zilianza kutumika kubeba abiria kuanzia mwaka 2008. Mwaka 2010 Serikali ilipitisha kanuni na masharti ya usafirishaji wa pikipiki pamoja na bajaji. Aidha, katika kipindi hicho hakukua na utaratibu wowote wa kusimamia biashara ya uendeshaji pikipiki pamoja na bajaji zinazobeba watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2010 hadi Februari, 2017 kumekuwa na jumla ya ajali 31,928 zilizosababisha vifo vya watu 6,529 na majeruhi 30,661.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa idadi ya watu ambao wanapoteza maisha kutokana na ajali za bodaboda basi hata tungekuwa vitani tungekuwa tunapigwa! Kwa hivyo, namuuliza Mheshimiwa Waziri, tuna mikakati gani ya ziada ya kutoa elimu juu ya waendesha pikipiki ili tuzipunguze ajali hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; barabara wanayokatisha Wabunge kuingia ndani na kutoka nje ya Bunge sio salama. Tarehe 5 juzi kagongwa Mbunge mwenzetu na kapata majeraha makubwa sana. Je, Serikali inawahakikishiaje Wabunge usalama wa eneo hilo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kupata *concern* hiyo. Ni kweli watu karibu 7,000 ni wengi na ajali zaidi ya 31,000 ni nyingi sana. Tunalolifanya, kwanza tumesemea iwepo elimu kwa kila mkoa na kila wilaya ambazo zinafanywa na *department* yetu inayoshughulika na masuala ya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nitoe rai hata kwa Wabunge tunapokuwa na vijana wetu, watambue kwamba vyombo hivyo pamoja na kuwa na matairi mawili lakini ni vyombo vya moto. Wazingatie masharti ya uendeshaji wake kwa sababu kwa kiwango kikubwa kwenye upande wa magari huwa kuna sababu zingine ambazo zinasababisha ikiwepo na uchakavu wa vyombo, lakini kwa bodaboda ajali nyingi zinasababishwa na kutokuzingatia utaratibu wa uendeshaji ikiwepo kwenda mwendokasi na kuendesha vyombo hivyo kabla ya kuwa wamejifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili hapa alilosemea la pili kuhusu kuzingatia masuala ya usalama, tumeshaongea kuweza kuweka utaratibu mahsusi ambao utakuwa unadhibiti. Siku ile walikuwa wamesimamisha magari lakini yule wa bodaboda akaja akapita moja kwa moja kama ambavyo nimesema wamekuwa na utaratibu huo wa kwenda kasi lakini tumeendelea kutoa elimu na tumesema ianzie hata ngazi za familia waweze kutambua kwamba kwenda kasi kwa vyombo hivyo vya moto pamoja na kuwa na matairi mawili lakini vinasababisha ajali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali letu la mwisho ni la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na.34

**Utaratibu wa Kutoa *Form* ya *PF3***

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Fomu ya *PF3* hutolewa na polisi tukio linapotokea na kumletea usumbufu mgonjwa kwani anatakiwa kuwa na uthibitisho wa fomu hiyo ili daktari atoe ushauri wake na pia mgonjwa hawezi kupatiwa huduma yoyote mpaka awe na fomu hiyo hata kama ana maumivu makali au hali yake ni mbaya;

Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kufanya marekebisho ya utaratibu ili kuwaondolea usumbufu wagonjwa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu mama yangu Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshmiwa Naibu Spika, Serikali iliweka utaratibu wa mtu anapokuwa ameumia apate *Police Form No. 3* kwa mujibu wa Kifungu cha 170 cha Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi ili aweze kupokelewa na kupewa matibabu katika hospitali zetu. Msingi mkubwa wa hiyo fomu ni kutaka kujua mazingira ya mtu huyo aliumia wapi na alikuwa anafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *PF3* inatumika pia kama kielelezo Mahakamani kama mtu ameshambuliwa ama amepigwa ili Mahakama ijue ameumia kiasi gani na kwa kuwa rahisi kutoa adhabu stahiki. Hata hivyo, kuna matukio mengine yaliyo wazi ambayo *PF3* hupelekwa hospitali kwa urahisi wa matibabu na kwa msingi huo *PF3* bado inakidhi matakwa yaliyokusudiwa kwa mujibu wa kifungu nilichokitaja hapo juu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mchemba, swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa kuwa wananchi wengi wamekuwa waoga kwenda kwenye kituo cha polisi hususan wanawake na kwa kuwa maeneo mengi hayana vituo vya polisi hususan vijijini. Je, Serikali iko tayari sasa kugatua madaraka kwa Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ili waweze kupata matibabu pale wanapopata ajali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuona uhalisia unaotokea kwenye *grass root.* Niseme tu tumepokea wazo hilo, itabidi tuongee na wenzetu wa TAMISEMI kwa sababu likiamuliwa kufanyika katika msingi huo kuna vitu ambavyo lazima tujiridhishe navyo na aina ya maumivu ambayo yanaweza yakatumika kwenye ngazi ya viongozi wetu wa Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu ambacho huwa tunakiepusha na kulazimisha ipitie polisi hasa ni kwa wale ambao wanaweza wakafanya makosa makubwa kwa mfano, mtu aliyeenda kuiba akawa amejeruhiwa angetamani sana asipitie polisi aende moja kwa moja hospitalini. Kwa hiyo, huwa tunaona apitie polisi na wale wengi wanaokwepa kupitia polisi tunakuwa tunajua watakuwa wana vitu wanavyovihofia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa vitu ambavyo vimefanyika katika ngazi ya familia labda mtu amepata ajali ya kawaida katika ngazi ya familia ama katika eneo na anafahamika, ana kumbukumbu nzuri za kutokuwa na

vitendo vya kihalifu ni maeneo ambayo tunaweza tukaongelea tukaenda katika taswira hiyo aliyoisemea Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Nitaleta kwenu matangazo na tangazo letu la kwanza linahusu wageni waliopo Bungeni leo.

Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi ambao wamekuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu na karibuni sana wanafunzi mliokuja kujifunza, tunaamini mnapotoka hapa mtakuwa mmejifunza mengi, mtapata fursa ya kujua mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili, linatoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu ya Bunge na inahusu uhakiki wa taarifa za namba ya utambulisho wa mlipa kodi. Yaani, *TIN Number.* Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa Maafisa toka Mamlaka ya Mapato Tanzania watakuwepo kwenye viwanja vya Bunge kuanzia leo tarehe 10 Aprili, 2017 hadi tarehe 14 Aprili, 2017 kwa ajili ya kuhakiki taarifa na namba za utambulisho wa mlipa kodi.

Waheshimiwa Wabunge, ili muweze kuhakikiwa mnatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo:-

Ya kwanza ni fomu ya maombi ya *TRA* ambayo unapaswa kwenda ukiwa umeshajaza.

Ya pili ni kwamba fomu hiyo iambatane na nakala ya kitambulisho kimojawapo kati ya kitambulisho cha mpiga kura au kitambulisho cha Taifa au leseni ya kuendesha gari.

Halafu cha tatu fomu hizo zinaweza kujazwa kupitia mtando wa *TRA.* Pia Waheshimiwa Wabunge wenye *TIN* za biashara wanaelekezwa kuhakiki taarifa zao katika ofisi za mkoa ziliposajiliwa biashara hizo. Uhakiki huo utafanyika kwenye zahanati ya zamani jengo la ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kutumia fursa hii ili muweze kuondokana na usumbufu wa uhakiki wa taarifa zenu za mlipa kodi katika matawi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwani muda uliopangwa unakaribia kwisha. Kwa hiyo, mnaombwa mwende mkahakiki taarifa hizo lakini ni fursa nzuri ya kuitumia ili kuepuka foleni zilizoko nje ya maeneo haya.

Waheshimiwa Wabunge, lingine naona wote tunamwona hapo Mheshimiwa Mbatia. Tunamshukuru Mungu amemrudisha salama. Karibu sana Mheshimiwa Mbatia, tumefurahi kukuona na tunamshukuru Mungu amekurejesha salama ukiwa na afya njema. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo, tunaendelea.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. HUSEEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, uangalie na huku nyuma. Mwisho kabisa huku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja nimekupa nafasi.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68(7). Hivi karibuni Mheshimiwa Spika alitoa mwongozo kuhusu kamata kamata ya Wabunge. Jana majira ya saa tano asubuhi huko Mkoani Morogoro nyumbani kwangu, watu ambao wanajiita kuwa ni askari wakiwa na gari la Polisi, wakiwemo Askari ndani la gari hilo wakiwa na silaha za moto waliizunguka nyumba yangu Mkoani Morogoro kwa

lengo la kunikamata na familia yangu ilipohoji nina kosa gani hawakujibiwa, ila waliambiwa kwamba mimi niko Dodoma kwa shughuli za Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijaribu kumpigia *RCO* wa Mkoa wa Morogoro kumuuliza na akakiri kwamba aliagiza vijana waje kunikamata. Hivi sasa kuna kamata kamata za kila namna na watu wanapotea katika mazingira ya kutatanisha, lakini vile vile kitendo cha askari kwenda na silaha za moto kuizunguka nyumba yangu kimesababisha sintofahamu hata kwa watoto wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama kiongozi, *RCO* angeweza hata kunipigia simu kuniita, hakufanya hivyo! Naomba kurejea Mwongozo wa Spika ambao alisema Bungeni kwamba Wabunge wakiwa kwenye shughuli za Kibunge kama Mbunge anahitajika afuate utaratibu wa kuwasiliana na Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako juu ya hali hii ambayo inaendelea kwa Wabunge kuendelea kuonekana kama si watu ambao wanafanya majukumu yao na kuendelea kutudhalilisha wakati tukiwa kwenye shughuli za Kibunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Naomba mwongozo Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na 64(1)(f) na (g). Naomba nisome hizi (f) na (g), inaanzia kule 64 bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba, naomba nisome (f), inasema; Mbunge hatasema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote na (g); hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya Alhamisi Bungeni hapa Mbunge alitoa maneno ambayo yalikuwa yanadhalilisha, yanaudhi na ni matusi kwa Wabunge na

watu wengine ambao sio Wabunge. Hasa pale aliposema; ninyi CHADEMA mlipomleta Masha na Wenje, ni nani alikuwa mwanamke pale, katika hao wawili nani mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hizi za kuudhi za matusi na za kudhalilisha Wabunge, hasa wa Upinzani zimekuwa zikiendelea kutolewa na Mbunge huyo huyo bila hatua yoyote kuchukuliwa. Amekuwa akitukana, hakuna hatua inayochukuliwa, amekuwa akidhalilisha, hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nipate mwongozo wako, Kanuni hii ya 64(1)(f) na (g) inatumika kwa Wapinzani peke yake au hata Wabunge wengine inawahusu? Kama kweli inatumika kwa Wabunge wa Upinzani peke yao ndiyo wanaochukuliwa hatua pale wanapotoa kauli kama hizi tena hatua kali kweli kweli, Mbunge huyu amekuwa akilindwa na Bunge hili na akitoa kauli hizo hizo za kuudhi na za matusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako tuelewe hii Kanuni ni kwa ajili ya Wapinzani peke yake. Ahsante. Ni Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la dharura.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Natumia Kanuni ya 47(1)(2) na ya (3) na wewe ikikupendeza utatumia Kanuni ndogo ya (4) kuruhusu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niombe shughuli za Bunge ziahirishwe ili tujadili jambo la dharura ambalo limekuwa likitokea kwa muda mrefu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kukitokea matukio ya sintofahamu na sio tu kuhusu Wabunge, hata raia. Kumekuwa na kikundi ambacho kimekuwa kikiteka watu, miongoni mwa watu waliowahi kutekwa ni Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Bashe kwenye Mkutano Mkuu wa CCM, ndugu Malima, Ben Saanane amepotea, juzi ametekwa ndugu Roma Mkatoliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ni jambo la dharura kwa sababu hawa ni wale ambao wanafahamika. Hatujui ni Watanzania wangapi hawafahamiki katika ngazi za chini na zipo taarifa ambazo binafsi nimezipokea kutoka kwa baadhi ya Mawaziri wakinitahadharisha mimi binafsi kwamba Bashe kuwa makini wewe ni mmoja kati ya Wabunge kumi na moja ambao wamewekwa katika *list,* mkikaa barabarani vibaya mnaweza kupoteza maisha yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema jambo hili ni dharura kwa sababu kikundi hiki kilichomo ndani ya Idara ya Usalama wa Taifa ambacho kimeamua kuchukua mamlaka haya ya kuteka watu kinaharibu heshima ya Serikali yetu, kinaharibu heshima ya chama changu ambacho mimi na Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi tuliomba ridhaa ya kutaka kuwaongoza Watanzania na sio kuwahatarishia maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba uruhusu jambo hili tulijadili kama Bunge na ikikupendeza Bunge hili liunde *committee* maalum ya kuweza kuchunguza jambo hili linaloendelea katika nchi yetu, ama kuiagiza Kamati ya Usalama na Mambo ya Nje ya Bunge hili iweze kufanya kazi yake na kutuletea taarifa kwa ajili ya usalama wa wananchi wa nchi hii. Hali ya nchi sio salama, Watanzania wanataharuki, Watanzania wanajadili mambo haya katika mitandao na *there is no statement* ya *hope* kutoka Serikalini... *(Makofi)*

## MWONGOZO

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, naomba ukae. Kanuni ya 47 inataka nikupe nafasi ya kutoa hiyo hoja. Kwa hiyo naomba ukae.

Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ninaomba mwongozo wako kwa kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kujua, kwasababu kuna taarifa ambazo zipo, zinaonesha katika nchi kuna shughuli mbalimbali ambazo zimefungwa na wafanyabiashara wanafunga shughuli zao, mfano maduka, mahoteli na shughuli zingine, zimekuwa zikifungwa na wafanyabiashara wameshindwa kufanya biashara zao na kusababisha Serikali kukosa mapato; lakini mpaka sasa hivi hakuna utatuzi wowote unaoonekana ndani ya Serikali na kwasababu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina kazi ya kuisimamia Serikali. Tunataka kujua sasa, kwamba Bunge linachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba linanusuru tatizo hili ambalo liko katika nchi hii, ili kuhakikisha kwamba wafanyabishara wetu wanafanya biashara pia Serikali inapata mapato kutokana na kodi inazoweza kukusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, asante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakwenda na kanuni namba 47. Taifa limekuwa gizani kwa utamaduni mpya uliozuka, utamaduni wa kuteka watu. Utamaduni ambao sio wa kwetu, ni utamaduni wa kimafia, utamaduni ambao kwa mara ya mwisho kwenye mipaka ya bara na viziwani tuliusikia alipotekwa Mzee Kasi Mhanga Zanzibar miaka hiyo, lakini utamaduni huo haujakuwepo tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini toka operesheni hii ya kuteka nyara ianze, kila anayehusika na usalama likiwemo Jeshi la Polisi *always* wanasema hatujui, hatujawaona kwenye vituo vyote. Nchi inabaki kwenye tahayari, kapotea Ben Sanane, mara miili sita, saba imeokotwa Mto Ruvu, miili ikaendwa kuzikwa bila kufanyiwa *postmortem* kwa amri ambayo hatujui ni ya nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bashe alitekwa, Nape alitekwa akaokolewa na Maulid Kitenge, vinginevyo pengine angekuwa ametekwa lakini hakuna mtu anazungumza kitu. Waziri wa Mambo ya Ndani yuko kimya, mpaka najiuliza kama anabanwa kwa kiasi hicho, huyu ni mtu *potential* ambaye alifikia *ranks* za kugombea Urais na bado ana *future* kwa nini asijiuzulu alinde heshima yake kuliko kukaa kwenye *mess* hii. Kujiuzulu ni utamaduni mzuri, Mzee Mwinyi alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani miaka hiyo, mwaka 1976 ikatokea *mess* akajiuzulu aka- *bounce back* miaka ya 1980 akaja kuwa *president* wa hii nchi, Ndugu yangu Mwigulu nikushauri. Kwa hiyo kama hushirikishwi, mambo yanafanyika hamna mtu anakuja na majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo juzi baada ya kutekwa Roma Mkatoliki tumepata mwanga. Yupo mtu Dar es Salaam alituambia anajua Roma aliko na angerudi kabla ya Jumapili, kama Waziri Kivuli nikatoka Jumamosi ku-*demand* aachiwe siku ile ile na akaachiwa nashukuru Mungu. Sasa basi hatujui nani *next* atatekwa, *it could be me* ingawa mimi *I don't care much* kwa sababu, Mbeya *I got my back. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *it could be you, it's a war nobody served from*, kwa hiyo kwa nini Bunge hili lisijadili hatimaye limlazimishe Bashite kama alivyojua kwamba Roma Mkatoliki yuko wapi na angemrudisha Jumapili, sasa Bunge hili tujadili na baadaye tumlazimishe Bashite atutajie aliko Ben Sanane na atutajie kwamba ile miili iliyotupwa Ruvu na kuzikwa harakaharaka bila *postmortem* ni akina nani kwa sababu huyu anaonekana anajua undani wa mambo haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimeombwa miongozo kadhaa na Waheshimiwa Wabunge. Mwongozo wa kwanza umeombwa na Mheshimiwa Devota Minja, akielezea tukio ambalo limetokea Morogoro, tarehe 9 Aprili, 2017. Kwa maelezo yake Mheshimiwa Devota Minja anasema nyumbani kwake walienda polisi wenye silaha za moto, walikuwa wanataka kumkamata lakini wakataarifiwa kwamba yupo Dodoma. Sasa wakati akijenga hoja yake ameeleza kwamba, naye anafikiri kwa kuwa watu wengine wameshakamatwa katika mazingira ya kutatanisha na akaturudisha kwenye mwongozo ambao Mheshimiwa Spika amewahi kutoa, ama maelekezo aliyowahi kuyatoa kuhusu Wabunge kukamatwa na kwamba Spika lazima ataarifiwe.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza jambo limetokea Morogoro jana, kwa hivyo si jambo ambalo mimi niliyekaa hapa kwamba nina uwezo wa kulitolea mwongozo kwa mujibu wa hii kanuni ya 68(7). Kanuni ya 68(7) inataka mwongozo uombwe kwa jambo lililotokea mapema Bungeni. Kwa sababu hiyo pamoja na maelezo kwamba Mheshimiwa Spika, aliwahi kutoa maelekezo kuhusu yeye kutaarifiwa, hapa hapa Bungeni tuliisoma ile sheria inayohusu Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge na inaeleza ni katika makosa gani Mbunge anapotakiwa kukamatwa Spika atataarifiwa na ni makosa yapi ambayo Mbunge anaweza kukamatwa bila Spika kutaarifiwa. Tulishasoma hapa na si lengo langu kurudia hivyo vifungu. Kwa hiyo, mwongozo wangu kwenye hili ni kwamba kanuni ya 68(7) inanitaka nitoe mwongozo kwa jambo lililotokea mapema Bungeni na hili halijatokea Bungeni.

Mwongozo wa pili nimeombwa na Mheshimiwa Bilago, naye anaeleza kuhusu uvunjwaji wa kanuni ya 64(1) (f) na (g) akitoa maelezo kwamba siku ya Alhamisi, yupo Mbunge ambaye alitumia lugha za kuudhi na kudhalilisha pale ambapo aliuliza maswali kuhusu wagombea waliokuwa wameletwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo.

Ameeleza kwamba je, kanuni hii ambayo inakataza lugha ya kuudhi na kudhalilisha je, inatumika kwa Wapinzani pekee ama kwa watu wote.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kanuni ya 68(7) inanitaka nitoe mwongozo kwa jambo lililotokea Bungeni wakati huo nikiwa mimi nimekaa. Tuelewane Waheshimiwa Wabunge, hizi kanuni tumetunga wenyewe, mwongozo ukisoma hii kanuni kwa nini inasema hivyo, ina maana sana, kwa sababu hutaweza kukitaka kiti kitolee jambo mwongozo ambalo hata chenyewe hakilijui. Huwezi kuomba mwongozo wa kiti kwa jambo ambalo sio chenyewe kilichokuwa kimekaa hapa.

Kwa hiyo tuisome vizuri hii kanuni kama tunaona kuna sababu ya kuiwekea marekebisho, sisi wenyewe ndio tuliotunga na tuirekebishe ili mambo ya wiki iliyopita, mambo ya siku iliyopita yaweze kufanyiwa kazi, lakini kwa kanuni hii tunayoitumia jambo litatolewa mwongozo na yule ambaye wakati huo alikuwa amekaa hapo ama lililotokea siku hiyo, kwa ajili ya kuweza kuonesha namna gani kanuni zimevunjwa. Kwa hiyo mwongozo wangu Mheshimimiwa Bilago jambo lilikuwa la Alhamisi na kama una tatizo nalo utumie kanuni nyingine ili Bunge liweze kushughulika nalo.

Jambo lingine, lililoombwa kuna mambo mawili yanafanana, la Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Mheshimiwa Bashe, kwa hiyo ngoja nijibu mwongozo niliyoombwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka, kuhusu biashara zinazofungwa na kwamba zinakosesha mapato Serikali. Sasa Mheshimiwa Frank Mwakajoka anaomba mwongozo kwa sababu jambo hili ni kana kwamba Serikali iko kimya haijatoa maelezo ni namna gani itaweza kushughulika nalo.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wa jambo hili katika maswali hata yaliyokuwepo leo jambo hili halikuwepo. Kwa hivyo ukilitolea maelezo kwamba mimi nitoe mwongozo leo kwa jambo hili ambalo halijatokea hapa ndani sina huo mwongozo wa kuutoa. Hata hivyo, niseme wazi Naibu Waziri nadhani ni wiki iliyopita alitoa maelezo hapa na Wabunge

wote mlikuwepo kwamba biashara zinafungwa ni kweli, lakini ziko biashara zinazofunguliwa pia. Kwa hiyo, jambo hili halijatokea leo kwa hivyo siwezi mimi kulitolea mwongozo.

Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi wao wametumia kanuni ya 47 wakitoa maelezo kuhusu kuahirisha shughuli za Bunge ili kuweza kujadili jambo la dharura. Jambo hili limeelezwa kwa kirefu na hawa Waheshimiwa wawili niliowataja, lakini linahusu jambo ambalo limekuwa likitokea hapa na pale, ama tumeliona kwenye vyombo vya habari na tumelisoma. Maelezo yao kwa ujumla yanahusu yale mambo yanayowapata wananchi ambayo watu kadhaa wametajwa kama mifano kwamba wamekuwa wakitekwa ama wamekuwa wakikamatwa. Sasa nadhani wote tunafahamu matakwa ya kanuni ya 47.

Hili jambo la hawa watu kukamatwa ama kutekwa kwa sababu sasa hata wale waliokamatwa na wenyewe wamewekwa kwenye kundi la kutekwa; sina uhakika sana kama tunao uwezo wa kutenganisha hayo mambo mawili nani amekamatwa na nani ametekwa; lakini maelezo yaliyotolewa kwa kirefu ni kwamba wakati mwingine mtu akiwa haonekani polisi ndiyo sehemu ya kwanza ambayo inaulizwa na yako mazingira ambayo polisi haijatoa maelezo kwamba hao watu wako wapi na mifano imekwishakutajwa. Mheshimiwa Bashe ameenda mbali zaidi akisema kwamba kipo kikundi ndani ya Idara ya Usalama wa Taifa ambacho kinafanya kazi hiyo,

Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na yeye ameeleza kwamba hili jambo sasa limekuwa kama utamaduni kwa maana ya kwamba linatokea kila wakati na akaenda mbele zaidi na kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aweze kujiuzulu akiona inafaa.

Waheshimiwa Wabunge, kanuni ya 47 huwa ni lazima isomwe na 48 kwa sababu 48 ndiyo inayoweka masharti ya matumizi ya kanuni ya 47. Sasa kwa kuwa kanuni ya 48(4) inasema:-

"J*ambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake.*

Waheshimiwa Wabunge, masuala haya yaliyoulizwa na Mheshimiwa Bashe na pia yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mbilinyi yako chini ya utaratibu wa kisheria na Bunge hili litashughulika na mambo ambayo ni yenye maslahi ambayo sheria haina uwezo wa kuyatolea majibu. Kwa sababu hiyo sitalihesabu hili jambo kwa mujibu wa kanuni ya 47(4) sitalihesabu kwamba ni jambo la dharura lakini ni jambo ambalo utaratibu wa kawaida wa kisheria unaweza ukafanya kazi. Kwa hiyo hayo ndio majibu yangu kuhusu matumizi ya kanuni ya 47.

Baada ya kusema hayo tunaendelea. Katibu!

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Tutaendelea na majadiliano na hapa ninazo orodha kutoka vyama vyote. Nitayasoma hayo majina lakini niwakumbushe kwa sababu katika mjadala Wabunge wengi wakisimama wanapenda kutumia maneno, tena wengine wanachanganya na kingereza ni-*declare interest* ama niseme nina maslahi gani. Kanuni ya 61 inasema utasema una maslahi gani ya kifedha, kwa hiyo usiseme nataka kusema nina maslahi fulani halafu ukashindwa kututajia ni maslahi gani ya kifedha na ni kiasi gani, ndivyo kanuni inavyotutaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo yale maneno tuyaache, tutumie tu muda vizuri kwenye kuchangia. Mtu

anasema niseme nina maslahi kwa sababu ni sehemu ya Kamati sasa hiyo siyo maslahi, lazima utueleze maslahi ya kifedha ndivyo ambavyo kanuni zetu zinataka.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninayo orodha ya kuchangia kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Chama cha Wananchi *CUF* na wachangiaji kutoka Chama cha Mapinduzi. Tutaanza na wachangiaji kutoka Chama cha Wananchi *CUF* na tutaanza na Mheshimiwa Abdallah Ali Mtolea, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuishauri Serikali mambo mawili, matatu. Awali ya yote kwanza niwape pole wananchi wangu wa Temeke kwa changamoto wanazozipata kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha Jijini Dar es Salaam. Niwaombe tu tuendelee kuomba kwamba ziendelee kunyesha mvua zenye neema na wala zisiwe zile zenye balaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maeneo machache hasa katika ukurasa wake wa 15 mpaka ukurasa wa 18 ambapo anazungumzia masula mazima ya uwezeshaji, ajira na mahusiano kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba bado *ratio* ya Watanzania wasiokuwa na ajira imezidi kuongezeka na mpaka sasa takwimu bado zinatuonesha kwamba zaidi ya watu laki nane wanaingia kwenye soko la ajira kila mwaka na takribani watu 50,000 pekee ndio hubahatika kupata nafasi za kazi na hapa haijalishi zile ajira bora au ajira ilimradi ajira. Ukweli bado upo pale pale kwamba hata hao wachache ambao wanapata nafasi za ajira mazingira yao ya kufanya kazi bado ni magumu sana.

Wafanyakazi ambao wanafanya kazi kwenye magodauni, viwandani bado wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wanafanya kazi katika mazingira

ya unyanyasaji mkubwa, wanafanya kazi bila kuwa na *protective gears,* kuwa na vifaa vya kuwazuia na hatari zozote ambazo zinaweza kujitokeza katika mazingira yao ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo bado pia hakuna vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi ambazo zinaweza kutetea maslahi ya wafanyakazi. Naitaka Serikali ihakikishe kwamba kila sehemu ambayo watu wanafanya kazi kuwe na chama cha wafanyakazi. Jambo hili wanapoachiwa wafanyakazi wenyewe wajiundie vyama vyao wanapata changamoto kubwa, wanapata upinzani mkubwa kutoka kwa waajiri kwa sababu waajiri hawataki kuona kuna vyama vya wafanyakazi kwa sababu vitadai maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi ni vizuri akaunda *taskforce* ambayo itasimamia uanzishwaji wa vyama vya wafanyakazi kila eneo ambapo kuna wafanyakazi wanafanya kazi katika eneo hilo, kwa sababu hakuna mtu mwingine wa kuweza kutetea maslahi ya wafanyakazi kama hakuna chama cha wafanyakazi katika hilo eneo husika. Hao ndio watakaoweza kuhakikisha kwamba wafanyakazi maslahi yao yanaboreshwa, lakini pia mazingira yenyewe yanakuwa rafiki na wezeshi kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa sana la fao la kujitoa kwenye mifuko ya hifadhi za jamii. Kumekuwa na kero kubwa na kelele nyingi sana kwa wafanyakazi huko mtaani. Katika Bunge la Kumi ilipitisha sheria hapa ya kuondoa fao la kujitoa kwenye mifuko ya hifadhi ya kijamii. Hili limekuwa ni pigo kubwa sana kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sisi ambao tumefanya kazi katika *private sectors* hatukuwa hata siku moja tuna malengo ya kufanya kazi mpaka uzeeke. Unafanya kazi kwa malengo, kwamba ufanye kazi labda miaka mitano au sita uache kazi uende ukajiajiri mwenyewe. Unategemea baada ya kuacha kazi uende ukalitumie fao

lako la kujitoa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii upate fedha uende ukafanye uwekezaji mwingine, uendeshe maisha yako kwa kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wafanyakazi hawezi kwenda ku-*access* fao la kujitoa eti mpaka wafikishe miaka 55, nani ana uhakika wa kesho? Kwa hiyo yapo mambo mazuri ambayo yamefanywa na Bunge la Kumi lakini yapo pia mambo mabaya ambayo yamefanywa na Bunge la kumi. Ni wajibu sasa wa awamu hii kuyarekebisha yale mabaya kwa maslahi ya wananchi wetu. kwa hiyo, nilikuwa nategemea katika bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri aje hapa na mpango wa kutaka kuileta sheria hiyo Bungeni, ili tuifanyie mabadiliko turudishe fao la kujitoa kwa wafanyakazi katika mifuko ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni kweli Serikali inaamini kwenye yale ambayo inayahubiri, tunahubiri hapa kuijenga Tanzania ya viwanda. Hatuhitaji hivyo viwanda vijengwe na wageni, tunahitaji Watanzania wenyewe ndio waweze kuvijenga viwanda hivyo, ili viwanufaishe Watanzania. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Mheshimiwa Mwijage, anakwambia kwamba, ukiwa na milioni 15, milioni 20, milioni 30 una uwezo wa kuanzisha kiwanda chako.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu ambaye anadai fedha zake *NSSF* au *PPF* ambazo zinaweza kuwa milioni 30 au milioni 40 anaweza kumbe na yeye kuanzisha kiwanda chake. Leo unapomzuwia kuweza kuchukua fedha yake eti mpaka atimize miaka 55 maana yake ni kwamba hamtaki vijana wa nchi hii sasa wamiliki viwanda wakiwa na umri mdogo, sasa, kwa nini Serikali iwazuie vijana kutajirika wakiwa na umri mdogo?. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu ambao wako makazini leo ni kati ya miaka 25 mpaka miaka 35. Kumbe huyu anaweza kupata fedha yake na akaamua kuachana na ajira akaenda kuwekeza kwenye viwanda. Leo Serikali inamzuia mtu huyu asimiliki kiwanda kwa sababu tu eti

hajafikisha miaka 55. Hii haiwezi kuwa sahihi. Kwa hiyo, nizidi kuishauri Serikali ilete hapa hiyo sheria ili tubadilishe turudishe fao la kujitoa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni utumiaji wa dawa za kulevya. Nashukuru sana kwa jitihada ambazo zimeanza za kuanzisha vituo vile vya kutoa dawa za *methadone,* kwa kuwasaidia wale ambao wameathirika na matumizi ya dawa za kulevya ili waweze kuacha matumizi hayo taratibu. Ukweli ni kwamba, inaonekana kama hivyo vituo vilikuwa tu vya majaribio, dawa hizo zinatolewa kwa ubaguzi mkubwa. Waathirika wanapokwenda wanatengwa, wanaambiwa kwamba wale ambao wanatumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga ndio wanapewa hizo dawa za *methadone,* lakini wale ambao bado wanatumia ile njia inayoitwa *cocktail,* wao hawapewi dawa hizo za *methadone. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kinachotokea ni nini; wale wanaotumia *cocktail* ambao na wenyewe wana nia ya kujitoa kwenye dawa za kulevya, wanalazimika sasa na wao kuanza kutumia ile njia ya kujidunga, ili waweze kupata hizo dawa. Hiyo njia ya kujidunga ni njia hatari sana, sasa kama kweli lengo ni kuwasaidia vijana wetu kwa nini tuwabague? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuongeze tuongeze uwezeshaji, tuongeze hizo dawa ziwe za kutosha, ili kila aliyekuwa tayari kuachana na dawa za kulevya aweze kupata hizo dawa na aache, tuache kuwatenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, ni vizuri hivi vituo vikasogezwa karibu na maeneo ya watu. Kwa mfano katika Jimbo la Temeke, sehemu pekee ambazo hizo dawa zinatolewa ni kwenye Hospitali ya Temeke. Sasa kwa nini huduma hii isisogezwe kwenye kila kata? Sisogezwe kwenye kila zahanati kuwe pia na huduma hii ya kutoa hizo dawa za *methadone?* Kwa sababu, hawa waathirika wanapotembea umbali mrefu kuzipata hizi dawa, wakati mwingine wanashindwa kwenda kwa hivyo, wanakatiza zile

dozi. Kwa hiyo, kama lengo la Serikali ni kuwasaidia hawa vijana, basi wahakikishe tunakuwa na dawa za kutosha, lakini pia hivi vituo vinasogea kwenye maeneo ambayo wananchi ndiko wanakotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho nililokuwa nataka kuchangia hapa ni kuhusu utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Kwa masikitiko makubwa sana Ofisi hii ya Msajili wa Vyama vya Siasa katika hizi siku za karibuni imekuwa ni ofisi yenye vituko na kufanya mambo ya ajabu, tofauti na majukumu ya Ofisi hii yanavyotakiwa kufanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia ofisi hii ikiviamulia vyama nani awe kiongozi wa chama hicho kwa vile tu Msajili labda pengine ana maslahi yake binafsi. Sitaki kuzungumzia namna ambavyo amemrudisha Profesa Lipumba, eti awe Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi – *CUF* kwa sababu kesi iko Mahakamani. Pia juzi tu hapa amemrudisha mtu kumfanya awe ndiye makamu mwenyekiti wa Chama cha *NCCR* Mageuzi wakati hakuwa na sifa wala hakustahili kuwa hivyo. Sasa tunataka kuuliza haya mabadiliko ya majukumu na nguvu ya Msajili wa Vyama vya Siasa yametoka wapi na yameanza lini na kwa maslahi ya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyotambua sisi, Msajili wa Vyama vya Siasa ni Karani tu wa kutunza kumbukumbu za vyama vya siasa. Lakini leo anajipa nguvu kubwa na kuvipangia vyama nani aweze kuviongoza. Lakini amekwenda mbali zaidi, juzi hapa kati ameshirikiana na wahuni wachache kutoa ruzuku ya Chama cha Wananchi – *CUF* kuipeleka iende huko mtaani iende ikaliwe. Sasa tunajiuliza, hivi fedha za Serikali ambazo ni fedha za walipa kodi wa nchi hii, zinawezaje kutolewa bila utaratibu na zikaingia mtaani? Serikali... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Michael halafu Mheshimiwa Cecilia Pareso ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nianze kwa kumshukuru zaidi Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na afya na kutuchangia sisi kuwa miongoni mwa waja wake ambao leo wameweza kuendelea na shughuli zao ambazo wamejipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianzie hapo ambapo Mheshimiwa Mtolea ameishia; na hili; mimi bahati niko kwenye Kamati ya Katiba na Sheria; tulilizungumza na tulisema pia kwenye Kikao cha Kamati, kwamba kuna taasisi za Serikali ambazo ziko chini ya ofisi nyingine kubwa za Serikali, utendaji wao kazi unakuwa ni mbaya na mbaya kiasi cha kuweza kuhataraisha hata usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yanayofanywa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa yana hatari kwa sababu, kwanza yanahatarisha hata muungano wetu kwa sababu wanachezea chama ambacho kina nguvu sana upande mmoja wa muungano na chama ambacho kwa sababu yake watu wengi wa upande huo wa muungano waliteseka, walikufa na wengine bado wana vilema vya kudumu mpaka hivi sasa. Anachezea Chama cha Wananchi – *CUF,* taasisi ambayo imeundwa kwa miaka mingi, watu wamejitolea nafsi zao na kila kitu chao kwa ajili ya taasisi hii. Hii ni taasisi kubwa ambayo watu hao hawatakubali kuona inaharibiwa namna hii na watakapofikishwa mwisho, kile ambacho watakifanya kitakuwa na hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema hapa, kwamba hata namna Serikali inavyofanya kazi inatujengea uhasama na inatuvunjia udugu kati ya pande mbili za muungano, kwa sababu upande mmoja unatumia kama ndio *torturing centre* au *camp* ya upande mwingine. Kwa sababu zilitolewa kauli kwenye Bunge hili au na baadhi ya

viongozi wa siasa wa juu kabisa wakasema wanaofanya makosa upande mmoja wa muungano waletwe upande mwingine ambako watashughulikiwa ipasavyo. Hii ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kinachoniumiza zaidi ni ile kuona kwamba hizi taasisi ni *subsidiaries* tu, yaani ni taasisi ndogo, kama nilivyosema mwanzo, zinasimamiwa na taasisi nyingine, lakini Ofisi ya Waziri Mkuu binafsi sioni inafanya nini kukemea ofisi hii ambayo iko chini yake. Msajili wa vyama vya siasa anavuruga, lakini katika majukumu makubwa ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kujenga mahusiano mema kati ya Serikali na vyama vya siasa. Hebu tupate maelezo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, wanalifanyaje hili wakati wanaona wazi Ofisi ya Msajili wa Vyama inavuruga vyama vya siasa, inahatarisha au inaharibu mahusiano mema kati ya Serikali na vyama vya siasa? Tupate maelezo ya kina na hasa katika hili linaloendelea ndani Chama cha Wananchi – *CUF.*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niongeze zaidi kwenye hili itaeleweka zaidi, kwamba, hizi taasisi ambazo ziko chini zinapoachiwa namna hii ndio tunaona hata ufisadi. Tumeambiwa hapa, kwenye ripoti nyingi tu, ya mkaguzi na hata taarifa zinazotolewa na Wizara husika, kwamba kwa mfano mashirika yetu ya umma mengi hayafanyi kazi vizuri au yanafanya kazi katika namna ambayo, zile bodi zenyewe zinashindwa kusimamia mashirika, lakini Wizara mama pia, zinashindwa kusimamia mashirika! Vinginevyo tusingekuwa tunaona taarifa hizi zinazoitwa ma-*scandle* sijui ya *NSSF* na wengine au taasisi kama hizi *security funds* kuwekeza kwenye miradi ambayo haina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, pamoja na kwamba, taasisi hizo zina bodi zao, lakini pia hizi zinakuwa chini ya Wizara mama. Ofisi ya Waziri Mkuu ni mojawapo inasimamia *NSSF,* lakini katika mambo ambayo yalikuwa yamesemwa hapa ya kasoro kiutendaji ni hivyo. Sasa tunajiuliza hivi inakuwaje kwamba, yule anayekabidhiwa ulezi hatazamwi tena yule mtoto anamlea vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, haya yote yanatokea mpaka tukafikia hapo Bodi inawezekana zimeshindwa kufanya kazi, lakini Wizara mama ndio zimeshindwa zaidi kwa sababu, zimeshindwa kuchukua hatua kabla ya kufikia uharibifu mbaya. Nasema tena kwa msisitizo, suala hili linalofanywa na Msajili wa Vyama vya Siasa Ofisi ya Waziri Mkuu iwajibike ipasavyo na itupe maelezo ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine litakuwa ni masuala haya ya ujumla tu, namna gani vijana wa nchi hii wanavyokosa uhakika wa maisha yao na tuna wizara kama hii, lakini wakati mwingine mimi nikasema labda haya maneno yamekuwa mengi kwenye hii Wizara. Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu Wenye Ulemavu, yote haya yako mahali pamoja na sasa hivi naona mwanangu Mheshimiwa Mavunde kabaki peke yake Msaidizi wa Waziri, sasa sijui haya mambo yanakwendaje? Vijana wa nchi hii wanatakiwa kuhakikishiwa usalama wao, wanatakiwa kuhakikishiwa heshima yao, wanatakiwa kuhakikishiwa kweli hiyo tunayoita hawa ndio Taifa la kesho au Taifa *in the making,* basi kweli wawe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitisho wanavyopata vijana wetu sasa hivi vya kutekwa, vya kupotezwa, kwa kweli vinasikitisha. Binafsi niliwahi kuwa karibu na ndugu Ben Saanane, mwanangu Ben Saanane, katika kama siku tatu hivi. Kwa hiyo, kila linapotajwa jina lake hapa mimi naleta picha mama yake Ben, najiweka mimi kwenye nafasi ya mama yake Ben, anafanya nini mwanamke yule sasa hivi? Hebu wanawake wa Bunge hili, tuungane kumdai Ben kwa ajili tu ya mama yake Ben na si kwa sababu nyingine yoyote. Hebu Serikali itwambie kijana huyu na vijana wengine hawa wanaokamatwa na kurushwarushwa kila wakati wanafanyiwa nini na wategemee nini kutoka kwenye nchi yao hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuelezwe vijana wetu na hasa Ben Saanane na nawaomba tena wanawake wa Bunge hili tumsemee mama yake Ben. Kila jina hili likitajwa mimi

naamini wanawake ambao tumepitia *labor ward,* tunarudishwa kwenye machungu yale, kwa hiyo hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi nyingine ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni hii Kamisheni ya Usuluhishi wa Migogoro. Nitatafuta ile kesi mahsusi nitampa mtendaji yule kwa sababu aliniomba, lakini kuna taarifa hizi za jumla pia ambazo nilikuwa naomba sana wazifanyie kazi. Kwamba utendaji wa taasisi hii unaonekana kama vile hausaidii sana upande wa Serikali, kwamba kesi zinazopelekwa kule hazishughulikiwi vile ambavyo tungetarajia. Kwa hiyo, Serikali inabeba mzigo zaidi wa kulipa gharama na fidia kwa ajili ya wale ambao wanakwenda mbele ya Kamisheni hii kwa ajili ya kutatuliwa migogoro yao. Kwa hiyo, hilo naomba pia Serikali itupe maelezo juu ya namna gani hii taasisi nayo inatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niizungumzie Tume ya Uchaguzi. Kama taasisi nyingine zilizo chini ya Ofisi hii na yenyewe nayo ina mazonge yake mengi. Tunashuhudia amani ya nchi hii inahatarishwa sana na ujumla wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa maana ya hizi taasisi zake ndogondogo zilizoko humu. Tume yetu ya Uchaguzi lazima iwe na maelekezo, iwe kwenye nafasi inayostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nathubutu kusema kwamba, uchaguzi wa kuchagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, pia umevurugwa sana na Tume ya Uchaguzi, kwa sababu msimamizi wa uchaguzi ule alikuwa ametwambia kwamba yeye pia alikuwa anataka kupata taarifa zaidi za uthibitisho kwamba, nani ndiye, nani siye kutoka Ofisi ya *NEC.* Inavyoelekea *NEC* ikampa maelezo kwamba kutoka Chama cha Wananchi – *CUF* watu wanne wote wanafaa waje hapa na wagombee na tuliwaona mbele hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napata wasiwasi kwenye taasisi muhimu kama hizi ambazo tunazikabidhi majukumu muhimu kama haya ya kuendesha nchi hii

yanavurugwa, lakini kama nilivyosema tena, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi inayolea haitoi kauli wala haioni kama inaguswa na matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla basi, kama itakuwa kupitishwa bajeti, tunasema ile *value for money* iwe pia kwenye huduma. Je, tunapitisha bajeti kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa huduma hizi inazotoa? Nini inafanya mpaka kweli ituhakikishie sisi kwamba, inastahili kupata pesa hizi kwa ajili ya hizi taasisi zake zifanye kazi wakati huduma yenyewe inayotolewa mimi ninaiita ni chini ya kiwango? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Riziki. Mheshimiwa Raphael Michael atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Pareso, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuanza niipongeze sana Hotuba ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na ningeomba basi Serikali ichukue yale mazuri yote ambayo inaona yanaweza yakaisaidia Serikali kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu nichangie suala la demokrasia. Hotuba ya Waziri Mkuu inaonesha kwamba, hali ya demokrasia katika nchi yetu inaboreshwa, lakini ningependa Serikali ijitathmini kama kweli Taifa hili sasa linasimamia misingi ya demokrasia. Ni vizuri ijitathmini kwa makini kwa sababu, kuna kila viashiria vya kuporomoka kwa misingi ya demokrasia katika nchi yetu, kila viashiria vya kukosekana kwa uhuru wa habari, viashiria vya kukosekana kwa utawala unaofuata sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikajitathmini kwa sababu hata yote yaliyokuwa yanatokea asubuhi hii, yanalalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge, ni kuonesha namna ambavyo misingi ya utawala bora katika Taifa hili imeshaanza kupotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wananchi wanapiga kelele kuhusu marekebisho ya Katiba walikuwa wanaona kwamba wana haki bado ambazo hazijakaa sawasawa katika dhana nzima na muktadha wa demokrasia katika nchi hii, lakini angalau kipindi hicho walipokuwa wakipiga kelele hali ilikuwa ni nafuu kidogo, lakini leo hali imekuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inatuonesha kwamba kuna kuboreshwa kwa hali ya demokrasia na misingi yake katika nchi hii. Naendelea kusisitiza ni vizuri Serikali ijitathmini sana katika suala hili. Haiwezekani leo tuseme kuna misingi ya demokrasia katika nchi hii wakati vyama vya siasa haviruhusiwi kufanya mikutano ya hadhara, likiwa ni jukumu lake la msingi kabisa la kisheria na Serikali imekaa kimya na viongozi wakubwa wa nchi hii wanaunga mkono jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwaje Serikali isijiamini kiasi kwamba leo inakuwa sawa na kumfunga adui yako minyororo mikononi kwenye mti ukampiga kadri unavyoweza halafu ukajisifu kwamba unafanya vizuri. Kwa sababu kama leo unazuia vyama vingine visifanye kazi ya siasa, halafu kuna mtu mmoja peke yake kwa sababu ni Mwenyekiti wa chama kimoja cha nchi hii, kwa kutumia kofia yake aliyonayo ya mamlaka yake anaweza akazunguka nchi nzima akijaribu kuzungumza yale ambayo anatenda yeye, hatakiwi ajibiwe, hatakiwi akosolewe, ni Taifa la namna gani? Demokrasia inakuwa iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo Mheshimiwa Rais anatupa Kauli Mbiu ya HAPA KAZI TU; kwa nini Rais asijue kwamba kazi ya Wanasiasa ni kufanya siasa? Kwa nini hajui kwamba viongozi wa vyama vya siasa wajibu wao, kuanzia kiongozi wa tawi mpaka Taifa ni kufanya siasa? Kwa nini umpangie kiongozi wa kisiasa kufanya vikao vya ndani tu? Kwa nini nchi hii wanasiasa wanaoruhusiwa kufanya kazi wawe ni Wabunge tu, lakini viongozi waliopewa kazi ya

kisiasa, Makatibu, Wenyeviti na Viongozi wengine wazuiwe kufanya kazi zao za kisiasa kwa sababu ya kuogopa vivuli vyetu wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali ijitathmini kama kweli nchi hii inatimiza misingi ya demokrasia. Kama inajiangalia vizuri, vyama vya siasa viruhusiwe kutimiza wajibu wake wa kufanya kazi za kisiasa kwa sababu chama cha siasa ni lazima kinadi sera zake, ni lazima kinadi falsafa yake, ni lazima vinadi itikadi zao, kikiwemo Chama cha Mapinduzi ambacho kinatakiwa kitetee Serikali yake. Vyama vya Upinzani viikosoe Serikali ili Serikali ijitathmini na ijitazame kama iko sawasawa. Sasa kama vitu hivyo haviruhusiwi katika Taifa hili demokrasia iko wapi ndani ya Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani si sahihi Mheshimiwa Waziri Mkuu kusema kwamba misingi ya demokrasia katika Taifa hili inatekelezwa; labda atwambie tumerudisha nchi hii nyuma miaka 40 sasa, jambo ambalo si jema na sio lenye afya katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijiulize, Serikali inajipimaje kwa wananchi wake wa kawaida kama haitaki kusikia kutoka kwingine? Haitaki kusikia wananchi wanasema nini. Mnasubiri tafiti za kitaalam ambazo mara nyingine zinatolewa kwa woga wala haziwezi kuwapa picha nzuri ya namna ambavyo Taifa lipo, lakini hamjui wananchi wa chini wanasema nini kuhusu ninyi; mtawajua kama mtaruhusu *wing* hii ya pili ifanye kazi yake ya kisiasa vizuri, mtasikia malalamiko ya wananchi na mtajua mmekosea wapi na mjirekebishe wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani Serikali inapaswa kutimiza wajibu wake vizuri katika kuhakikisha kwamba inasimamia misingi ya demokrasia katika Taifa hili ili tusije tukaliingiza Taifa hili katika matatizo. Nchi hii yetu sote; tumezaliwa hapa na tutafia hapa, tunapaswa kuipigania katika nyanja zote ili tuhakikishe kwamba wote tunaishi maisha ya furaha katika Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la usalama wa kiuchumi katika nchi hii. Wananchi wanaumia. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inasema kwamba hali ya uchumi na usalama wake uko vizuri. Lakini leo wafanyabiashara hawana uhakika na biashara zako; wafanyabiashara hawajui kwamba kesho kutatoka tamko gani na nani atazungumza nini. Wakulima vile vile hawajui kwamba wanaishi maisha gani yenye uhakika na wafugaji vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inatuonesha kwamba kuna utulivu wa kiuchumi. Leo benki hazikopeshi kwa sababu hazina uwezo wa kukopesha; tunaambiwa kwamba benki zina mitaji na zipo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali pia katika eneo hili ijiangalie na iangalie vizuri kwamba tulipokuwa na tulipo pana tofauti gani, na kwa nini kulikuwa na hali nzuri ya watu kukopa na kukopesheka na kulikuwa na utulivu wa kufanya kazi. Leo maafisa wa *TRA* hujui ni wakati gani watafilisi mwananchi, leo hawajui ni wakati gani benki itafilisi wananchi kwa sababu wananchi hawana uwezo wa kulipa. Sasa katika sura hii tunaendeshaje hii nchi na huu uchumi wa viwanda tutaupata kwa namna gani? Ni lazima Serikali ijipime sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la utalii; Mkoa wa Kilimanjaro umebahatika kupata Mlima Kilimanjaro. Mlima ambao ndio unaowakilisha Taifa hili katika sura ya vivutio vya utalii ambavyo vina heshima duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba Mkoa wa Kilimanjaro Mji wetu wa Moshi upate hadhi ya kuwa Jiji. Nadhani Serikali ingetusikia kilio chetu; haiwezekani Mkoa ambao una kivutio cha utalii ambacho ndio kinachochangia pato kubwa katika sekta ya utalii kuliko kivutio kingine chochote kile ishindwe kupata Jiji kama yalivyo Majiji mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isikie kilio chetu cha kufanya Mji wa Moshi uwe Jiji ili tuweze kuongeza shughuli za utalii katika Mkoa wa Kilimanjaro ili tuweze kuongeza watalii na kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilikuwa naomba Serikali isikie kilio chetu cha kukarabati uwanja wa ndege wa Moshi, uwanja ambao umejengwa tangu wakati wa malkia. Lakini leo imekuwa ni kazi kweli kukarabatiwa mpaka umekuwa ni gofu; eneo lile sasa lipo katika mazingira hatarishi na inawezekana hata watu wakalivamia. Kama lingejengwa ni eneo ambalo lingeinua sana utalii kwani ni uwanja wenye uwezo wa kujiendesha wenyewe. Nilikuwa naomba Serikali itazame kama ina dhamira kweli ya kuinua utalii katika taifa hili na kuinua pato la taifa kupitia utalii na pia kusaidia wananchi wa Kilimanjaro kujiinua katika uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la viwanda. Viwanda vingi vya Moshi vimekufa, na ni vile ambavyo vilibinafsishwa kwa sera mbovu ya ubinafsishaji ambayo imeumiza sana uchumi wa viwanda katika Taifa hili. Sasa naiomba Serikali isimame katika maneno yake, kwamba kwa muda mfupi uwezekanavyo viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa na waliobinafsishiwa wakashindwa kuvifanyia kazi basi wanyang'anywe kama hawawezi kuendelea kuviendeleza na kama wanaweza kuviendeleza waviendeleze ili wananchi wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu viwanda zaidi ya kumi na tano Mkoa wa Kilimanjaro vimekufa lakini tunalalamika hakuna ajira; tunaanza kufikiri ajira za kupitia kwenye mifuko ya vijana na akinamama ya Halmashauri, tunawaza kufikia ajira kupitia Mfuko wa Taifa wa Ajira wa Vijana lakini tuna viwanda ambavyo vipo, vilikuwa vinatengeneza ajira leo vimekufa na Serikali haioneshi jitihada zozote za kuhakikisha ajira zinapatikana. Naomba viwanda vile vifanyiwe kazi, vifunguliwe mapema ili viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Pareso atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Ikupa Stella Alex ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza naunga mkono maoni yaliyotolewa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni na nafikiri Serikali ni vizuri mkayapitia, mkasoma na mkayachukua kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani iliingia kwa mbwembwe nyingi ikijiita ni Serikali ya 'Hapa Kazi tu.' Lakini Serikali hii ya 'Hapa Kazi Tu' pia kupitia hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 11 inasema ili kuboresha demokrasia hapa nchini hatuna budi kujenga jamii inayoheshimu na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Wameandika hivi kwenye vitabu lakini sisi Wabunge na wananchi ni mashahidi kwamba hii Serikali ya hapa kazi ndio Serikali ambayo inavunja katiba, inavunja sheria, haifuati taratibu na haifuati misingi ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi? Sababu zipo nyingi lakini kutaja tu kwa uchache hoja mojawapo tu, leo tunawadhibiti na kuwanyamazisha wananchi na vijana mbalimbali ambao wanatoa maoni yao kwa namna yoyote katika nchi hii. Tunajenga vijana wawe waoga kwenye nchi yao, tunawaziba midomo vijana na wananchi wasitoe maoni yao wakati katiba ya nchi imetoa uhuru huu kwa wananchi kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunavinyima vyama vya siasa visifanye mikutano wakati katiba na sheria zinaruhusu; na uhai wa vyama vya siasa, chama chochote cha siasa ni kufanya mikutano ya hadhara, ni kukutana na wanachama wake. Uhai wa wa vyama vya siasa ni kuongeza wanachama kwa sababu hawa wanachama; ni kama ilivyo makanisa

leo mtu yupo dhehebu hili kesho dhehebu lile vivyo hivyo kwenye vyama vya siasa, leo mtu yupo chama hiki na kesho yupo chama hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuendelea kuimarisha vyama vyetu kwa kuongeza wanachama, tunaongeza wanachama kwa kupitia mikutano ya hadhara; lakini Serikali leo inapiga marufuku mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, inavunja katiba ya nchi iliyojiwekea, inavunja sheria. Sasa ndio tunajiuliza hii ndio hapa kazi kweli ya kuvunja katiba na kuvunja sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo watu wanatekwa, wananchi hawana amani; kwenye mitandao sasa hivi ukisoma wananchi wanasema hata nikienda mahali naaga naenda sehemu fulani kwa sababu sijui kama nitarudi salama au nitatekwa. Tumeshuhudia hapa kuna watu wametekwa wamepotea, hawajulikani walipo, hakuna kauli ya Serikali; hatujasikia kauli nzito inatolewa na Serikali, tunajiuliza kama Serikali imekaa kimya je, ndiyo inayohusika na hili jambo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama na ninyi mngekuwa mnaliona jambo hili kweli linatishia amani ya wananchi mngetoa kauli, hamtoi kauli watu wanatekwa, watu hawajui wanapotelea wapi; hatujui kama kina Ben Sanane haijulikani kama ni wazima au wameshauwawa, haijulikani walipo. Hamuwezi mkajiita hapa kazi tu kwa kufanya hivi vitu; au inawezekana mnajiita hapa kazi kwa kufanya hivyo vitu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Serikali hii kupitia Msajili wa Vyama vya Siasa ilitakiwa ilee hivi vyama vya siasa. Leo mnashabikia ugomvi wa ndani ya Chama cha wananchi *(CUF);* Serikali imechukua upande ina-*support* upande mmoja na kuacha upande mwingine. Wakati wanachama wa chama hicho wanawatambua viongozi ikiwemo Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *CUF* kama ndio Katibu Mkuu wao, lakini Msajili wa Vyama vya Siasa badala ya kulea chama hiki na kuhakikisha mgogoro uliopo unatatulika

wamechukua upande na wanashabikia upande ule ambao wanaharibu Chama cha Wananchi *CUF.* Sasa hii ndio hiyo inayoitwa 'Hapa Kazi Tu'. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Devotha ameeleza hapa asubuhi, hakuna tena ile hadhi ya Ubunge; Mbunge unaonekana si kitu na hasa upande wa upinzani wakati wowote unaweza kuvamiwa nyumbani kwako. Yaani Mbunge ni mtu ambaye anaweza akapotea kwenye nchi hii? Mbunge kama anatakiwa polisi akipewa taarifa ya kwenda kituoni hivi atapotea? Kwa nini tunamchulia Mbunge kama ni mtu ambaye anaweza kupotea? Kwa nini polisi wanatumia madaraka yao vibaya kuwaita Wabunge na kuwataka wakati wowote na kutumia silaha nzito utafikiri Mbunge ni jambazi sugu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Wabunge tutetee hadhi yetu na ni lazima Wabunge tusimame tutetee hadhi ya mhimili wa Bunge; tukisimama hata mhimili wa Serikali nao utaweza kuona kwamba Bunge lina hadhi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya katiba mpya nadhani yapo pale pale, tunahitaji katiba mpya. Rasimu ya katiba mpya ilitengenezwa kwa fedha nyingi za walipa kodi, mmeiweka kapuni, mmeificha na hatusikii tena Serikali ya Awamu ya Tano mkizungumzia suala la katiba mpya. Watanzania wanahitaji katiba mpya; tunahitaji katiba mpya na tunaitaka katiba mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi. Kumekuwa na mifuko mingi sana, kuna hizo asilimia kumi ambazo zinatengwa kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri. Kumekuwa kuna mifuko mingine kupitia Wizara mbalimbali, ya Vijana, ya Fedha na vitu kama hivyo. Kwa nini isifike mahali sasa mifuko hii ikaunganishwa kuliko kuwa na mifuko mingi ambayo inatoa fedha kidogo ambayo mwisho wa siku hata ukipima ufanisi wa hizo fedha haupo kabisa? Kwa nini tusiwe na mfuko mmoja wa pamoja ambao utatoa mikopo kwa vijana, akinamama na makundi mbalimbali ili kuwawezesha kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu ni kuunganisha hii mifuko na kuufanya mfuko mmoja ili iweze kwenda kutoa mikopo kwa wananchi wetu na kuwaimarisha kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 ambayo tunaimalizia mwezi Juni. Bajeti tuliyoipitisha ilikuwa ni ya shilingi trilioni 29.5 lakini mpaka kufikia Februari fedha za maendeleo zilizotolewa kwa Halmashauri na Wizara ni asilimia 35 tu. Sasa asilimia 35 tumebakiza miezi kama miwili kwenda kumaliza mwaka wa fedha; kutakuwa na muujiza gani wa kwenda kukamilisha hizi fedha za maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu ambazo zinaelezwa na Serikali, kwamba kwa nini wameshindwa kufikisha hiyo wanasema kuna fedha za wafadhili nyingine zimechelewa na nyingine hazijatolewa. Wakati tunapitisha bajeti hapa mwaka jana tulieleza athari ya *MCC* na wafadhili wengine kujitoa, mkasimama mkatetea sana hoja hii mkasema nyie mnaweza kujitegemea, mapato yenu ni mazuri na leo hizi ndio athari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine tulikuwa tunaona hizi taarifa Serikali ya Awamu ya Tano mnasema mnakusanya karibu Shilingi trilioni 1.2 kila mwezi. Serikali ya Awamu ya Nne iliyopita ilikuwa inakusanya kati ya bilioni 800 mpaka 900 kila mwezi. Kwa hiyo, ninyi mmejigamba kwamba mnakusanya mapato zaidi kila mwezi halafu siku hizi hata hatuoni hizo taarifa za *TRA* tena; mnajigamba kwamba mnakusanya vizuri kuliko Serikali iliyopita, lakini mnakusanya zinakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu zipo taabani hakuna fedha za maendeleo; wenyewe mnasema mpaka Februari fedha zilizokwenda ni asilimia tano tu, zingine zinaenda wapi? Mnakusanya zinakwenda wapi? Mtafikiaje kutekeleza bajeti hii ya Shilingi trilioni 29 wakati fedha zenyewe hazijakwenda?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine inayotolewa kwamba wananchi hawana uelewa wa walipa kodi, mashine za *EFD;* ni hoja dhaifu sana ambazo zinatolewa na Serikali. Nadhani mnapaswa kutafakari na kutumia taarifa za wataalam ili muweze kufikia haya malengo ambayo yanatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti inayokuja ya mwaka 2017/2018, mnasema mna bajeti ya Shilingi trilioni 31.6; mimi naomba Watanzania muwashangae kama ambavyo mimi naishangaa hii Serikali. Hii ambayo tunamaliza sasa hivi ni trilioni 29 wakati fedha za maendeleo imefika asilimia 35 halafu hiyo *projection* ya 2017/2018 ni Shilingi trilioni 31, hivi kuna muujiza? Kuna Yesu atashuka awaletee fedha nyie mkatekeleze hii bajeti? Kwa kweli inashangaza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka Serikali ituambie mnaenda kufanya mabadiliko gani katika ukusanyaji wa kodi au katika kuimarisha kodi ili hiyo bajeti ya trilioni 31 iweze kufikiwa? Mtupe majibu sahihi. Hata hivyo, kama haifikiwi kama ambavyo hii ya sasa hivi tunamaliza haitafikiwa kwa nini msije na bajeti halisi hata kama itakuwa na kiwango kidogo ambayo inaweza kutekelezeka? Kwa nini mnawafurahisha Watanzania kwa namba kubwa wakati utekelezaji wake unakuwa ni sifuri? Kwa hiyo, tunaomba tuambiwe ni kwa namna gani mnaenda kufanikiwa na bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi

wake kwenye busara wa kuhamisha Wizara zote kuja Makao Makuu Dodoma. Pili, vile vile nimpongeze Waziri mwenye dhamana ndugu yetu Jenister Mhagama kwa kusimamia vizuri wizara hizi; zinaturahisishia sisi kama Wabunge kuweza kupita katika maofisi ambayo yako jirani, kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze na Wizara ya Afya; niiombe sana Serikali ione namna ya kuboresha maboma mbalimbali ambayo tumejenga huko kwenye majimbo yetu hasa zahanati na vituo vya afya ili yaweze kumalizika na kufanya kazi kama ambavyo sera inaelekeza kuwa kila Kijiji na Mtaa kuwa na zahanati na kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na kwenye Jimbo langu; mimi na Waheshimiwa madiwani wenzangu na Serikali tumeweza kujenga zahanati 13 na kituo cha afya kimoja kizuri sana ambacho kimesimamiwa na diwani mmoja anaitwa Mlumbe kutoka pale Yamkeno. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ione namna ya kuboresha vituo hivi ili kusudio lile la kuwa na zahanati na Kituo cha Afya Kilonani iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niishukuru sana Serikali kwa eneo langu la Makambako kwa kutupa vifaa vya upasuaji; naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo imetupa vifaa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maji. Naomba nipate majibu juu ya miradi ile mikubwa ya Miji 17 kwa Wizara hii ya Maji, fedha ambazo zinatoka India, katika miradi hii 17 mikubwa, mmojawapo upo katika Jimbo langu la Makambako. Kwa hiyo, naomba nipate majibu kutoka kwa Serikali, kwamba ni lini sasa fedha hizi zitakuja ili wananchi wa Makambako wawe na matumaini kwamba watapata mradi huu wa maji kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba Waziri mwenye dhamana atakayemteua ataanza kuja Makambako na nashukuru sana Waziri alikuja kama ambavyo Rais alisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo. Niiombe Serikali ione namna ya kuboresha Wizara hii ya Kilimo hasa pembejeo hizi za ruzuku kwa sababu Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi juu ya pembejeo za ruzuku. Nadhani Serikali ione namna ya kupunguza tozo na kodi mbalimbali hasa kwa pembejeo hizi za mbolea ili kusudi kila maduka yauze na mkulima aende kununua kwa bei ambayo ni ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile Serikali ione namna ya kuboresha mbegu. Wako watu ambao wamekuwa wakifanya kazi ya kuchakachua hizi mbegu; wakulima wetu wanapopanda mbegu hizi zimekuwa hazioti. Niiombe sana Wizara kwamba ifufue maeneo ambayo walikuwa wanapanda mbegu kama pale Uyole, Njombe tulikuwa na pale *NDC,* tuna maghala pale na mashamba walikuwa nayo, wafufue suala hili la pembejeo ili wananchi wetu waweze kupata. Kwa hiyo, suala la mbolea nimeshalizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu; niombe sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, pamoja na kazi nzuri anayoifanya, ingawa wapo watu wengine hata ungefanya kazi watasema hakuna kinachofanyika; unajua mtoto wa kambo hata ungemlea namna gani atasema hakuna kazi zinazofanyika; Waziri unafanya kazi nzuri kupitia Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwamba katika ahadi zile za rais za kilometa sita za kujenga lami katika Mji wa Makambako, nikuombe sana na ile kilometa moja ambayo ulisema ingeanza mwaka huu wa 2016/2017 na muda uliobaki ni mfupi, nimwombe sana Waziri ahakikishe kwamba, kilometa sita zile ambazo Rais alisema, mwaka wa 2017/2018 zinajengwa, ile ahadi itekelezwe ili wananchi wangu wa Makambako waweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme. Nikupongeze sana Mheshimiwa Profesa Muhongo, Naibu Waziri wako

pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo tunaiona mnaifanya, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme, kwenye jimbo langu, maana kipindi kilichopita ilikuwa nipate awamu ile ya pili ya *REA;* lakini yule mkandarasi ambaye mlinipa, *Lucky Export* na baadaye mkamwondoa, kwamba hakuwa anakidhi vigezo, sasa mmeniambia mnaniletea mwingine kutokana na majibu ambayo nilimuuliza hapa Naibu Waziri. Niombe sana ahakikishe safari hii mkandarasi huyo anakuwa *site* kule Makambako katika vijiji vile nilivyovitaja ili shughuli hii ya umeme wananchi wangu waweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia. Waziri wa Viwanda yuko hapa na Waziri wa Fedha yuko hapa, Waziri Mkuu alipokuja Makambako aliwaona wale wananchi, yaani mimi Mbunge wao silali. Chonde chonde, niwaombe sana kuhakikisha kwamba tunawapa fidia wananchi hawa kwasababu wameteseka zaidi ya miaka 18. Nikuombe sana, fedha hizi kwa Serikali ni hela ndogo, ili tuhakikishe sasa; kwa sababu na kwenye Bajeti ya Mwaka 2016/2017 walishawekwa; nimwombe sana ndugu yangu Mheshimiwa Mpango tuhakikishe kwamba fedha hizi zinatolewa ili wananchi wangu wa Makambako waweze kupata kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliwaahidi kwamba jamani suala la fidia tutakwenda kulimaliza. Nimwombe sana na mimi namwamini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo. Ndugu yangu Mheshimiwa Mwakyembe uko hapa, Rais alituahidi kutuboreshea uwanja wetu wa michezo, nimwombe katika Mpango wake wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018 ahakikishe anaweka bajeti kwa ajili ya kuanza kutengeneza uwanja wetu wa michezo pale Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu. Niipongeze sana Serikali, tangu ilipokuwa inatoa fedha kwa ajili ya elimu bure watoto wameweza kuongezeka na kadhalika, lazima

tuipongeze Serikali kwa kazi nzuri. Tumwombe Waziri mwenye dhamana kuhakikisha mnapeleka vifaa vya maabara ili watoto wetu waweze kupata elimu yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fedha; tuhakikishe zinakwenda kwa wakati katika halmashauri zetu ili na sisi kama Madiwani tukiwa huko tuweze kusimamia zifanye shughuli za maendeleo kama ambavyo zimepangwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini liko jambo hapa lazima niliseme, nisipolisema hapa nitasema wapi. Wapo Wabunge wenzangu wamesema, hivi iko sheria gani inayosema wewe Mbunge kwa sababu una kinga ukiitukana Serikali usikamatwe, sheria ya wapi? Kama umeitukana Serikali ni lazima ukamatwe upelekwe kwenye vyombo husika ukahojiwe kwa nini umeitukana Serikali. Kwa hiyo tusiweke kama kinga kwa sababu tuna kinga basi tuitukane tu Serikali halafu tusikamatwe, mimi sikubaliani kabisa, lazima tukamatwe, chombo kinachohusika kitufikishe mahali panapohusika. Unajua wako watu walizoea Serikali iliyopita kazi yao ni kuitukana Serikali, lazima tukubaliane na mabadiliko! Wewe unaitukana Serikali wakuache tu, unapita unaitukana Serikali wakuache, haiwezekani! Haiwezekani! Serikali inafanya kazi nzuri, tunaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga. Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmeona uchangiaji wa Mheshimiwa Sanga hata asipopata nafasi huko mbele kashachangia bajeti ya Wizara zote, kwa hiyo tukiiga mfano wake utakuwa ni mzuri zaidi.

Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja ajiandae.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nipende kumshukuru sana Mungu kwa ajili ya kila mmoja wetu aliyeko hapa ndani kwa sababu ni

wengi walitamani kuwepo hapa siku ya leo lakini wameshindwa, si kwamba sisi ni wema sana ila ni kwa rehema tu za Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie fursa hii kutoa pole nyingi sana kwako Mheshimiwa Naibu Spika, Spika wa Bunge lakini pia kwa Wabunge wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Mheshimiwa Dkt. Elly Macha. Kundi la watu wenye ulemavu tumepoteza, Tanzania na duniani kote, kwa sababu ikumbukwe mwaka jana Mheshimiwa Dkt. Elly Macha alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Wasioona Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, mambo aliyoyafanya katika kipindi hiki cha mwaka mmoja ni mengi na yanafahamika. Mheshimiwa Jenista Mhagama pongezi nyingi, Mheshimiwa Dkt. Possi tulikuwa naye na hata sasa hivi ametuachia alama kwamba hata kwenye upitishaji wa sheria mbalimbali watu wenye ulemavu wanaonekana; kwenye uundwaji wa bodi tunaona watu wenye ulemavu tunaonekana, kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Possi ameacha alama. Nimpongeze Mheshimiwa Mavunde, amekuwa pamoja na sisi kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Dkt. Possi ameondoka, amekuwa ni msikivu sana. Kwa hiyo naomba niwapongeze sana kwa utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niishukuru sana Serikali kwa kupatia mwarobaini tatizo la vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kilikuwa ni kilio cha watu wenye ulemavu ama watoto wenye ulemavu lakini Serikali imetoa mwarobaini wake kwa kutatua tatizo hili la vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa asilimia kubwa. Lakini pia katika bajeti ya mwaka huu yapo mambo mengi ambayo yameongezeka ambayo kwa bajeti ya mwaka jana hayakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kuna suala zima, ukisoma kwenye randama ndipo unaona hivi vitu. Wakati napitia randama ndipo nilipoona; kuna suala zima la ununuzi wa madawa, mambo ya ununuzi wa kuni kwa habari ya

vyuo vya watu wenye ulemavu, lakini pia bajeti ya chakula imeongezeka kutoka milioni 38 ya mwaka wa fedha huu tunaoumaliza na kufikia milioni 126 kwa mwaka huu wa fedha ambao ndio tunapitisha sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niipongeze sana Serikali kwa kuwakumbusha tena wakuu wa mikoa kwa habari ya uundwaji wa kamati za watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya kijiji mpaka mkoa. Kwa nini nasema kuwakumbusha tena; Serikali ilishatoa agizo, nakumbuka ilikuwa Januari mwaka huu wakati likijibiwa swali langu la nyongeza, Serikali iliagiza kwamba hizi kamati ziundwe. Sasa ushauri wangu katika hili kuwakumbusha tu haitoshi ama kwa sababu agizo tayari lilishatolewa kikubwa ambacho ningeomba ni kwamba ingetolewa *time frame,* kwamba hizi kamati ziwe zimekwishaundwa ifikapo lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua naomba nitoe mfano mdogo, watu wawili wanaweza wakaja kwangu, mmoja akaniambia Ikupa unatakiwa ufanye kazi hii, akaondoka. Mwingine akaniambia Ikupa ifikapo kesho saa tano asubuhi uwe umekwisha kufanya hii kazi. Kwa vyovyote vile mimi nitafanya haraka sana kwa huyu aliyeniambia kesho ifikapo saa tano asubuhi hii kazi iwe imekwishakamilika. Kwa hiyo, niiombe Serikali itoe *time frame* kwa habari ya huu uundwaji wa hizi kamati ili pia hawa wakuu wa mikoa waweze kujipanga kwa habari ya bajeti na waweze kutoa kipaumbele kwa habari ya uundwaji wa hizi kamati. Muda hautoshi sana kuelezea manufaa ya hizi kamati lakini nafahamu kwamba Waheshimiwa Wabunge mnafahamu na Serikali inafahamu umuhimu wa kamati hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niipongeze Serikali kwa kuvikumbusha vyombo vya habari kuhusu kutumia lugha ya alama ama kuajiri wakalimani wa lugha ya alama. Nasema kuwakumbusha kwa sababu mwaka jana ilishatolewa *time frame* na Waziri mwenye dhamana kwamba ifikapo Machi mwaka huu, 2017, hivi vyombo vya habari viwe tayari vinatumia lugha ya alama ama vimeajiri wakalimani wa lugha ya alama lakini sasa kinachotakiwa

ni ufuatiliaji, kwamba ni chombo gani ambacho kinatumia lugha ya alama na ni chombo gani ambacho hakitumii na ni kwa sababu zipi. Kwa hiyo naishauri Serikali, kikubwa sasa hivi si kuvikumbusha tena bali ni kuvifuatilia kwamba ni vipi vinatumia na vipi havitumii kwasababu zipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee idara ya watu wenye ulemavu. Wakati napitia kwenye randama idara hii haina kifungu na idara hii ina umuhimu mkubwa sana. Tukiongelea vyuo vya watu wenye ulemavu ambavyo sasa hivi ni vyuo vipatavyo vitano vimekwishafungwa na ni vyuo viwili tu ambavyo vinafanya kazi na vyenyewe kwa kusuasua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii ina umuhimu sana, itahudumia vyuo vya watu wenye ulemavu, itahudumia hizi sherehe za Kitaifa za watu wenye ulemavu lakini pia itahudumia mafunzo kwa ajili ya watu wenye ulemavu, jambo ambalo sasa kwa kuinyima idara hii kifungu ama kutokuitengea fedha ina maana inakwamisha ufanisi wa haya mambo ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naendelea kupitia randama inaonekana kwamba hii idara inahudumiwa kwenye hifadhi za jamii; sasa kwenye hifadhi za jamii sio mambo yote ambayo yamekuwa *accommodated,* mengi yameachwa kwa sababu bajeti ya pale naona pia sio kubwa sana. Kwa hiyo niiombe sana Serikali idara hii ni muhimu, ipatiwe kifungu na itengewe fedha ili iweze kufanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee Baraza la Ushauri la watu wenye ulemavu. Baraza hili ni muhimu, kama ambavyo niliuliza swali mwezi Januari na nikajibiwa kwamba litatengewa fedha. Fedha iliyotengwa ni kidogo, ni kiasi cha Shilingi milioni 4.3 tu ndiyo ambayo imetengwa kwenye hili baraza. Fedha hii haitoshi kwa sababu shughuli za baraza ni kubwa, kwa kikao kimoja inaweza ikatumika

shilingi milioni nne mpaka milioni tano, kwa sababu lina wajumbe wapatao 20. Sasa kwa kuitengea shilingi milioni 4.3 hii fedha ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwenye hili eneo la baraza fedha iongezeke angalau ifike hata Shilingi milioni 20, katika Shilingi milioni 20 vikao vinavyofanyika ni vinne. Kwa hiyo, kama vinafanyika vikao vinne ina maana hapo tunakuwa na wastani wa angalau Shilingi milioni tano kwa kila kikao, Shilingi milioni 4.3 ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ikumbukwe kwamba vyanzo vya fedha vya hili baraza mojawapo ni fedha ambazo zinaidhinishwa katika Bunge hili Tukufu na hiki ndicho chanzo pekee cha uhakika vyanzo vingine ni vya wafadhili; wafadhili si chanzo cha uhakika. Nitoe mfano mdogo, mtoto anakuwa na uhakika wa chakula anachopika mama yake nyumbani kwake na si chakula cha kutegemea kwa jirani. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali itoe hizi fedha, iongezee hili baraza fedha angalau ifike hata Shilingi milioni 20 ili tuwe na uhakika kwamba hili baraza litafanya kazi kama ambavyo niliahidiwa Januari wakati swali langu linajibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu. Mfuko huu ni muhimu na hata wakati nachangia mpango mwezi Januari niliongea, kwamba *once* huu Mfuko utakapopatiwa fedha mambo mengi ya watu wenye ulemavu yatakuwa *solved* tofauti na sasa hivi. Unajua tunachoongelea sasa hivi ni kwa sababu hakuna fedha, ni kwa sababu bajeti inayotengwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu inakuwa ni ndogo sana ndiyo maana mambo mengi yanakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba niunge mkono hoja iliyopo Mezani na naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. La kwanza kabisa, kwa niaba ya familia yetu ya marehemu mzee Sitta, nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Serikali nzima, uongozi wa Bunge unaoongozwa na Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa vyama kisiasa, viongozi wa dini, wananchi wote Tanzania kwa jinsi ambavyo walitufariji sana sisi familia ya marehemu Mzee Samuel Sitta; tunawashukuru sana, tunaomba ushirikiano mliotupa sisi uendelee. *(Makofi)*

Mungu ibariki Tanzania, lakini pia tunamwomba Mungu aiweke roho ya marehemu Samuel Sitta mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa kifo cha mwenzetu, Mheshimiwa Dkt. Macha, tumwombe Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu Dkt. Elly Macha mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia katika sekta tatu. Kwanza kabisa naomba nianze na Sekta ya Kilimo. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Urambo, nasema wazi kwamba huwezi kuzungumzia hali ya kiuchumi na maendeleo ya kiuchumi ya wananchi wa Urambo bila kuzungumzia suala la tumbaku. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote mnapoongea mkizungumzia suala hili kwa sababu ni muhimu sana katika maendeleo ya wananchi wa Urambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya wananchi wa Urambo kwa jinsi alivyochukua hatua mbalimbali katika kunusuru zao la tumbaku, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na hatua mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu amezichukua bado kuna maswali ambayo ningeiomba Serikali ichukue hatua za haraka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa Bodi ya Tumbaku imevunjwa, je ni lini Serikali itaunda bodi mpya kwa sababu sasa hivi mwezi wa Nne ndiyo masoko ya tumbaku yanatakiwa yaanze? Pia, pamoja na kuunda bodi mpya, Serikali imejipanga vipi kuiimarisha Bodi mpya ya Tumbaku ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi hususan upatikanaji wa *classifiers,* wale ambao wanapanga tumbaku katika *grades* zinazotakiwa wakati wa kuuza tumbaku na msimu ndiyo huu mwezi wa Nne?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa Serikali itueleze, wakulima wana tozo nyingi, sasa hizi tozo Serikali imejipangaje kuziondoa ili mkulima naye anufaike na zao lake analolihangaikia mwaka mzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati huo huo amri ilitolewa na Serikali ya kuvunja uongozi wa *AMCOS* mbili za Utenge na Nsenda, lakini msimu wa tumbaku umefika, lini Serikali itaondoa amri hiyo ili kuwe na uongozi katika *AMCOS* hizo waweze kushughulikia uuzaji wa tumbaku haraka iwezekanavyo kwa sababu kama nilivyosema mwezi wa Nne ndiyo wanaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tumbaku, tunaiomba sana Serikali itilie mkazo hasa upatikanaji wa mbolea. Tunapoanza na mbolea kuchelewa kutakuwa na matatizo makubwa. Je, wakati huu ambapo Bodi ya Tumbaku imevunjwa nani atakayeshughulikia suala la upatikanaji wa mbolea haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye upande wa changamoto nyingine tuliyonayo, upande wa suala la maji. Sasa hivi sisi Urambo hatuna maji na kuna mpango ambao Serikali imeuandaa wa kupata maji kutoka Malagarasi, lakini utachukua muda mrefu, je, Serikali imejipangaje kipindi hiki ambacho mradi wa Malagarasi unaendelea, hawawezi kutuchimbia visima, hawawezi kutuchimbia mabwawa ili tutumie wakati tukisubiri mradi huu wa maji wa muda mrefu kutoka Mto Malagarasi? Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ifanye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni suala la afya. Ningeiomba Wizara ya Afya kwanza kwa kuanzia hebu ibane halmashauri kwa kushirikiana na viongozi wa halmashauri (TAMISEMI); kwamba ni jinsi gani halmashauri zimepanga fedha hususan kwa ajili ya kuokoa maisha ya mama na mtoto? Kila siku wakati wa kujifungua hapa Tanzania tunapoteza akinamama 30. Je, Serikali kwa kupitia Wizara ya Afya imejipangaje ili kuhakikisha kwamba fedha mahususi zinapangwa kwa ajili ya kuokoa vifo vya akinamama na watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huohuo nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuchagua Jimbo la Urambo au Wilaya ya Urambo kuwa miongoni mwa wilaya ambazo zitapata fedha moja kwa moja kupelekwa kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nauliza moja tu; je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba zahanati zetu zinakuwa na watumishi waliotosha? Kwa mfano, sisi tuna zahanati 21, hamuwezi kuamini katika zahanati 21, 15 hazina maafisa tabibu, sasa wagonjwa wanaandikiwa matibabu na nani? Wakati huo huo upungufu ni asilimia 77, yaani ufanisi wa utumishi ni aslimia 33 tu. Sasa fedha zikipelekwa moja kwa moja kwenye zahanati na vituo vya afya nani anashughulikia fedha hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa ushauri kwamba haraka iwezekanavyo tusaidiwe sisi wa Jimbo la Urambo kupewa wafanyakazi wa kutosha haraka sana ili waweze kutekeleza hili zoezi la kupeleka fedha moja kwa moja kwenye zahanati. Wewe fikiria mahali ambapo kuna watumishi wawili nani anamwangalia mwenzake? Nani anatimiza wajibu wa kuhudumia wagonjwa? Nani anatunza fedha? Kwa hiyo la kwanza ni upatikanaji wa watumishi haraka iwezekanavyo lakini pili, tunaiomba Serikali iajiri wahasibu ili hizi fedha zitakazokuwa zinapelekwa kwenye zahanati ziweze kutunzwa kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, kutokana na uhaba mkubwa watumishi kwa asilimia 77 katika Jimbo langu, naamini na wenzangu wako kwenye matatizo ya hivyo hivyo. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Urambo naomba Wizara husika ituanzishie Chuo pale pale kama ilivyo Nzega na kadhalika ambacho kitafundisha Watumishi wa kada ya kati ili na sisi tupate watumishi haraka iwezekanavyo kutokana na uhaba tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kanda ya Magharibi, ukichulia hasa Mkoa wa Kigoma na Tabora, hatuna Hospitali ya Kanda. Tunachukua nafasi hii kuiomba Serikali na sisi Mkoa wa Kigoma na Tabora tujengewe Hospitali ya Kanda kwa sababu inatubidi kuja Dar es Salaam au kwenda Mwanza wakati wenzetu wanazo karibu kadri iwezekanavyo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa nafikiria kwamba hili suala la upatikanaji wa Watumishi wa Afya, Serikali ilitilie maanani ndugu zangu. Kwa hali ilivyo, kama Serikali haitachukua mkakati maalum, tutapata shida sana kuhusu watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri suala la upungufu wa Watumishi wa Afya liangaliwe ipasavyo na nitashukuru sana. Kama viongozi wetu, Mawaziri mtakuja kwetu kule kama alivyofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuja Tabora kuangalia suala la Tumbaku na Mawaziri husika naomba mje mwangalie uhaba wa watumishi tulionao kwenye Mkoa wetu wa Tabora kwa ujumla lakini pia Wizara Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashukuru kwa kupata nafasi, lakini naomba sana, katika kujumuisha hapa, tupate majibu, lini tumbaku itapata uongozi wa haraka iwezekanavyo? Ile Bodi ya Tumbaku ipate uwezo wa kuajiri wafanyakazi wa kutosha ili masoko sasa yanayoanza mwezi huu yaende kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Emmanuel na Mheshimiwa Papian John wajiande.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema ili nami niweze kushiriki Bunge. Tulikuwa na wenzetu ambao walipenda kushiriki nasi lakini wamepoteza roho zao. Namwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri anazozifanya katika nchi yetu. Kazi zinaonekana, yapo baadhi ya maneno, lakini nasema, unaweza kuwa na macho lakini usione, unaweza kuwa na masikio usisikie; na unaweza kuwa na pua pia ukashindwa kunusa. Ila kubwa naomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu kuhakikisha kwamba analeta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Baraza lake la Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoifanya. Naomba wasonge mbele pamoja na changamoto kubwa, lakini naamini bahari kubwa ndiyo ivukwayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa napenda nichangie baadhi ya maeneo hususan katika suala zima la barabara. Ujenzi wa barabara umeweza kuchochea shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuwezesha hata kuongeza ajira katika baadhi ya maeneo. Pia natambua shughuli kubwa inayofanywa na Wizara ya Ujenzi katika kuhakikisha kwamba inaimarisha miundombinu ya ujenzi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nioneshe masikitiko yangu kuhusu kusahaulika ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Saadani - Bagamoyo. Ahadi ya ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani - Saadani ni ahadi ambayo tangu sijazaliwa mpaka sasa, leo hii nimeingia Bungeni.

**MBUNGE FULANI:** Tangu *primary*.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, alikuja hapa Mheshimiwa Rished miaka 15, ameizungumzia barabara ya Tanga – Pangani – Saadani, lakini Serikali imemwahidi itajenga; amekuja Mheshimiwa Pamba akaambiwa barabara ipo kwenye upembuzi. Leo nimeweza kuibana Serikali, lakini bado inaniambia kwamba Serikali imeonesha nia, itaweza kutengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itambulike kabisa, hata ukitaka kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ni lazima uoneshe nia; lakini ikifika saa 12.00 si unafuturu! Hivi kuna kizungumkuti gani katika kuijenga barabara ya Tanga – Pangani - Saadani?

Mheshimiwa Naibu Spika, binadamu wameumbwa na wivu, binadamu wameumbwa na matamanio; leo tunaona baadhi ya maeneo mbalimbali yanatengenezewa barabara za lami, hivi sisi Pangani tumemkosea nini Mwenyezi Mungu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yetu ya Pangani uchumi wetu tulikuwa tukitegemea zao la mnazi. Mnazi umekufa, lakini leo ili mtu aje Pangani lazima aje kwa makusudi maalum. Tuna Mbuga ya Saadani, lakini wawekezaji au watalii wanashindwa kuja kwa sababu ya miundombinu mibovu ya barabara. Leo tunaona mvua zinazonyesha, shughuli mbalimbali zimekwama. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hitimisho lake, kuna barabara ambazo zimeshafanyiwa upembuzi na usanifu, ni nini mkakati wa Serikai kuhakikisha kwamba inajenga barabara hizi ili sasa turudishe imani kwa wananchi? Wakati mwingine wananchi

wanatupa malalamiko sisi wawakilishi wa wananchi, wanasema tumekuja Bungeni kusinzia na kunywa *juice. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Naomba katika bajeti hii Serikali ihakikishe kwamba inatujengea barabara ya Tanga – Pangani – Saadani. Kama tulikuwa pangoni, sasa na sisi tupae angani ili tuweze kupata maendeleo ya dhati kabisa katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sema mwanangu! *(Makofi)*

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie ni kuhusu suala zima la maji. Tumekuwa na chanzo kikubwa cha maji katika Wilaya yetu ya Pangani. Tuna mto Pangani ambao unatiririsha maji baharini ambao umekata katikati ya mji, lakini tumekuwa na tatizo kubwa la maji. Leo tunaona wananchi wetu wakati mwingine wamepauka; siyo kwamba hawapaki *lotion* wala mafuta, ni kwa sababu tu ya tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuhakikishe katika Wizara hii, Mheshimiwa atupe majibu, ana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanatumia vyanzo hivi vya maji ili kuhakikisha kwamba wanawatua ndoo mama zetu katika suala zima la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie ni kuhusu suala zima la upanuzi wa Shule za Sekondari na Vyuo. Kumesababisha mahitaji makubwa ya ajira hususan kwa vijana wenzetu na tunatambua kabisa sasa hivi kumekuwa na ongezeko kubwa la vijana, lakini wamekuwa na changamoto kubwa ya kukosa ajira. Vijana wenye *degree* wanashinda maskani, hawana shughuli kubwa ya kufanya, lakini natambua shughuli kubwa anazozifanya mama yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Anthony Mavunde

kuhakikisha kabisa vijana wetu wanapata mafunzo, lakini Serikali ione kabisa nia yake ya dhati namna gani tunaenda kutatua tatizo la ajira katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwe na mkakati maalum ambao kutatolewa tamko maalum kwa Halmashauri zilizokuwepo katika Wilaya zetu kuhakikisha kwamba inatengeneza ajira kila mwaka na kutoa taarifa Bungeni ili vijana wetu wenye elimu na wasio na elimu wawe wanapata fursa mbalimbali za ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, naomba Wizara ya ajira iangalie baadhi ya mashamba kuhusu wawekezaji hususan katika mashamba ya Mkonge. Katika Jimbo langu la Pangani tuna mashamba makubwa mawili kwa maana ya shamba la Mwera *Estate* na Sakura *Estate* lakini Watanzania wale maskini ambao wanafanya katika uzalishaji mkubwa wa mikonge, wamekuwa wanapata tabu, wananyanyasika; mikataba yao imekuwa ya ujanja ujanja; hali duni; mazingira mabaya! Kwa hiyo, naiomba Wizara hii, hususan Mheshimiwa Jenista Mhagama apate nafasi ya kupita kule ili kuwapa faraja na waone kwamba na wao ni sehemu ya Tanzania, kwa sababu wamekuwa kama wapo katika ukoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kwa dhati kabisa iende katika maeneo yale ili wawekezaji wale wahakikishe kwamba wanawaboreshea maslahi na kutengeneza ajira ili waweze kunufaika. Wakati mwingine wanaweza kukwambia mkonge haulipi; sasa kama haulipi, kwa nini wasilime mihogo ambayo inaweza ikalipa? Kwa hiyo, unakuta ni ujanja tu wa wawekezaji lakini kubwa tunajua kabisa mkonge unalipa, lakini mkonge uendane na maslahi ya wale wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niipongeze Serikali kuhusu suala zima la elimu bure, lakini pia itambue kuna baadhi ya maeneo katika nchi yetu ilichelewa kuwekeza katika suala zima la elimu. Katika Jimbo langu la Pangani, sisi mpaka mwaka 2005, tulikuwa na shule mbili tu za Serikali,

lakini kwa jitihada ya Serikali kuhakikisha kwamba inatengeneza Shule za Kata, leo hata mimi mtoto wa Mama Ntilie nimefika katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, naipongeza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ni kwamba, tuna changamoto mbalimbali hususan ukosefu wa Walimu wa Sayansi. Naiomba Serikali, ili kuhakikisha katika bajeti hii na sisi tunapatiwa Walimu, sisi miaka ya nyuma katika Wilaya yetu ya Pangani tulikuwa tukiitwa KKY kwa maana ya Kufuma, Kushona, Kupika na Kuzaa ndiyo kazi za watu wa Pangani na kukaa barazani. Kupitia Serikali hii, leo imeweza kuwezesha vijana mbalimbali katika nchi yetu, wameweza kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo ni jambo jema na tutaendelea kuliunga mkono, lakini kubwa tunaiomba Serikali iendelee kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu mizuri na kuhakikisha kwamba inatupatia Walimu wa Sayansi ili siku moja Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli atokee katika Jimbo la Pangani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maneno mengi sana ya kusema, itoshe kusema kwamba naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimwa Emmanuel Papian John na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza leo kwa sababu ni mara ya kwanza kuongea katika Bunge hili la Kumi na Moja, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtoa haki. Pili, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniona, kwa kutambua mchango wangu na kunirejesha Bungeni. Namshukuru sana, namshukuru sana, namshukuru sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nitachangia kitu kimoja tu. Nitachangia ukurasa

wa 21 Kifungu cha 31 kuhusu kilimo. Hotuba yangu itakuwa ni ndefu, kwa hiyo, nusu nitaongea kwenye hotuba ya Waziri Mkuu sitamaliza, nusu nitaongea kwenye Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara ya Kilimo na nitaongea kitu kimoja kuhusu tangawizi. Leo naiongea tangawizi kwa mapana yake. Watu wanaweza wakajiuliza, hii tangawizi ni nini? Wengine hawaelewi tangawizi ni nini. Tangawizi ni zao la viungo *(Spices),* lakini tangawizi ni malighafi ya kutengeneza dawa za binadamu, kutengeneza *cosmetics,* nikiwa na maana ya vipodozi, vinywaji na vitu vingine vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niigawe hii tangawizi katika mafungu matatu; kwanza nitaiongea tangawizi kiulimwengu, kwa Afrika na mwisho nitaiongea kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani hapa, ulimwenguni, nchi bora tano zinazoongoza kwa kulima tangawizi ya kwanza ni India, lakini India inaongoza kwa kulima tangawizi duniani na inayoongoza kwa kutumia tangawizi duniani. Nchi ya pili ni China; ya tatu ni Nepal; na ya nne ni Nigeria. Ni nchi ya Kiafrika hii na inalima tangawizi kweli na ina-*export* tangawizi kwa wingi mno.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnasoma vitabu vya kilimo, utakuta kwamba Nigeria imekuwa inategemea zao la tangawizi kwa *export* mpaka ilipofika mwaka 1960 ndipo ilipogundua mafuta, ikawa mafuta yako juu kwa tangawizi. Sisi huku, nikisema tangawizi, watu wanasema, "huyu naye na tangawizi!" Tangawizi ni zao zuri sana na lina *export* nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya nne ni Nigeria kwa hiyo ni ya kwanza kwa Afrika. Nchi ya tano ni Thailand. Nisiishie hapo kwa upande wa ulimwengu, twendeni tuangalie nchi zinazo- *export* tangawizi kwa wingi. Sasa kwa sababu India inalima tangawizi kwa wingi, lakini anai-*consume* yeye mwenyewe sana. Ameshindwa kuwa wa

kwanza kwenye ku-*export.* Nchi ya kwanza inayo-*export* tangawizi kwa wingi ni China; ya pili inakuja kuwa India; ya tatu, watu hawataamini, Nigeria ni *giant number three* kwa ku-*export* tangawizi; ya nne inakuwa ni German na Netherland.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi Afrika. Nilitaka kutoa picha ya tangawizi na ulimwengu kidogo tu. Twende Afrika sasa. Nigeria inaongoza kwa kulima tangawizi Afrika. Nigeria inajipambanua kwamba kwa nini inaongoza kulima tangawizi na ku-*export?* Inasema kwa nini inafanya hivyo? Kwa nini imeweza? Inasema ina ardhi kubwa sana yenye rutuba; inasema, ina mvua za kutosha na mito isiyokauka, lakini inasema ina hali ya hewa nzuri, ndiyo maana imeweza kuwa na *comperative advantage* upande wa tangawizi kuliko nchi zote za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Nigeria imefika hapo, kwamba ina-*export* tangawizi inapeleka *USA, Europe,* Morocco na nchi nyingi tu. Kitu cha ajabu, yenyewe kama Taifa inakubali kwamba wakulima wakubwa wa tangawizi kwa Nigeria asilimia 40 ni wanawake. Wanawake wa Nigeria ndio walioshika mashamba makubwa ya tangawizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hali ya hewa ya Nigeria, nakubali ni nzuri; ardhi ya Nigeria, nakubali ni nzuri. Ile hali ya hewa ya Nigeria ambayo imeruhusu kulima tangawizi, ipo Tanzania! Ukisema mvua, Tanzania tuna mvua; ukizungumza mito isiyokauka; tunayo, twende tuone mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Mkoa wa Ruvuma kuna mvua ya kutosha; Mkoa wa Njombe una mvua ya kutosha; Mbeya ina mvua ya kutosha, Rukwa na kigoma; Tanzania haina maana kwamba hatuna sehemu zenye hali ya hewa nzuri, haina maana kwamba hatuna mito ya kutosha, haina maana kwamba hatuna ardhi ya kutosha. Kwa nini wenzetu wamefanikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Nigeria imethamini zao la tangawizi, imekwenda imesimama imara

kwenye zao la Tangawizi, lakini kwetu sisi, Kipare tuna methali inasema, *"Ng'ombe kuramoshe ukuhundue."* Ina maana Ng'ombe anajipeleka mwenyewe machungani, anajirudisha mwenyewe. Wakulima wa Tanzania wanaolima tangawizi wako wenyewe. Serikali haijasimama imara ikalishika hili zao, ikatayarisha *project* maalum ya ku-*study* hili zao la tangawizi na ikasimama imara ikatafuta hili zao wapi tutalilima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa na Tanzania ya viwanda kama hatutakuwa na kilimo bora, hatuwezi. Itakuwa tunasema, Tanzania ya viwanda, Tanzania ya viwanda! Ni lazima tukaboreshe kwanza kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nitaliongea miaka mitatu na nusu. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Jimbo langu sasa ni Tangawizi. Nitazunguka nchi nzima kuhakikisha naboresha kilimo cha Tanzania na nina uhakika Serikali mtaniunga mkono kila siku. Ofisi nitakayokwenda kuiona mimi ni Ofisi ya Wizara ya Kilimo. Nitakwenda, nitashauri, nitapita, nitakwenda, nitarudi. Serikali naomba zao la tangawizi hebu tuliangalie, tukae, tuandike *project,* tutafute wenzetu wa Nigeria, twende tukai-*visit* Nigeria; siyo lazima mtulipie nauli, tutalipa wenyewe. Mimi nitakwenda Kaduna nikajue kwa nini Kaduna wanalima tangawizi kwa wingi? Nitafanya hiyo kazi. Hatuwezi kuzungumza suala la viwanda kwa nguvu, tutafika, lazima tujenge viwanda; kilimo kiko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze ukweli; zao la tangawizi ndugu zangu, ukiona Muhindi, ni *very aggressive* huku duniani; Mchina ni *very aggressive;* M-Nigeria ni *very aggressive;* kwa nini haya Mataifa matatu yanasimama kulima tangawizi? Wanajua faida yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo, naomba niishie nusu ya hotuba yangu. Wizara ya Kilimo, naendelea na zao la tangawizi na nitachangia kwa maandishi, nitamletea Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kabla sijamaliza, nirudi niseme naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nilikuwa nje

kwa mwaka mmoja na miezi kadhaa. Nilikuwa nawaangalia mnavyochacharika, Serikali mnafanya kazi sana, lakini naomba mwongeze nguvu kwenye kilimo cha Tanzania. Ni lazima tuondoke hapa tulipo. Tutaondoka tu kama tutakuwa na viwanda vya uhakika. Hilo linawezekana iwapo tutashirikiana wote tena tukitaka kujenga nchi vizuri, tushirikiane bila kujali itikadi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Papian John atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Hassan Elias Masala ajiandae.

**MHE. EMMANUEL J. PAPIAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya na jinsi anavyosukuma gurudumu la maendeleo kwenye nchi yetu. Siku zilizopita kwenye mwaka 2010 - 2015 wenzetu wa Kambi ya Upinzani walikuwa wanasifia sana utendaji wa Kagame. Walikuwa wanasifia sana jinsi anavyochapa kazi na jinsi ambavyo amenyanyua Shirika la Ndege; na *ATC* yetu imekufa wakiwa wanalaani pamoja na Rais wetu Mstaafu JK. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashangaa leo, Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amenunua ndege za kutosha, leo anapingwa. Jambo lingine ni kwamba, wakati wanasema anashauriwa na Kagame, wakati anajenga barabara Magufuli akiwa Waziri, swali ni je, alikuwa anashauriwa na Kagame? Wakati anakamata meli zilizokuwa zinatuibia samaki kwenye bahari kuu, alikuwa anashauriwa na Kagame? Nawaomba, mkikumbuka kudanganya siku nyingine mkumbuke pia namna gani ya kujibu hoja zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie jambo dogo tu la Utawala Bora. Leo Jimboni kwangu Kiteto siyo salama sana. Siyo salama kwa sababu ya utawala bora tu, ambao tuna-*miss* watu ambao kwenye sehemu zao hawafanyi ipasavyo. Kiteto kulitokea mauaji na sasa baada

ya Waziri Mkuu kutoka juzi tu miezi miwili wameshakufa watu wawili. Mashamba yameshachomwa zaidi ya thelathini. Tuna viongozi; tuna Mkoa, tuna Wilaya, tuna *OCD* tuna Mahakama na tuna Ofisi ya *DC.* Kwa nini vitendo hivi vinaendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niambiwe kwa nini vitendo hivi vinaendelea na Serikali haijachukua hatua? Suala hili ni uzembe wa Watendaji wetu. *Excuse* ndiyo nyingi. Unaambiwa wamekamamatwa ugoni, wameshikana wapi, lakina umma uliteketea. Siku za hivi karibuni, hapa Jimbo la Kibajaji waliuawa wananchi watatu. Kile kijiji watu walitawanywa, walikamatwa, waliwekwa ndani na Serikali ilionesha jitihada zake. Kwa nini Kiteto hizi jitihada hazifanyiki ili mauaji yaweze kukoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, Kiteto kuna watu wanafikiri kwamba ile amani ilitengenezwa tu. Hata wakati mauaji yanaendelea, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilikuwepo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ilikuwepo, Watendaji wote wa Serikali walikuwepo. Leo wanatumia *camouflage* kwamba wametengeneza. Wakati ule Mbunge alikuwa anaunga mkono hiyo hoja, *DC* aliyekuwepo alikuwa anaunga mkono, ofisi nzima, ndiyo maana umma uliteketea. Leo amani ipo kwa sababu tumefanya *changes* za utawala wa pale. Kila anaponyanyuka, nipo. Leo nimetengenezewa zengwe, nashughulikiwa. Nami watakaoshughulikiwa kukamatwa au kuwekwa ndani yawezekana nami nimo. Mimi nitakwenda kama Mandella. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukihisi kwamba naweza kudanganya na kusema uongo, siyo sehemu. Ukihisi kwamba naweza kuulinda uovu, siyo sehemu! Kiteto chama pekee, Kamati ya Siasa ya Wilaya ndiyo iliyookoa na kulaani vitendo viovu na Serikali ilikuwepo. Waziri Mkuu aliunda Tume; tunaomba ile ripoti itoke. Ile ripoti ina mambo mengi ndani yake. Ile ripoti itoke kwa sababu gharama ya Serikali imetumika, lakini kumefanyika *heavy investigation* juu ya matukio yaliyosababisha ile hali kuwa pale. Inaonesha vitendo vingi ambavyo vimefanywa na baadhi ya Watendaji mle ndani katika ile ripoti. Inaonesha *involvement* ya wale

wanasiasa waliofanya hayo mambo pale ili itusaidie *way forward* tujue namna gani ya kukabiliana na matatizo yaliyoko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, Kiteto wanasema imevamiwa sana. Leo wanafukuza watu kule, amani inaanza kupungua. Mtu amekaa miaka 20 au 15, maisha yake yako kule, hajui kwingine kwa kwenda, leo anaambiwa aondoke, anakwenda wapi? Wanasema ni wavamizi, lakini wanasahau kwamba leo wale tunaowafukuza kule; leo Wilaya yangu nusu ya wafugaji wako Kilindi kwa Mheshimiwa Omari Kigua, naye awafukuze?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapozungumza, Kata yangu ya Dosidosi inayopakana na Kongwa, robo tatu ya wakulima wake wanalima Kongwa wakati ni wananchi wa Kiteto. Leo tuwafukuze? Wana zaidi ya miaka 30. Ukikaa unaulizwa, "ehee, leteni *document* ya shamba; hili shamba lako ulilipata lini?" Mtu ana miaka 30, ameoa, ana wajukuu analima Kongwa; ni mwananchi wa Dosidosi Wilaya ya Kiteto. Leo tufukuze watu kwa miaka 20 waliyokaa pale; kisa ni nini? Kwa sababu kuna mazingira ya rushwa, kwa sababu kuna ukabila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba mkubaliane nami, Bunge hili ikitokea kafa mtu Kiteto, namba msimame tuahirishe Bunge tuendelee na mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishakutana na vitu vigumu sana kwenye yale mazingira. Ukiona mgogoro hauishi, jua kuna watu wanachochoea huo mgogoro.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. EMMANUEL J. PAPIAN:** Jamani!

**MBUNGE FULANI:** Muda umekwisha.

**MHE. EMMANUEL J. PAPIAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamedi Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Elias Masala na Mheshimiwa Khatib Said Haji ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wake, dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama na ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini kwa kuwasilisha hotuba yao nzuri yenye mwelekeo wa kazi kwa kipindi hiki cha mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana ndugu yangu Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli amefanya kazi nzuri kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja, nasi wananchi wa Lindi tuna matumaini makubwa na yeye na tuko nyuma yake katika kuunga mkono jitihada kubwa anazozifanya katika kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuchangia katika hotuba yake ambayo ameiwasilisha Mheshimiwa Waziri wetu. Naipongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa inayoifanya ya kuongeza kukuza uchumi, lakini kupunguza umaskini wa wananchi wetu katika kuboresha sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Mawasiliano, Ujenzi wa barabara, Bandari, reli, viwanja vya ndege na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia namna ambavyo Serikali inaendelea kuboresha miundombinu yetu hasa ya barabara na hasa tukiangalia Jiji la Dar es Salaam tumeshuhudia msongamano wa magari unavyoendelea kupungua. Hizi ni jitihada kubwa sana ambazo zinafanywa na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada hizi za kuunganisha barabara za mikoa na mikoa na kuendelea kukarabati barabara hizi, ni vizuri sana tukaangalia katika Mkoa wetu wa Lindi kutoka Dar es Salaam, barabara inayokwenda Lindi kuna maeneo ambayo sasa hivi yanasumbua sana. Ukitokea hoteli tatu kwenda Mbwemkuru kuna maeneo yana mashimo mengi sana kiasi kwamba magari hayawezi kupita vizuri. Hata Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania alipokuja katika ziara yake Mkoa wa Lindi aliona namna ambavyo barabara ile imeharibika hata kama mashimo yale yalitiwa kifusi kidogo, lakini hali ilikuwa siyo shwari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba barabara hii waitazame kwa sababu kwa kweli tumehangaika katika kipindi kirefu sana tangu uhuru upatikane, lakini tunaishukuru Serikali yetu imejitahidi kuiwezesha barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iendelee kuiangalia vizuri ili iendelee kutuhudumia wananchi wa Mikoa hii ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 30 ameongelea vivuko na usafiri majini. Napenda kuishukuru sana Serikali kwamba katika kipindi cha Bajeti hii ambayo tunaimalizia katika eneo la Lindi Manispaa, tulipata pesa shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kujenga kivuko cha Lindi – Kitunda, lakini hatuoni chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kitunda wanahangaika sana hasa wanawake, pindi anaposhindwa kujifungua na analazimika kuja katika hospitali kubwa ya Mkoa kufanyiwa *operation* namna ya kumsafirisha mtu huyu ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ituangalie, itusaidie kwa nguvu zote ili tuweze kupata kivuko kiweze kutusaidia wananchi wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi huu wa *LNG,* uchakataji wa gesi katika eneo hili la Lindi Manispaa, Kata ya Mbanja, Kijiji cha Likong'o. Eneo hili lilishapimwa na

lilishatolewa hatimiliki ya eneo lile na wananchi sasa hawana uhakika tena wa wao kuendelea kuishi pale, lakini wananchi wale hawajapewa fidia zao mpaka leo.

Kwa hiyo, naiomba Serikali kuharakisha kwa sababu eneo lile limekuwa siyo lao tena na limeshakuwa sasa ni miliki ya Serikali kupitia Shirika hili la Mafuta. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu sikivu kuwasaidia wananchi hawa ili waweze kupata fidia na wao waweze kujiendeleza katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa sana katika kuwawezesha vijana wetu kupata mafunzo ya stadi za kazi na ujuzi ili na wao waweze kushiriki katika uendelezaji au uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana katika Mkoa wetu wa Lindi tumebahatika kupata Chuo cha *VETA* na kipo katika eneo la Lindi Manispaa. Tunajua Sera ya Elimu ni kujenga vyuo kila Wilaya, lakini kutokana na uchumi tuliokuwa nao, itachukua muda mrefu sana kuweza kuwa na Chuo cha *VETA* kila Wilaya. Ombi langu kwa Serikali ni kwamba, chuo hiki kimekuwa kinatoa mafunzo mengi sana pale Lindi, lakini vijana wanaoshiriki ni wachache sana kwa sababu ya ukata wa maisha. Chuo kina changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hakina mabweni ya kulala wanafunzi, lakini nyumba za Walimu na miundombinu pia ya maji machafu imekuwa ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, tuna imani kubwa na Serikali hii. Tunaomba itusaidie sana katika kuhakikisha Chuo kile kinakuwa na mabweni ya kulala wanafunzi ili ndugu zetu wanaoishi katika Wilaya nyingine ikiwemo Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Kilwa, Lindi Vijijini nao waweze kushiriki katika kupata mafunzo katika chuo kile cha *VETA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine kubwa sana; wanafunzi wanaosoma pale wanaishi katika

nyumba za watu binafsi wakilipa pango, kwa hiyo, imekuwa ni changamoto kubwa sana. Wanajilipia pango wenyewe, lakini hata gharama za maisha za kuishi ni za kwao wenyewe. Kwa hiyo, imekuwa ni changamoto kubwa sana na wazazi wengi wanashindwa kuleta wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itusaidie wakati mipango mingine; mipango ya muda mrefu inaendelea ya kutujengea mabweni, basi ihakikishe inatoa gharama ya chakula kuwapunguzia ukali wa maisha wanafunzi ambao wanasoma pale na nina imani mkitusaidia kutuchangia gharama za chakula, basi wanafunzi wa maeneo mengine ya Wilaya nyingine wataweza kushiriki katika kuja kusoma mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya na *Plan International,* tunao mradi wa *YEE.* Mradi huu unafanya vizuri sana katika eneo letu la Lindi Manispaa na Lindi Vijijini. Kwa hiyo, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Elias Masala, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda atamalizia.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafsi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Serikali yake kwa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mafanikio makubwa yameonekana ndani ya mwaka mmoja ambao tunakwenda kujadili bajeti ya Awamu ya Pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni kilimo, kama ambavyo limezungumziwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nataka nijielekeze katika kilimo cha zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako baadhi ya mapendekezo ambayo nilitaka niyatoe ili kuweza kuboresha Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Kwanza tunaipongeza Serikali, mwaka 2016 tulileta hoja hapa za kuondoa tozo ambazo zilikuwa ni kikwazo kwa wakulima wetu. Takriban tozo tano ziliondolewa na hii ilipelekea kuweza kupata bei kubwa mpaka kufikia 3,800 kwa zao la korosho. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nachingwea na wananchi wa Kusini kwa ujumla, tunaomba tuseme ahsante kwa Serikali yetu sikivu kwa kufuatiliwa kilio chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, mambo ambayo nilitaka niboreshe kwanza ni eneo la ucheleweshaji wa malipo. Minada imekuwa inafanyika na kwa mujibu wa *catalogue* za ufanyikaji wa minada, minada ile ilikuwa inatakiwa malipo yafanyike ndani ya siku zisizopungua sita, lakini kwa bahati mbaya makampuni mengi ambayo yalikuwa yanashinda zabuni ya kuchukua korosho za wakulima walikuwa wanachelewesha malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo ninapozungumza, toka mwezi wa Kumi na Moja kuna baadhi ya wakulima ndani ya eneo langu na maeneo ya Kusini baadhi, bado hawajapata malipo yao. Kwa hiyo, hii ni sehemu ya kero ambayo nafikiri Wizara pamoja na wadau wote wa zao la korosho lazima tujitahidi kurekebisha kasoro hizi ili mfumo uweze kuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo napenda kushauri ni suala zima la usajili wa vyama, hasa Vyama Vikuu wa Ushirika. Kwa Jimbo langu la Nachingwea tunatumia Chama Kikuu cha Lunali. Chama hiki kinajumuisha Ruangwa, Nachingwea pamoja na Liwale. Naomba

nichukue nafasi hii kuwashukuru watu wa kilimo kwa sababu tayari wameshaanza kuonesha utashi wa kwenda kusajili mara baada ya kukamilisha taratibu za kufilisi Chama Kikuu cha llulu ambacho kilikuwa kinahudumia wakulima wa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kupitia bajeti tunayoenda kuijadili, jambo hili litiliwe mkazo, sisi tunaotumia chama ambapo sasa hivi ni Kamati ya muda, tuweze kupata chama kikuu ambacho kitaenda kusimamia maslahi ya wakulima wa zao la korosho kabla hatujaingia katika msimu wa korosho ndani ya mwezi wa Kumi kuanzia mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ambalo nataka nishauri pia katika kilimo ni eneo la ajira kwa Watendaji. Kwa kipindi cha nyuma, kabla ya mfumo haujaboreshwa, Watendaji wengi ambao walikuwa wamechukuliwa katika Vyama vya Ushirika ni wale ambao hawakuwa na uwezo lakini pia hawakuwa na elimu ya utunzaji wa fedha. Mzunguko wa fedha katika msimu wa mwaka huu, umefikia siyo chini ya shilingi bilioni 40 katika Mkoa wa Lindi. Ukiangalia Watendaji ambao wanatoa fedha kwa wakulima, uwezo wao ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu mapato yamekua na fedha imeongezeka, naomba niishauri Wizara ya Kilimo itoe maelekezo kwa Vyama vyote Vikuu vya Ushirika na Vyama vya Msingi vitoe ajira kwa watu ambao wana elimu ya utunzaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nina vyama vitatu ndani ya Jimbo langu, wahasibu wake wana kesi, wamepelekwa Mahakamani kwa sababu ya kupoteza fedha za wakulima na hii yote ni kwa sababu walishindwa kutoa fedha kwa taratibu za kifedha jinsi inavyotaka. Kwa hiyo, ili tuweze kuwasaidia vizuri, ni lazima ajira sasa za wale Wahasibu wa hivi vyama zitolewe kwa watu ambao angalau wana elimu ambayo itaweza kuwasaidia kuweza kutunza fedha za wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilitaka nishauri katika kilimo ni suala la usimamizi wa tozo ambazo zimeondolewa. Ziko tozo katika zile tozo tano, bado mwaka huu, katika msimu huu zimeendelea kufanya kazi. Kwa mfano, iko tozo ya usafiri iliondolewa na hii tozo iliondolewa kwa sababu tulishauri maghala yatakayotumika, yatumike yale ambayo yako katika ngazi ya Vijiji pamoja na Kata. Bahati mbaya kutokana na kuchelewa kuanza kwa msimu, maghala yaliyotumika ni maghala makuu tu. Kwa hiyo, tozo ya usafiri ikalazimika kurudi tena na hivyo kuwakata wakulima kinyume na makubaliano na sheria ambayo tayari tulishaipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo naomba hili tulichukue, safari hii tungependa kuona maghala yote katika ngazi ya Kata, Vijiji yanakarabatiwa mapema iwezekavyo ili tozo hii ambayo ilijirudia, isijirudie tena katika msimu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho katika kilimo ni suala zima la pembejeo za ruzuku. Mwaka 2016 kwa maana ya msimu huu wa kilimo, Mkoa wa Lindi peke yake tumepokea tani 80. Themanini ukigawanya katika wilaya sita maana yake ni takriban kila wilaya ilikuwa inaenda kupata tani zisizopungua 20 mpaka 18, kitu ambacho ilikuwa ni utani mkubwa sana. Sasa hili naomba watu wa Wizara waliangalie; tunataka kilimo, tunataka tuimarishe viwanda; unapoleta mbegu tani 80 kwa mkoa mzima, ukagawanywe kwa wilaya sita, kwa kweli hii imetushangaza sana, hatujajua tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba watakapokwenda kujumuisha, watuambie kwa nini Mkoa wa Lindi safari hii tani za mbolea na mbegu za ruzuku ambazo mpaka sasa hivi ninavyozungumza zimeshindwa kwenda kwa wakulima, hazijaletwa kwa wingi kama ilivyo mikoa mingine ukilinganisha na Iringa na Mbeya ambako wamepeleka ziadi ya tani 1,000 wakati Mkoa wa Lindi na Mtwara, jumla yake

tani hata 200 hazifiki? Hili tunaomba tupate ufafanuzi ili tujue kama Mkoa wa Lindi na Mtwara kwa sasa hivi hatushiriki kilimo au kuna jambo gani ambalo linaenda kujitokeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo napenda kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu ni eneo la maji. Naipongeza Wizara ya Maji, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu wake; walikuja Jimboni kwetu Nachingwea wameona hali halisi. Tunao mradi mkubwa wa maji ya Mbwinji pale Nachingwea sasa hivi, unafanya kazi nzuri. Moja ya ahadi ambayo ilitolewa ni kuhakikisha maji yanasambazwa umbali wa kilomita tano katika vijiji vinavyozunguka yale maeneo ya chanzo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii tunayoenda kuimalizia, jumla ya shilingi bilioni moja ilitengwa. Shilingi bilioni moja hii ilitakiwa itumike kwa watu wa Masasi, Nachingwea pamoja na Ruangwa. Ndani na Wilaya ya Nachingwea tumepata vijiji sita; tuna kijiji cha Naipanga, Mtepeche, Mkotokuyana, Mandai pamoja na Chemchem.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate ufafanuzi wakati unapokwenda kujumuisha kiasi hiki cha fedha ambacho tayari mchakato wa kumpata mkandarasi umeshafanyika, ni lini sasa mradi huu unaenda kutekelezwa ili wananchi wa haya maeneo niliyoyataja waweze kupata maji safi na maji salama ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu ambao kwa kweli wanateseka kwa adha ya kupata maji umbali mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo napenda kuchangia katika hotuba hii ni suala la barabara. Mheshimiwa Rais alipofika Nachingwea, alitoa ahadi ya kusimamia, kuhakikisha ujenzi wa barabara ya Nachingwea - Masasi, Nachingwea - Nanganga inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 niliposimama hapa kuuliza swali, niliomba kupata ufafanuzi kwa sababu *feasibility study* ilishakamilika, ni lini barabara hii itajengwa?

Bahati mbaya tulipata shilingi bilioni moja; naomba kupitia bajeti hii ambayo tunaijadili, nijue kupitia utaratibu wa watu wa Wizara ya Ujenzi, wana mkakati gani sasa wa kwenda kuhakikisha barabara hii ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini tayari imeshakidhi vigezo ni lini itaaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili tuweze kuunganisha kati ya Wilaya za Nachingwea, Ruangwa, Liwale pamoja na Masasi ambao ni Mkoa wa Mtwara?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua namna gani ambavyo tunahangaika kupata adha kubwa ya usafiri katika maeneo haya yote. Kwa hiyo, watu wa Wizara ya Ujenzi, tunaomba sana watu wa mikoa hii na maeneo haya waweze kuangalia kilio chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la nishati. Mkoa wa Lindi na Mtwara kwa sasa tuko gizani. Hali ya upatikanaji wa umeme siyo ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri, amekuwa akitolea majibu mazuri pale tulipomwuliza, lakini naomba pamoja na kujenga kituo kile ambacho kiko pale maeneo ya Mnazi Mmoja, bado naomba nijue ni jitihada gani ambazo Wizara inakwenda kufanya, kwa sababu sasa hivi mashine zinazofanya kazi kwa umeme ambao unasambazwa mikoa yote miwili, hazizidi mashine nne. Je, tukishajenga kituo tunachojenga, bado inaweza kwenda kuwa ni suluhu ya kudumu ukiondoa jitihada nyingine za kuongeza mashine?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kupitia Wizara, naomba Mheshimiwa Muhongo Profesa wangu, tusaidie watu wa Mikoa hii ya Lindi na Mtwara. Kuna utaratibu gani kupitia Wizara za kuongeza hizi mashine ambazo zitakwenda kututoa gizani sasa hivi kama ambavyo hali imekuwa? Pia naomba na nitafurahi sana nikimwona anakuja katika maeneo haya ambayo siyo kwa muda mrefu wananchi wetu wametutupia lawama kwamba hatusemi na hatujawasilisha kero hii ambayo kwa kweli imekuwa ni changamoto kwa maendeleo ya Wilaya kubwa kama ya Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri tukishamaliza kikao hiki atutembelee katika haya maeneo ili kuona hali halisi ya namna tunavyopata athari.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo nataka nilizungumzie ni suala la ajira kwa vijana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu Waziri, rafiki yangu, Ndugu yangu, Mheshimiwa Anthony Mavunde, wamekuwa wanafanya kazi, ni wabunifu wa *project* mbalimbali ambazo zinaenda kuwainua vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie katika eneo moja, sisi Lindi na Mtwara tuna vyuo hivyo ambavyo tumevitja. Tuna *VETA* Lindi na Mtwara. Programu ambazo zimepitishwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masala. Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia leo kuwepo hapa katika hali ya uzima. Pili, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba hii muhimu iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchangia naomba kwa heshima kubwa tu nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu na nimwombe Mufti Bulembo kidogo ampe nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu ili atusikilize. Naomba tu Mufti Bulembo, tafadhali! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kwa dhati ya nafsi yangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kumteua Profesa Kabudi kuwa Waziri wa Sheria na Katiba. Hii inatoka ndani ya moyo wangu. Sambamba na hilo, nampongeza kwa kumwondoa Mheshimiwa Mwakyembe katika nafasi hiyo na kumpeleka katika Wizara ile ya kucheza; atacheza, sasa tunamwona anapiga makofi uwanja wa Taifa. Huu ni ujumbe tosha kwamba akufukuzaye hakwambii toka, waona nyendoze zimebadilika; waweza ukae, huwezi ondoka. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza sana Kamati ya Katiba na Sheria. Naipongeza kwa dhati sana kwa kuacha mapenzi ya vyama na kueleza lile lililo sahihi na la ukweli kwa mustakabali wa nchi yetu. Nawapongeza kwa dhati kwa kuona umuhimu wa kumwambia na kumweleza Msajili wa Vyama vya Siasa kama yeye wajibu wake ni kuvisajili na kuvilea vyama vya siasa na siyo kuvifarakanisha vyama vya siasa. Atekeleze wajibu wake na siyo kufanya mambo kwa mapenzi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba sana utusikilize. Mheshimiwa vyama hivi, mpaka chama kinaposimama kuna mambo mengi kinayopitia. Siyo jambo rahisi; vimeundwa vyama zaidi ya 20 ndani ya nchi hii, lakini hadi leo vyama vilivyosimama ni vyama visivyozidi vinne. Leo kwa sababu tu ya ulevi wa madaraka wa mtu mmoja, anatumia nafasi yake kufanya hujuma za waziwazi kwa ajili ya kukiteketeza Chama cha Wananchi - *CUF*, hilo jambo siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikitika sana kwamba amani ya nchi yetu ni miongoni mwa sekta muhimu ambayo vyama vya siasa wanabidi kuvisimamia inavyopasa. Leo hii tunaona yanayofanyika, tunaona jitihada zinazofanywa hata kumbeba yule kibaraka anayetumiwa na wanaomjua; baada ya kufanikiwa kuingia Buguruni, leo wanaandaa njama za kuvamia katika Makao Makuu ya Chama Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yanafanywa chini ya usimamizi wa watu wanaojulikana na kuna Waziri mmoja wa Zanzibar anaitwa Hamad Rashid ndiye *plan master* wa kuandaa mambo haya kwa kushirikiana na Makamu wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ally Iddi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema wazi haya ili dunia ijue na Watanzania waelewe. Haya yanayotokea kwetu siyo ya bure, ni mambo yamefanywa. Haiwezekani mtu anaacha chama mwenyewe zaidi ya mwaka mmoja anaenda kukaa huko, anarudi anajishauri. Hata kama ni mke, unakuta ameshaolewa na watoto ameshazaa na mume mwingine. Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yanayofanyika kwetu, leo hii nitashangaa nisikie Sofia Simba leo karudi kajitangaza tayari ni Mwenyekiti tena *UWT.* Hamtakubali! Kwa hiyo, kuchochea hayo katika vyama vyetu vya upinzani ni jambo la athari mbaya, jambo ambalo halitaipeleka Tanzania katika neema ambayo tunatarajia kuipata kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, neema ya Mwenyezi Mungu inakuja kwenye masikilizano. Msituchochee ndani ya Vyama vya Upinzani ili mkidhi haja zenu. Haiwezekani! Mlipoomba kura kwa Watanzania, mlisema Watanzania mtawaletea maendeleo, mtaleta elimu, maji; hamkusema kama mtafitinisha vyama vya siasa ili mambo hayo muweze kuyapata. Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukae tufikirie, tunapoandaa uwanja; tunapopanda nyasi tucheze vizuri, msitupandie michongoma ili tuumie miguu yetu. Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ujumbe huo umeupokea, naomba tufanye kila linalowezekana lililo ndani ya uwezo wenu, Serikali isaidie kutatua migogoro hii na isiwe wao ndio sababu ya kuimarisha migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, hivi karibuni katika vyombo mbalimbali vya habari ilitangazwa kwamba Watanzania tuko nafasi ya 153 kwa kukosa furaha duniani. Kwa kweli hili jambo lilinisikitisha, lakini halikunipa homa sana, lakini sasa baada ya kukosa furaha, inakuja Tanzania tunajengewa hofu ya lazima. Hili la furaha tungeliacha mbali, lakini hofu ambayo Tanzania tunajengewa sasa ndiyo jambo ambalo linanitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo haya yanayotokea ndani ya nchi sasa hivi katika tawala zote zilizopita hatukuzoea kuyaona. Wamepita Marais kadhaa na Mawaziri Wakuu kadhaa, hatukuona matukio yanayotokea ndani ya Tanzania yetu ya leo. Leo hivyo vikosi vinavyokwenda vinachukua watu na kuwapeleka ambako hakujulikani na bado sisi Watanzania, sisi Wawakilishi wa wananchi wa Tanzania tuliomo humu, kama hatukusemea hili na Serikali ikawajibika katika hili, itakuwa hatutendi haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la swala, anaweza akanyakuliwa mmoja, wawili na swala wakaendelea na safari, lakini siyo kundi la binadamu, kundi la Watanzania. Iwezekane yafanyike hayo na bado sisi tuendelee kufanya mambo mengine; hili jambo ni la hatari. Leo Mheshimiwa Bashe amesema, kama kuna orodha ya Wabunge kumi ambao wako *listed* haijulikani ni nini kitakachowapata wakati wowote. Mimi nimeingiwa na homa, sijui kama na mimi nimo! Eeh, Mungu wangu, tulinde waja wako na hizi hujuma ambazo hatujui nani anayeziandaa. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Amen! *(Makofi)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu cha hatari! Mheshimiwa Bashe anasema amepata taarifa kutoka kwa baadhi ya Mawaziri wa Serikali; hili siyo jambo dogo. Nadhani leo sisi Wabunge tusingekuwa na lingine la kujadili zaidi ya kufikiria hili. Kama kuna *list* ya Waheshimiwa Wabunge, hao raia wadogo wao wakoje?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunajadili bajeti ya maendeleo, maendeleo yapi yatakayopatikana wakati tayari tumejengewa hofu ya namna hiyo? Maendeleo yanaletwa pale watu wanapokuwa na amani, wanapojadili mambo kwa uwazi, wanaposema kwa uwazi; na mambo yale wakakaa wakapata muda wa kuyafikiri. Leo ikiwa Wabunge kumi hatujui, Mheshimiwa Selasini sijui yuko, sijui nani yupo, tunakaa sasa kila mmoja ana maswali ndani ya moyo; haijulikani ni nani yumo kwenye hiyo *list,* hebu Serikali tutoleeni hofu juu ya haya mambo. Tutoleeni hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Wafanyabiashara hawana furaha, Wamachinga hawana furaha, Wanasiasa hawana furaha, bodaboda hawana furaha; sasa jamani ikiwa kila mtu hana furaha na kila mtu anaiishi kwa hofu, ni Tanzania ipi tunaipeleka na ni wapi tunaipeleka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo anayeapa nambari moja Tanzania ni Mheshimiwa Rais, anaapishwa mbele ya Watanzania wote wanaona. Leo Mheshimiwa Rais baada ya kula kiapo kulinda na kuitetea Katiba, ni wa mwanzo anayetangaza vyama vya siasa ni marufuku kufanya mikutano ya kisiasa katika nchi hii. Hebu niambieni, ni nini kinachofanyika? Vyama vya siasa mnavipa ruzuku; sasa mnavipa ruzuku waende wakale na wake zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnawapa ruzuku wajitangaze watoe elimu ya siasa, elimu ya uraia, wajipanue wapate wanachama ili siasa za ushindani zitendeke ndani ya nchi. Leo mnawaambia tunawapa ruzuku, lakini ni marufuku kufanya mikutano ya vyama vya siasa. Maana yake nini? Sasa wataenda kuvizuia vyama vya siasa kupewa ruzuku, mnamchukua kibaraka Lipumba, mnamchotea mahela ya Serikali, anaenda kutumia anavyotaka yeye. Hiyo siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, haya mambo anayefikiria kwamba kufa kwa *CUF* ndiyo neema yenu Zanzibar, anajidanganya. Ziko roho zilizotangulia kwa

ajili ya *CUF* na ziko tayari roho nyingine kuzifuata kama mtafikiria kukifuta Chama cha Wananchi – *CUF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, kama nafasi itakuwepo, tutaendelea na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri Mkuu, Mawaziri pamoja na Manaibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimwambie kaka yangu Mheshimiwa Khatib, kwamba ugomvi wa mke na mume mara nyingi huwa wanamalizia chumbani. Mnapogombana huko chumbani, mkitoka nayo nje, hayo mambo yanakuwa yako hadharani, kila mmoja anayaingilia. Sasa msilichukulie kwamba Serikali ya CCM ndiyo inayowafitinisha ninyi. Ugomvi huu ninyi mmeutoa chumbani, mmeuleta hadharani. Sasa naomba sana, msiizungumzie Serikali kwamba ndiyo inayowahujumu ninyi. Hebu mkakae mmalize matatizo yenu, msiingize Serikali kwenye matatizo yenu.

**MBUNGE FULANI:** Wewe sio Waziri Mkuu.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Sasa nimekujibu basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze na bajeti ya Mfuko wa Bunge. Niungane na maoni ya Kamati ya Bajeti kwamba Mfuko wa Bunge unakabiliwa na changamoto nyingi za kutokupata fedha kwa wakati; na hata zinapopata hizo fedha, hazipati fedha yote. Naiomba Serikali iangalie

huu Mfuko wa Bunge, kwani huu mhimili wa Bunge ndiyo unaopitisha bajeti zote hizi za Serikali ambazo zinakwenda kufanya shughuli za maendeleo. Ni mhimili huu wa Bunge. Sasa Mhimili huu, ndio huu huu tena ambao haupewi fedha za kutosha kuhakikisha kwamba zinatimiza majukumu yake ya kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bajeti ili iweze kuhakikisha kwamba inatoa fedha za kuhakikisha zinaendesha shughuli za Bunge bila kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, safari hii Bunge limefika mahali Waheshimiwa Wabunge wamesafiri kwenda kwenye Kamati bila malipo kutokana na kutokuwa na fedha katika Mfuko wa Bunge. Sasa naiomba Serikali, pamoja na kwamba mihimili yote ina umuhimu wake, lakini mhimili huu una umuhimu zaidi kwa sababu ndiyo unaokaa kupitisha mambo yote haya ambayo hata wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu huwezi kwenda kukagua shughuli za maendeleo kama fedha hazijapitishwa na mhimili huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, katika mapendekezo yaliyotolewa kwenye kitabu cha bajeti ukurasa wa 14, tusipoangalia hili Bunge linaweza lisifike mwezi wa Sita. Wameomba mapendekezo pale wanasema, Kamati inaishauri Serikali kuridhia maombi ya bajeti ya shilingi bilioni 21 ili Bunge liweze kutekeleza majukumu yake mpaka kufikia mwezi Juni. Kwa hiyo, naiomba Serikali basi iweze kutekeleza hili angalau Bunge liweze kufanya shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la maji. Naishukuru Serikali, kule kwangu Korogwe nilikuwa na tatizo sugu la maji ambalo bado lipo halijakamilika, lakini angalau sasa limeanza kutekelezwa. Alikuja Naibu Waziri akatembelea akaona. Tuna Mto Pangani unapita katikati ya Mji wa Korogwe, alikuja akazungumza na akaenda kutekeleza, akatuletea fedha angalau shilingi milioni 500, tumeanza kuchukua maji kutoka kwenye Mto Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwaomba Wizara ya Maji kwamba ni vizuri zile fedha ambazo walituahidi, shilingi bilioni mbili kwamba watatupa katika bajeti hii, basi waweze kuzitoa fedha hizo itakapokuwa tumepitisha kwenye bajeti ili ziweze kufanya kazi ya kutengeneza miundombinu pamoja na matenki ili kusudi wananchi wa Korogwe waweze kuondokana na tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la afya. Pale Korogwe kuna Chuo cha Uuguzi na chuo kile kiko chini ya Wizara ya Afya. Chuo kile hakijawahi kutengewa fedha miaka 10, lakini kina jengo ambalo limejengwa limesimama, ni la muda mrefu, miaka 10 halijawahi kutengewa bajeti. Fedha ambayo imeteketea pale ni fedha ya walipa kodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, jengo lile badala ya kuwa limesimama vile, matokeo yake litaanza kupata *crack,* Serikali itaanza kutenga bajeti nyingine kwa ajili ya kukarabati jengo lile. Naiomba sana Serikali iangalie ni namna gani itakavyomalizia lile jengo la Chuo cha Uuguzi pale Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alitembelea eneo lile siku ambayo nimemwalika kwenye Jimbo langu kwa ajili ya kuja kuona shughuli za maendeleo, hususan ujenzi wa Kituo cha Afya ambacho ni cha ghorofa tatu. Namshukuru Mheshimiwa Waziri alikuja akaona tunafanya kazi nzuri na nategemea Mheshimiwa Waziri kwamba Mwenyezi Mungu akikujalia basi mnaweza mkatupiga jeki katika kile Kituo cha Afya, hasa ikizingatiwa kwamba Halmashauri ya Mji wa Korogwe haina Hospitali. Sasa kwa kuwa haina Hospitali, basi kile Kituo cha Afya ndiyo kitatufanya sisi tuwe na hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri alienda akaona kile chuo na akaliona lile jengo lilivyo, basi atusaidie zipatikane fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo lile ili ile fedha ya wananchi iliyokuwa imetumika wakati ule isiweze kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena suala la maji. Kuna miradi ile ya *World Bank,* ilikuwa itekelezwe pale Msambiazi, Lwengera Relini na Lwengera Darajani. Katika Bunge lililopita kulitengwa fedha, shilingi milioni 560 kwa ajili ya mradi wa Msambiazi na Lwengera Relini na Darajani, lakini fedha zile zinavyoletwa kule, maelekezo yanayofika kule, badala ya kujenga ule mradi wanasema zile fedha zilipe madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Maji na Umwagiliaji, mradi ule, wananchi wa Msambiazi wanachojua wao, wametengewa fedha. Sasa fedha inapokuja inaenda kulipa madeni ya miradi mingine iliyopita. Tunawaeleza nini wananchi wa Msambiazi na Lwengera Relini na Lwengera Darajani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itenge fedha za madeni, ilipe madeni na zile zinazotengwa kwa ajili ya miradi, zipelekwe kwenye miradi husika. Ni matumaini yangu kwamba, Waziri wa Maji amenisikia. Ni vizuri hizo fedha zikatoka zikaenda kujenga ule mradi wa Msambiazi kama ambavyo ilikuwa imepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la barabara. Naiomba Serikali, hizi Halmashauri ambazo zinaitwa Halmashauri za Miji, naishauri Serikali kama inawezekana; kwa kuwa tayari inaitwa miji, Halmashauri za Miji au Manispaa, tuanze kutenga bajeti angalau ya kilometa mbili mbili au moja kwa ajili ya lami ili iendane na hadhi hiyo inayozungumzwa kwamba Halmashauri za Miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pale Korogwe Mji, pale ni sebuleni; ukitoka Dar es Salaam, unakuja Korogwe, ndiyo hiyo inayokwenda moja kwa moja Kilimanjaro, Arusha, inaenda Nairobi, Kenya. Sasa pale sebuleni mkitusaidia kila mwaka tukawekewa angalau kilometa moja au mbili za lami, tutaishukuru sana Serikali angalau mji ule uweze kuwa na barabara za lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naisema hiyo, inaweza ikasaidia sana kuondokana na zile barabara za changarawe ambazo zinatengewa fedha kila mwaka. Tukijenga hizi za lami zinakuwa na mifereji ambayo imejengewa, lakini hizi za changarawe hazijengewi na mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali, kwenye miji hii ili tuifanye iwe miji mizuri, tujitahidi basi angalau kila mwaka tukiwatengea hiyo kilometa moja au mbili ili kusudi miji hiyo iweze kuwa mizuri kwa maana ya kuwa na lami katika mji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nishukuru tena, yangu machache yalikuwa ni hayo. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tutamalizia na Mheshimiwa Neema William Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia Hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kwanza nianze kwa kutoa pole kwa kifo cha mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Elly Macha, Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza mchango wangu kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Naipongeza kwa kuweza kujenga na kukarabati barabara urefu wa kilometa 430 ambayo ni 62% ya lengo alilojiwekea katika kujenga barabara urefu wa kilometa 692 kuanzia Julai, 2016 hadi Februari, 2017. Naipongeza sana Serikali yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa masikitiko makubwa, pamoja na pongezi hizo, Mkoa wangu wa Njombe hauna barabara ya lami hata moja. Naishukuru Serikali imeweza kutenga bajeti katika barabara zote za

Mkoa wa Njombe, lakini hakuna barabara hata moja iliyoanza kutengenezwa. Mfano, Barabara ya Itonyi – Ludewa – Manda; kuna Barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke; kuna Barabara ya Njombe – Makete; Barabara ya Njombe – Mdandu – Iyai; zote hizo zimetengewa bajeti, lakini bado hazijaanza kutengenezwa. Naiomba Serikali yangu sikivu, ianze sasa mchakato wa kuweza kutengeneza barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la afya. Siku zote nimekuwa nikisimama ndani ya Bunge hili na kuiomba Serikali; Wilaya ya Wanging'ombe ni wilaya mpya, hatuna hospitali. Wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe wanakwenda kutibiwa Hospitali ya Ilembula ambayo gharama zake ni kubwa. Wananchi wanashindwa kukidhi mahitaji ya afya kwa sababu gharama ni kubwa sana. Naiomba Serikali iangalie umuhimu wa kuweza kujenga Hopitali ya Wilaya ndani ya Wilaya ya Wanging'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna pesa ambazo zilielekezwa zipelekwe kwenye Zahanati na Vituo vya Afya vilivyomo ndani ya Wilaya ya Wanging'ombe, lakini mpaka sasa hivi pesa zile hazijapelekwa ili kuweza kujenga Zahanati na Vituo vya Afya. Matokeo yake sasa wananchi wamekusanya nguvu kubwa kuweza kujenga maboma kwa ajili ya Zahanati hizo na Vituo vya Afya, lakini pesa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi hazijapelekwa. Hii inawavunja nguvu wananchi kwa sababu wanatumia nguvu kubwa kujenga maboma kwa ajili ya hizo Zahanati na hivyo Vituo vya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikataja tu Vituo vya Afya na Zahanati chache ambazo ziko ndani ya Wilaya ya Wanging'ombe hazijapelekewa pesa ilhali pesa zilipangwa. Kuna Zahanati ya Itambo, Katenge, Igima, Mmerenge, Ivigo na kuna Vituo vya Afya, Mdandu, Igagala na Ilembula. Tunaomba sasa pesa zipelekwe ili Zahanati na Vituo vya Afya hivyo viweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna Hospitali ya Mkoa ya Kibena. Ile Hospitali ya Kibena ndiyo ambayo tunaitegemea sisi pale kwenye Mkoa wa Njombe, lakini hospitali ile majengo ni machakavu, vilevile wodi za wagonjwa ni chache. Kwa mfano, kuna wodi moja tu ya wanaume, wagonjwa wa Kifua Kikuu wanalala humo humo, wagonjwa wa ajali za bodaboda wanalala humo humo. Mtu anakwenda na ugonjwa mwingine, anakuja kupata ugonjwa mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweze kuongeza wodi za wagonjwa katika Hospitali ya Kibena, vilevile na kukarabati yale majengo kwani yamekuwa machakavu sana. Tunaomba Serikali iweze kutatua tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Jimbo la Lupembe, wananchi wamejitolea ekari 52 kwa ajili ya kuweza kujengewa hospitali katika Halmashauri ile ya Mji wa Njombe. Naiomba Serikali ifikirie sasa kwa kina na kuona umuhimu kwamba wananchi wa Jimbo la Lupembe nao wanahitaji hospitali ukizingatia kwamba Mkoa wetu wa Njombe ndiyo kwanza unaanza kukua na hivyo huduma nyingi za afya tunakuwa bado hatujapata vile inavyostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la maji. Nimekuwa nikizungumzia suala la maji mara nyingi sana ndani ya Bunge hili na kuiomba Serikali iweze kutatua tatizo la maji katika Tarafa ya Wanging'ombe. Tatizo la maji Tarafa ya Wanging'ombe katika Jimbo la Wanging'ombe limekuwa ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda mwaka 2015 kuomba kura kwa ajili ya kumwombea Mbunge ambaye ni Waziri wa Maji, Mheshimiwa Lwenge, kwa kweli akinamama na akinababa tatizo lao kubwa sana kule ambalo walikuwa wakilitaja mara kwa mara ni tatizo la maji. Ukienda Kata ya Kijombe, Saja, Ilembula, Wanging'ombe yenyewe tatizo la maji ni kubwa sana. Tunaomba tatizo hilo liweze kutatuliwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mji wa Makambako wanapata maji kwa msimu. Kipindi cha kiangazi maji hakuna kabisa. Maji yanapatikana kipindi cha masika tu. Tunaomba Serikali iweze kuangalia tatizo hilo la maji katika Mji wa Makambako ili akina mama wa Makambako waweze kujikwamua katika tatizo hilo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Njombe Mjini hali ni hiyo hiyo, tatizo la maji bado lipo na inapunguza ufanisi mkubwa sana kwa akinamama kufanya kazi kwa sababu, muda mwingi wanakuwa wanatumia kwenda kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Lupembe katika vijiji 45, vijiji 31 vyote havina huduma ya maji. Hali ni mbaya. Tunaomba Serikali iweze kutatua tatizo hilo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye elimu. Shule zetu zilizopo ndani ya Mkoa wa Njombe, kwa maana ya Shule za Msingi na za Sekondari majengo yetu ni machakavu, lakini vilevile tuna uhaba wa madarasa na uhaba wa Walimu wa Sayansi katika Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukakuta Shule ya Sekondari haina Mwalimu hata mmoja wa sayansi na shule nyingine zina Mwalimu mmoja au wawili. Kwa kweli, naiomba Serikali sasa itambue umuhimu wa kuongeza Walimu wa sayansi katika shule zetu za sekondari ndani ya Mkoa wa Njombe na kuweza kukarabati madarasa hayo pamoja na kujenga madarasa mapya kwa ajili ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kilimo. Kule kwetu Njombe tuna zao kubwa la chai, lakini hivi sasa bei ya chai imeshuka sana. Kilo moja wanauza 250/= wakati gharama za uzalishaji zinazidi kilo moja ya chai. Gharama za uzalishaji katika kilo moja ya chai ni shilingi 450/=, unaona kuna tofauti hapo ya karibu sh. 200/=. Tunaomba Serikali iangalie soko la chai katika kilimo chetu cha chai ndani ya

Mkoa wetu wa Njombe ili wale wakulima ambao wanalima chai waweze kupata faida na wasiwe wanazalisha kwa hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pembejeo. Mbegu zinachelewa kufika kwa wakati, lakini mbolea ya kukuzia inachelewa kufika. Hazifiki kwa wakati, lakini cha kusikitisha zaidi muda wa kupanda umeshapita, muda wa kuweka ile mbolea ya kukuzia umeshapita; wananchi wanalazimishwa wanunue zile mbolea, wanunue na zile mbegu, wakati huo muda unakuwa umeshakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, hiyo siyo sawa na siyo jambo jema kwa wananchi wetu kuwafanyia hivyo. Tunaomba mbegu na mbolea za kupandia zifike kwa wakati ili zisije zikachelewa halafu tena bado mnawalazimisha wanunue hizo mbolea na hizo mbegu, inakuwa ni hasara kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nimalizie tu katika suala la umeme. Lupembe bado kuna changamoto kubwa sana ya umeme. Katika vijiji 45, vijiji 30 vizima havina umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya.

Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Nitayasoma majina ya wachangiaji wetu wa mchana leo, halafu nitatoa maelezo kidogo ya mambo yaliyopo hapa Mezani.

Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mheshimiwa John Peter

Kadutu, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mheshimiwa Lucy Magereli, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Kasuku Bilago.

Wachangiaji hawa nimewasoma kwa pamoja, kwa hiyo, tutaanza na orodha yoyote kati ya hivi vyama vilivyoleta orodha hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, mambo manne kwa ajili ya kukumbushana, moja ni kwamba eneo hili la Siwa wanaoruhusiwa kupita ni Wahudumu na siyo Wabunge. Yamekuwepo mazingira mengi ambapo Waheshimiwa Wabunge wanakatiza hapa katikati.

Kanuni yetu ya 66 inazungumzia staha ya namna yetu ya kuenenda humu Bungeni; unaweza ukapita viti kwa nyuma ukakatiza hapo nyuma, lakini usipite hapa mbele maana utarudishwa. Sababu, Kanuni yetu ya 66 inasema usipite katikati ya mzungumzaji na Spika. Sasa ukipita hapa ni vigumu sana wewe kutokuwa umekatiza mbele, yaani kati ya mtu anayezungumza na Kiti.

Kwa hiyo, niwakumbushe tuwe tunajitahidi kupita nyuma ya viti kuliko kukatiza hapo mbele, japokuwa inaonekana ni njia ya mkato. Hilo ni la kwanza.

La pili, kuhusu kutoa pole na pongezi Kanuni ya 154, kwa sababu Mheshimiwa Spika, alishatoa hiyo pole kwa niaba ya Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa pole kwa upande wa Serikali. Kwa hiyo, tuzingatie ile Kanuni, tusiendelee na hizo pole kwa sababu Mbunge anayekuwa hajatoa pole na amechangia, anaonekana kana kwamba hajali, kumbe anafuata Kanuni. Kanuni yetu ya 154 inataka tuzingatie hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lingine Mheshimiwa Spika alilizungumza sana wiki iliyopita. Tujitahidi sana, tusiwashe *microphone* kabla hujaruhusiwa kuzungumza kwa sababu, kimsingi kila mtu anayewasha *microphone* anaonekana. Sasa tukianza kutaja majina hapa mbele kwamba fulani; na ikaonekana unatajwa kila siku, nadhani kwa wananchi na pia wakati mwingine watu wanaokuja kujifunza hapa, linakuwa siyo jambo jema.

La mwisho, ni kuhusu kutembelea kile Kiti cha ziada cha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na mambo mengine, anayo ofisi kwa ajili ya mambo ya kiofisi. Hapa Bungeni siyo kwamba Wabunge mnazuiwa kwenda kumwona, lakini mkamwone kwa mambo ya dharura, mambo ya haraka. Kwa sababu anapokuja Bungeni hata yeye anakuwa amekuja kushiriki kama Wabunge wengine.

Sasa kila wakati akiwa na mtu anayezungumza naye, yeye anasikiliza saa ngapi? Ndiyo maana tunajikuta mazingira ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna mambo anaweza akaulizwa hapa, kumbe lilikuwepo hapa hapa Bungeni, lakini sisi tulikuwa kila wakati tunamzungumzisha. Kwa hiyo, haelewi sasa kwamba hilo jambo lilitokea wakati gani wakati alikuwepo. *(Makofi)*

Sasa naomba tujitahidi, siyo kwamba mnazuiliwa kwenda, lakini twende kwa mambo ambayo siyo yale ya kila siku ambayo anaweza kuombwa akaonwa kwa kufuata utaratibu mzuri. Tumpe nafasi na yeye ya kushiriki kama Wabunge wengine.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 1l.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo ajiandae.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imesheheni mambo mazuri. Pia nipongeze Kamati zote tatu kwa maana ya Kamati ya UKIMWI, Kamati ya Katiba na Kamati ya Sheria na Bajeti kwa kuwasilisha vizuri maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na ninyi, ambaye ametujalia afya na nguvu kuweza kuhudhuria na kusema chochote katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja katika kuchangia na nianze na afya. Kama unavyofahamu Chama chetu cha Mapinduzi ambacho ndiyo chenye Serikali llani inasema kila kata itajengwa kituo cha afya na kila kijiji itajengwa zahanati. Kwa kuzingatia hilo sasa kwenye Jimbo langu la Lushoto nimebahatika kujenga zahanati kumi na tatu na vituo vya afya viwili. Zahanati karibia tatu zimeisha zinahitaji madaktari na nyingine kama tano zimepigwa bati lakini bado usafi na zilizobaki bado zinahitaji kumaliziwa. Kwa hiyo, sasa niombe Serikali yako Tukufu kwamba ipeleke pesa katika halmashauri ili iweze kumalizia zahanati zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Lushoto ina Majimbo matatu na Hospitali ya Wilaya moja. Takribani Wilaya ya Lushoto ina wakazi zaidi ya laki sita lakini hospitali

ile imehemewa yaani inajaza kiasi kwamba kwa kweli sijui nieleze nini. Niiombe Serikali na niishauri katika bajeti hii inayokuja basi watenge bajeti ya kutosha ili Hospitali ile ya Wilaya iweze kupanuliwa hususan chumba cha akina mama wajawazito na chumba cha mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekee kwenye kilimo. Niiombe Serikali yangu tukufu ijielekeze katika sekta ya kilimo kwani kama tunavyofahamu kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu hili na kimebeba takribani asilimia sabini. Niiombe Serikali yangu itenge mafungu ya kutosha katika kilimo na pia iwawezeshe wakulima wetu wadogo wadogo hawa hususan wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Lushoto ni ya milima na mabonde, ni ya wakulima wa bustani mfano mbogamboga na matunda. Wakulima wale wanachangia asilimia kubwa katika Halmashauri zetu lakini cha kushangaza hawapati pembejeo. Niiombe Serikali sasa kwa jicho la huruma iwaangalie wakulima wale wa mbogamboga hususan wale waishio Lushoto waweze kupata pambejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo naiomba Serikali iweze kujenga mabwawa katika Wilaya ya Lushoto kwani mvua nyingi sana zinanyesha kule lakini zinaharibikia baharini. Kwa hiyo, niiombe Serikali sasa ijenge mabwawa ili wananchi wetu waweze kulima kilimo cha umwagiliaji. Pia hii itakuwa ni fursa kwa vijana wetu na ili wasikimbilie mjini basi tuwajengee miundombinu ili waweze kujiajiri wenyewe na kulima kilimo cha umwagiliaji. Naamini hii italeta tija kwa vijana wetu na wala hawatakimbilia mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye miundombinu. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbarawa kwa kazi kubwa anayoifanya. Ila nimuombe sasa kuna barabara hiyo tangu ninasoma darasa la kwanza kila siku naambiwa itapanda hadhi, lakini haipandi. Barabara hiyo imeanzia Mlalo - Ngwelo - Mlola - Makanya ikaenda mpaka kwa

Stephen Ngonyani (Maji Marefu) Korogwe Vijijini mpaka kwa mzee wangu Mheshimiwa Kitandula. Nimuombe sasa Mheshimiwa Waziri Mbarawa hebu afumbe macho tu barabara ile ipandishwe hadhi kwani ni muda mrefu sana na kila nikisimama kwenye Bunge lako Tukufu naisemea barabara ile. Kwa heshimiwa kubwa na taadhima niliyokuwa nayo kwake nimuombe basi barabara safari hii ipandishwe hadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara zetu za mchepuko. Kama unavyofahamu Lushoto ni ya milima na mabonde kwa hiyo Lushoto bila barabara kwa kweli hatuwezi kusafiri. Lushoto kuna barabara kuu moja tu ikipata *breakdown* basi sisi Lushoto tumekwisha hata mahitaji tunashindwa kupata. Kwa hiyo, niiombe Serikali yako Tukufu sasa Mheshimiwa Mbarawa kwamba kuna barabara ambayo inatoka Dochi - Ngulwi mpaka Mombo ni ya mchepuko na itakuwa mbadala kwa ajili ya *breakdown* itakayotokea maeneo ya Soni - Mombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara aliahidi Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne kilometa nne mpaka sasa sijapata maelezo yake. Niiombe sasa Serikali yako Tukufu hebu tuweze kupatiwa kilometa nne zile angalau tuweze kutengeneza Mji wetu wa Lushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sasa Serikali hususan Waziri wa TAMISEMI kwamba zile barabara ambazo zipo Halmashauri zirudi kwa Wakala wa Barabara yaani *TANROADS. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna hii Idara ya Ardhi kule Halmashauri nayo irudi kwa Mkuu wa Wilaya kwa sababu ndiye anayesuluhisha migogoro ya ardhi zaidi kuliko Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu; Wilaya ya Lushoto kama nilivyosema ina Majimbo matatu lakini haina chuo cha *VETA*. Kwa hiyo, nimuombe mama yangu mpendwa Waziri wa Elimu atujengee hata chuo kimoja cha *VETA* kwani

maeneo yapo tayari, kuna karakana, gereji na majengo mengine. Kwa hiyo, nimuombe Waziri wangu huyu aweze kuliona hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanikiwa kujenga maboma zaidi ya ishirini, lakini bado hayajaezekwa kwa maana ya kupigwa bati. Sasa basi niiombe Serikali yako na Waziri wa TAMISEMI apeleke pesa za kutosha kule kwenye Halmashauri ili maboma yale ambayo tumeyajenga kwa nguvu za wananchi tuwape moyo wasije kukata tamaa juu ya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme; kwanza nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Muhongo kwa kazi kubwa anayoifanya na Naibu wake, ila nimuombe kitu kimoja maana tunapata maswali magumu sana kule vijijini, unakaa tu hapa Bungeni unapigiwa simu haya vijiji vingapi vimepata umeme unawaambia jamani bado hata orodha hatujaipata. Kwa hiyo, nimuombe Waziri wangu sasa niweze kupata ile orodha ya vijiji ili niweze kuwajibu watu wangu wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa vijana; kama unavyofahamu sasa hivi vijana ni wengi mno hususan vijana wa bodaboda na wauza mitumba.

Kwa hiyo, niiombe Serikali sasa wajengewe uwezo ili waweze kujiajiri wenyewe na kama unavyofahamu sasa hivi vijana wengi wemejiunga na vikundi na wana *SACCOS* zao. Pia hizi *SACCOS* naomba ziundwe kisheria ili zitambulike na kukopesha hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Moses Mlata atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Philip Mbogo na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad ajiandae.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Na mimi niungane na wengine kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa namna ambavyo aliamua kwa vitendo kuleta Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma. Kwa kweli ni uamuzi wa kishujaa na busara, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu yeye ndiye aliyeongoza jahazi la Mawaziri kwa maana ya Wizara zote kuja hapa. Nimpongeze sana Mheshimiwa Jenista na Ofisi yake maana yeye ndiye aliyetangulia kufungua mlango kumpokea Waziri Mkuu. Kwa kweli pongezi sana Mheshimiwa Jenista kwa kuratibu zoezi hili na kuhakikisha Wizara zote zinakuja hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza haya kwa sababu Dodoma ni pacha na Mkoa wa Singida. Kwa hiyo, pacha wetu akipata neema na Singida tunapata neema kwa maana ya kwamba Wizara zote na watu wengi watakaoishi hapa Dodoma watatumia bidhaa kutoka Singida. Kwa hiyo, sisi wana Singida tumejiandaa kuleta mazao mbalimbali kwa maana ya kuku, karanga, viazi, vitunguu na mazao mengine mengi pamoja na mafuta mazuri sana ya alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kidogo kwamba mara nyingi Makao Makuu ya Serikali jengeni Mji uwe Makao Makuu ya Serikali. Naomba ile miradi mikubwa ya uwekezaji leteni kwenye Mikoa yenu iliyo jirani ukianzia Singida ili Mji huu ujengeke kama Mji wa Kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niwapongeze Mawaziri wote. Mawaziri safari hii mmekuwa wanamgambo kweli kweli. Mmeweza kuchapa kazi hamjakaa maofisini. Sisi

wenzenu tunataka tuwaambie, mnapofika mikoani hata wale watendaji wenu waliopo kule hakika wanapata hamasa ya kufanya kazi. Pia wananchi wanapoona Mawaziri mnatembelea miradi na kuangalia changamoto mbalimbali hiyo tunajijengea imani kwa wananchi kwamba Serikali yao inawajali. Pongezi sana Mawaziri wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru hivi karibuni Waziri wa Nishati na Madini alikuja Singida kufungua Mradi wa *REA III*. Kwa kweli napongeza sana na tunawaomba wale wakandarasi wakatimize sawasawa na mkataba unavyosema ili wananchi waendelee kunufaika na mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoileta hapa nataka kusema iko sahihi kabisa, lakini nataka kushauri katika eneo moja tu. Eneo hilo ni kutokana na diplomasia ya kiuchumi inayofanywa na Mheshimiwa Rais wetu. Marais waliopita wamefanya lakini na yeye amefanya diplomasia kubwa sana maana tumeshuhudia viongozi wakuu mbalimbali wa nchi wakitembelea nchi yetu, kwa kweli ninampongeza lakini tumeshuhudia mikataba kwa maana ya makubaliano *(MoU)* zikisainiwa pale Ikulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuuliza ni nani anayefuatilia makubaliano haya kwa sababu tunahitaji kupata mrejesho kwamba ilisainiwa 20, 60 au mingapi na imetekelezeka mingapi? Pamoja na kwamba tumeona kuna mingine imeshaanza, lakini kwa ushauri wangu kwa sababu nina mfano halisi, tangu Rais wetu ameingia naomba nisitaje Marais au wakuu wa nchi ambao wameshakuja hapa kwetu na kusaini mikataba mbalimbali ni tisa, ni mingi.

Kwa hiyo, nashauri kuwe na chombo maalum cha kitaifa ambacho kitaundwa kiwe chini ya Kamishna ambaye ni mbobezi katika masuala ya uchumi na diplomasia. Chombo hiki kiwe na wanasheria, wanadiplomasia, wachumi na kadhalika ili waweze kukaa kuainisha *MoU* hizi na kuhakikisha zinapelekea kwenda kwenye mkataba

unaotekelezeka. Kamishna huyu awe anaweza ku-*communicate* na taasisi zote zinazohusika kutokana na *MoU* hizo au makubaliano hayo ili kuleta matokeo chanya ambayo yamekusudiwa na viongozi wetu husasan Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hayo kwa sababu kabla ya awamu hii alikuja Rais kutoka China na viongozi wengi pamoja na wafanyabiashara na Rais wetu akaenda. Alipofika hapa wakaingia *MoUs* nyingi lakini utekelezaji wake mmoja tulifika pale Beijing China wakatuambia kwamba kulikuwa na makubaliano ya ndege ya China kuja Tanzania kuleta watalii, lakini hakuna aliyeweza kujibu suala lile hatimaye ndege ile ilihamia Kenya. Hii inatia uchungu na ndiyo maana nimeshauri kuwe na chombo maalum kitakachosimamia makubaliano hayo kupelekea kwenye utekelezaji unaoleta matunda chanya katika taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isije tukaishia tu watu kupiga picha na kumwaga wino, ni lazima tuwe na mkakati huo. Pia kuwe na *library* ya kutunza mikataba au makubaliano hayo. Ni nani anaweza akatuambia, je, kuna maktaba inayotunza, iko mingapi? Napenda nijue kwa miaka mitatu au minne awamu iliyopita na hii, je, ni mikataba au makubaliano gani ambayo yamefikia kwenye utekelezaji? Naomba sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kumalizia, tulipotoka ni mbali Taifa hili na Mungu wetu amekuwa akitupenda Watanzania, amependa sana Taifa letu. Naomba kusema anayefikiri na kudhani amesimama na aangalie asianguke. Kwa sababu ufalme ukifitinishwa hakuna atakayebaki salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba anayedhani amesimama na aangalie asianguke. Tusije tukawa kama wale wajenga mnara wa Babeli kila mtu akazungumza lugha yake kwa sababu walitaka kumpandia Mungu kichwani ndio maana Mungu akawasambaratisha. Naogopa Taifa hili tusije

tukasambaratishwa kwa kunena na kutaka kupanda kwenye maeneo ambayo hakika sio nafasi yako. Anayedhani amesimama na aangalie asianguke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namtia moyo Rais wangu, endelea kufanya kazi, haukuja kimakosa maana kila utawala ni maridhio ya Mwenyezi Mungu. Fanya kazi tupo pamoja, kuwa mnyenyekevu mbele za Mungu na Mungu atakuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fulani niliwahi kusema kuna watu humu ndani wako kama hali ya hewa ya Dar es Salaam. Dar es Salaam jua litawaka leo, kesho ni mafuriko, leo ni mafuriko kesho ni kipupwe. Kwa hiyo, kuna watu ni vigeugeu, leo watasifia jambo, kesho watalibeza, leo watalalamikia jambo, kesho watalibeza. Rais wetu kama nyumba inavuja tia gundi, tia nta, endelea kuchapa kazi kwa maana mvua haiwezi kuacha kunyesha. Naomba nimtie moyo Rais wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na sisi Wanasingida tumejiandaa sawasawa, michango mingine nitachangia kwenye Wizara zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ni Mheshimiwa Richard Philip Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad na Mheshimiwa Lucy Magereli ajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mungu kwa kuweza kutufikisha siku hii ya leo. Binafsi naomba nimpongeze Waziri Mkuu na timu yake na Mawaziri wote kwa jinsi ambavyo wameshirikiana naye katika kuandaa bajeti hii. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mavunde kwa kushiriki vyema kwenye bajeti hii pamoja na uwashaji wa mwenge Kitaifa

kwenye Mkoa wetu wa Katavi. Wametupa ushirikiano wa hali ya juu, tumekwenda nao na wamefanya kazi kubwa kwa kweli tunawapa pongezi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kidogo nigusie kwenye hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mbowe. Kuna mahali alizungumzia kwamba bajeti ya Serikali ni ya kisiasa, kwamba ina vyanzo hewa vya mapato. Naomba alichukue hili, yeye hotuba yake ndiyo ya kisiasa kwa sababu kwenye hotuba yake ile amesema kwamba Serikali kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 iliweka chanzo cha kodi kwenye kiinua mgongo cha Wabunge wakati kodi hiyo itakwenda kutozwa mwaka 2020. Naomba nimwambie kwamba yeye ndiyo amefanya kisiasa, sio sahihi. Nakumbuka mwaka jana nilileta *schedule of amendment* kwenye eneo hili na Kanuni ilifuatwa, kulikuwa hakuna *financial implication* kwenye masuala ya kodi kwenye kiinua mgongo cha Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwenye bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu ameweza kuzungumzia kwa kina kuhusu uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Naunga mkono, wameweza kutoa shilingi bilioni 1.5 kwa vijana kutoka kwenye ofisi yake na takribani shilingi bilioni 4.6 kwa upande wa mapato ya ndani kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo ninaloliona ni Halmashauri nyingi kutotimiza ile kanuni inayoelekeza kutoa asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa akina mama.

Kwa hiyo, niombe sasa ili tuweze kufikia kuwawezesha wananchi wetu kufanya shughuli za kiuchumi, Serikali iweke msisitizo kwenye kuhimiza Wakurugenzi na kuwasimamia ili waweze kuhakikisha kwamba fedha hizi zinakwenda, maana Halmashauri nyingi maombi yapo lakini watu hawajapewa hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yale mafunzo ambayo yaliweza kutolewa chini ya Ofisi hii ya Waziri Mkuu kupitia VETA, Don Bosco, tunaomba yawe endelevu na hapa ndipo

itakapokwenda kutusaidia katika kujenga ajira maana kuna watu wameweza kupata mafunzo haya na cheti. Naomba Serikali, Halmashauri zetu tuna mwongozo tunapeleka magari yetu kwa mfano *TEMESA,* lakini utaangalia gharama ile ambayo Halmashauri zinalipa kule *TEMESA* kwa baadhi ya huduma ni ghali sana.

Kwa hiyo, tuombe sasa Serikali kwa mafunzo haya ambayo yanaendeshwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tuweke ajira za mikataba kwa watu ambao wamepata mafunzo ya ufundi ili tuwe na mafundi wetu katika Halmashauri tupunguze gharama ambazo zinakuwa hazina tija kwa upande wetu, tukiwezesha vijana tayari tumejenga suala la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni migogoro. Ofisi ya Waziri Mkuu hili liko chini yenu kuna *CMA* na Mabaraza ya Wafanyakazi lakini kuna matatizo ya watumishi wanakuwa wanahamishwa bila tija tu kwa malalamiko ya baadhi ya viongozi. Utakuta kiongozi eneo moja tu analalamika kwa makosa ambayo mtu anaweza akasahihishwa basi anahamishwa, kwa hiyo, tunaongeza gharama kwa Halmashauri na ndiyo tunazidi kuweka madeni upande wetu wa Serikali kwa uhamisho ambao hauna tija. Tunakumbuka wakati Mheshimiwa Rais alivyoapishwa alisema kwamba hatamhamisha mtu, mtu atakuwa anachukuliwa hatua za kinidhamu kwenye eneo ambalo yuko. Sasa tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu itoe mwongozo kwa Wakurugenzi wasifanye uhamisho ambao hauna maslahi ya kihalmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la Bunge letu hili. Wabunge wamechangia, tumeona kwamba kuna ongezeko la bajeti karibu shilingi bilioni 21. Napenda kujua, kwa mwelekeo mpaka mwisho kuna upungufu wa shilingi bilioni 21 na gharama nyingine za msingi ambazo Serikali iliweza kuziomba na kuziahirisha, je, hii bajeti ya sasa hivi ya shilingi bilioni 121 kweli inakidhi? Kwa hiyo, tuangalie zile gharama nyingine, kwa mfano, ile wiki ya kwanza kutokana na Kanuni tarehe 11 Machi hatukuweza kufika, je, ile gharama

imekuwa-*incorporated* kwenye hiyo shilingi bilioni 21? Kwa hiyo, tunaomba kwa misingi ya Katiba kama Bunge tunaofanya hiyo kazi bajeti hii iweze kuangaliwa kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kuhusu walemavu. Ofisi ya Waziri Mkuu ina wajibu huo na sheria ipo ya mwaka 2010, Sheria Na. 9 na kuna Mabaraza ya Walemavu katika ngazi ya Kitaifa, Mkoa mpaka kwenye Kata. Je, nani mwenye wajibu wa kuhakikisha kwamba Mabaraza ya Walemavu kwenye Kata na Wilaya yanafanya kazi na kanuni zake zipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofanya kazi *TASAF* basi na walemavu wawe na mfuko wao tuweze kuwawezesha iwe ni sehemu ya ruzuku na isiwe mkopo ambao una riba na wapewe mafunzo kulingana na ulemavu mtu alionao ili aweze kufanya kazi yoyote ile. Siku moja redioni nilisikia mtu mwenye ulemavu wa macho anampima mtu na anashona nguo. Kwa hiyo, tunahitaji sana tuwaendeleze ili waweze kuondoka kutoka kwenye utegemezi. Kwa hiyo, tuombe sasa Ofisi ya Waziri Mkuu huu mfuko kama haupo basi muuanzishe na angalau hata kabla Bunge hili halijamalizika tuweze kuupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Mifuko ya Jamii. Mwaka 2012 tuliweka sheria ya kuzuia lile fao la kujitoa lakini sina uhakika, ila ni kwamba *NSSF* japokuwa hii sheria ilikuwa inazuia waliweza kuendelea kutoa fao la kujitoa. Nchi yetu tunahitaji hii mifuko ya hifadhi ya jamii iweze kusaidia katika kuleta viwanda na tumeona maelekezo kwenye randama humu kuna karibu mikoa 14 ambayo mifuko ya jamii inaelekezwa kwenye kuwekeza. Maoni yangu kwa sababu kuna mwingine anakuwa ameachishwa kazi na hana uhakika wa kupata kazi basi Serikali iangalie angalau katika lile fao la kujitoa ama akate asilimia 25 ya akiba mtu aliyonayo au theluthi moja yule mtu aweze kupewa ili katika kipindi cha mpito wakati anatafuta kazi ziweze kumsaidia katika kuendeleza maisha aliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa kisekta tunajua tuna Wizara zinahusika na haya mambo ya kisekta, upande wa viwanda, lakini nizungumzie kuhusu barabara ambayo kwenye bajeti hii ipo, ya Mpanda - Tabora kwa kiwango cha lami. *Tender* zilitangazwa lakini mpaka sasa hatujafahamu ni watu gani wamekwishapewa hizo *tender* kutokana na marekebisho ya mkandarasi mshauri. Kwa hiyo, tuombe watu wa *TANROADS* watuharakishie. Sisi tukifanya ziara kule wananchi wanatuuliza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Mpanda mpaka Tabora lini unaanza? Sasa kama fedha ipo tulishapata toka *ADB* kwa nini watendaji wetu wa *TANROADS* Makao Makuu wanachelewesha kurekebisha hiyo *BOQ* ili kazi ziweze kuwa *awarded?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa kilimo tumeona taarifa kwenye mpango, kilimo kimekuwa kimekua kwa asilimia 2.9 tofauti na malengo ya asilimia sita. Sasa tatizo ni nini na hapa ndiyo ajira kubwa ya wananchi wetu ilipo. Kwa mfano, Jimbo langu la Nsimbo asilimia 90 ya wananchi wangu ni wakulima wanalenga zaidi kwenye shughuli hii ya upande wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa maliasili, tuna Mbuga yetu ya Katavi, tunahitaji miundombinu iboreshwe na huduma ya *Bombardier* ya *ATCL* ianze ili watalii waje. Tuna viboko, Ziwa la Katavi, twiga mweupe ambaye atakuwa ndiyo kivutio zaidi kwa watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Juma Kombo Hamad. Kabla hajanyanyuka, naamini mmepata karatasi zinazoonyesha marekebisho madogo katika Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**NAIBU SPIKA:** Kama kuna Mbunge hana, zipo pale mlangoni, wahudumu naomba msaidie kuwagawia Waheshimiwa Wabunge ili warekebishe taarifa zao, Mheshimiwa Mbowe ameleta marekebisho ya hotuba yake.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Magereli, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha ajiandae.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie mawili, matatu kuhusiana na hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu kwa kuanza kuchangia katika sehemu ambayo mara nyingi tumekuwa tukiisemea au imekuwa ikizungumzwa humu kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wazanzibari mara nyingi wamekuwa wakijiuliza hatma ya Mashekhe hususan kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, lakini leo nimeamua kulizungumza hili kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu tukiwa na matumaini kwamba kilio hiki sasa kinaweza kikasikika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni juzi tu kupitia Mahakama Kuu ya Zanzibar, Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar alinukuliwa kupitia vyombo vya habari akisema kwamba Mashekhe wale wameletwa huku kwa makosa na sasa wanatakiwa warejeshwe Zanzibar kwa namna yoyote itakavyokuwa. Kwa bahati mbaya sana hatukuona hata dalili ya namna ambavyo kuna ushughulikiwaji wa suala lile kuona kwamba Mashekhe wale sasa watarejeshwa Zanzibar na kama ni kuhukumiwa basi watahukumiwa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka minne sasa Mashekhe wale wako ndani, haijulikani tatizo ni nini isipokuwa kinachoonekana pale ni mihemko au hisia tu za kisiasa ambazo zimewafanya Mashekhe wale wanaendelea kusota ndani. Miaka minne imetosha, kama masuala ya upelelezi hayajakamilika kwa nini basi wasipewe dhamana

wakaendelea kufuatiliwa wakiwa pamoja na familia zao na huku kesi ile inaendelea? Miaka minne ni mingi sana, naamini kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ni kubwa, Waziri Mkuu ni mtu mkubwa katika Serikali hii, ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali anaweza akasikia vilio hivi vya Wazanzibari kuona kwamba Mashekhe wale ni sehemu ya Watanzania wanasikilizwa na wanaachiwa na wanaendelea kuwa huru pamoja na familia zao, hilo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, katika mambo ambayo tutayapitisha kupitia Bajeti ya Waziri Mkuu hii ambayo tunaijadili sasa ni pamoja na kujadili Fungu Namba 27 ambalo linagusa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Ni jambo ambalo halikujificha, liko wazi kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa sasa ameamua kwa makusudi kabisa kuingilia na kupandikiza migogoro ndani ya vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu ofisi hii majukumu yake yamezungumzwa ndani ya sheria inayoongoza vyama vya siasa ya mwaka 1992. Moja, kusimamia kumbukumbu za vyama vya siasa; pili, kusajili vyama vya siasa ambavyo vimekidhi matakwa ya sheria hiyo; tatu, ni kufuta chama cha siasa ambacho kimekwenda kinyume na taratibu hizo ambazo zimezungumzwa ndani ya sheria pamoja na majukumu mengine lakini haya matatu ndiyo majukumu makuu ya Ofisi hii ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Kwa bahati mbaya sana Msajili wa Vyama vya Siasa leo amejipa majukumu mengine, sijui kayatoa wapi, madaraka haya sijui ameyatoa wapi ya kuona kwamba sasa ana mamlaka ya kuchagua chama cha siasa kiongozwe na nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wote wanafahamu, Watanzania wote wana akili timamu na wanafahamu kwamba Profesa Lipumba alijiuzulu Agosti, 2015 kwa kuandika barua ya kujiuzulu kabisa. Baada ya miezi kumi Profesa Lipumba anasema anarudi katika nafasi yake ya Uenyekiti. Katika Katiba hii ya Chama cha CUF hakuna sehemu yoyote ambayo inatoa mamlaka kwamba mtu

anapojiuzulu baada ya muda anaandika barua kwamba narudi kwenye nafasi yangu, hakuna. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilipokea barua na *minutes* zote za vikao kwamba sasa wanaokaimu nafasi ya Mwenyekiti ni hawa. Chama cha CUF kupitia Baraza Kuu la Uongozi kikaunda Kamati ya Uongozi ya Chama na kupeleka kila kilichotakiwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kutambulisha kwamba sasa wanaoongoza majukumu ya Mwenyekiti ni hawa kwa muda wa miezi kumi. Baada ya miezi kumi Profesa Lipumba anaandika barua ya kurudi kwenye nafasi yake ya Uenyekiti, *very shameful. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jaji akaamua kwa makusudi kabisa kwa sababu eti anataka kuivuruga CUF kutambua kurudi kwa Profesa Lipumba bila kufuata sheria, kanuni, Katiba ya nchi, kwa matakwa yake akaamua sasa kupandikiza mgogoro ndani ya Chama cha CUF. Chama cha CUF hakina mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke sawa, mama yangu mmoja pale alifananisha mgogoro wa Chama cha CUF na ndoa ya mtu na mke wake, akasema kwamba mambo ya mtu na mkewe yanamalizwa chumbani. CUF haikuwa na mgogoro, mgogoro huo ulimalizika mapema Profesa kajiuzulu, Mkutano Mkuu wa Chama ukaitishwa, *quorum* ikaridhika kwamba Profesa kajiuzulu kama Katiba inavyozungumza, ya nini leo Msajili kufanya haya? Tena angalia sasa cha kushangaza, Msajili wa Vyama vya Siasa anatambua vikao vile na mkutano ule ulikuwa halali lakini anasema maamuzi yake ni haramu. Maana yake ni sawa na kusema nguruwe haramu, lakini mchuzi wake halali, hii haiingii akilini, kwa makusudi akaamua kufanya alivyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi cha ajabu zaidi Msajili huyo wa Vyama vya Siasa alikuja kwenye Kamati, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, kama Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria tulimuuliza sheria hizi umezitoa wapi? Nashukuru Kamati yangu imeandika kama miongoni mwa maazimio, ukurasa wa 30, Kamati pia inaagiza Ofisi ya

Msajili wa Vyama vya Siasa kutoingilia migogoro ya vyama vya siasa, si jukumu lake. Migogoro ya vyama vya siasa viachiwe vyama vya siasa, Msajili asiwe ni sehemu ya mgogoro wa chama cha siasa. Chama kina taratibu, sheria, Katiba na kanuni zake, leo iweje yeye apange? Ni ajabu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi anatushangaza hapa sasa, anakuja kwenye Kamati anajitetea siku ya pili anasema anamtangaza kwamba sasa Sakaya ni Kaimu Katibu Mkuu. Sakaya alishasimamishwa uanachama, Sakaya alishasimamishwa uongozi, leo kwa sababu tu una mambo yako unayatafuta unakuja ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma, naamini unapomtaja Mheshimiwa Sakaya unamsema huyu ambaye ni Mbunge, Kanuni zinakutaka aitwe Mheshimiwa.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Sakaya, Mbunge wa Kaliua, anamtambua kwamba eti ni Kaimu Katibu Mkuu wa Chama, aibu! Katibu Mkuu wa Chama yupo anafanya shughuli zake za kisiasa kama kawaida unashawishiwa, wewe umepanda shetani gani? Aliyekushawishi ni nani? Kakupandikiza nini? Kama kuna mtu anakusukuma au anakushawishi, wewe ni Jaji unapaswa uwe na heshima. Tunasema kama ana ndoto ya kufikiria kwamba Chama cha CUF kinakwenda kufa mikononi mwake, Chama cha CUF hakifi, kitaendelea kuweko imara na kitaimarika zaidi. Kama anahisi kwamba Chama cha CUF kinakwenda kufa basi hilo alisahau kabisa *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo suala la utekaji. Nchi hii haiko salama tuseme kweli. Asubuhi watu wameomba miongozo umewakatalia ni suala la hatari. Kama unakumbuka kila siku zikienda mbele hali hii inazidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ulinisimamisha kidogo naomba dakika yangu moja ambayo ulinisimamisha...

**NAIBU SPIKA:** Zilikuwa ni sekunde 10 ambazo zimeshaisha.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulishuhudia Salma Said, Mwandishi wa *DW* alitekwa uwanja wa ndege...

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Lucy Magereli atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke ajiandae.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi leo nichangie katika hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na mimi nitajielekeza eneo moja mahsusi kabisa la ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ukurasa wa 10, kuna *quotation* pale alitoa iko kwa lugha ya Kiingereza lakini ilitolewa pia tafsiri isiyo rasmi ambayo na mimi ningependa pia niirejee, nayo inasema hivi; “Ukuaji wa uchumi unakuwa shirikishi unapotokea kwenye sekta ambazo watu maskini wanafanya kazi kama vile kilimo. Unatokea katika maeneo ambayo watu maskini wanaishi, kwa mfano, maeneo ambayo hayajaendelea na yasiyo na rasilimali. Unatumia nyenzo za uzalishaji ambazo watu maskini wanazo, kwa mfano, nguvu kazi isiyo ya kitaalamu na unapunguza bei za bidhaa ambazo watu maskini wanatumia kwa mfano chakula, mafuta na nguo.”

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye kati ya maeneo aliyoyazungumzia kwamba yamefanya vizuri sana ni eneo hili la ukuaji wa uchumi. Maoni yangu mimi binafsi ni kwamba ukuaji wa uchumi hauwezi kuja kama katika uchumi wa leo hatuwezi kuishirikisha sekta binafsi. Sekta binafsi imetengwa kabisa na kwa bahati mbaya kuna baadhi ya kauli ambazo zimekuwa zikitolewa na Kiongozi Mkuu wa nchi ambazo kwa kweli ukizitafakari kwa undani unaona kabisa kwamba kuna *a missing link somewhere* ambayo inatupelekea sisi kwenda kudumaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuombe Mheshimiwa Rais, lakini na Serikali kwa ujumla kwamba ile kampeni yake aliyoianzisha ya malaika waishi kama mashetani, sasa umefika wakati muafaka kwamba kauli hiyo ifutwe kwa sababu ugomvi huo wa kuwataka wale malaika sasa warudi kuishi kama mashetani umegeuka kiama kwa wale wenyewe mnaowaita mashetani kwa maana ya Watanzania wa hali ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaposhindikana sekta binafsi au wawekezaji walioko ndani ya nchi hii kuendesha na kukuza mitaji yao lakini kutoa michango yao katika uchumi wa nchi, mwisho wa siku anayeathirika siyo yule ambaye ni mwenye kipato hicho cha juu ambaye kwa *reference* ya Mheshimiwa Rais ni malaika lakini anayeathirika ni yule ambaye anaitwa shetani. Sasa na mimi kwa sababu niko kwenye kundi hilo la mashetani, naomba nilete ujumbe wangu maalum nikisema tunaomba waacheni malaika waendelee kuwa malaika, waacheni waendelee kufanya zile karamu zao kwa sababu zile karamu, yale makombo yanayodondoka kwenye zile meza za malaika kwetu sisi ndiyo riziki, ndiyo neema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotaka malaika wageuke mashetani, shida kubwa iko kwa Watanzania wa chini. Sasa nastaajabu tunapoona hotuba zinazosema kwamba kuna ukuaji wa uchumi. Tuwaache malaika wanaoshughulika na sekta ya ujenzi waendelee lakini

tuwasaidie waweze kuendelea kwa ustawi kwa sababu wanapofanya kazi zao za ujenzi sisi mashetani tunaokotaokota makombo kwa kupata kazi za ajira za ujenzi lakini wakiagiza bidhaa *in bulk* kwa maana ya bidhaa nyingi basi na sisi tunapata ahueni kwa sababu zinapokuwa nyingi sokoni na sisi tunapata kuzipata katika bei ya ambayo ni ya ahueni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitolee mfano wa mzalishaji na mwekezaji mmoja Bakhressa ambaye katika kibano ambacho amekipata kwa muda mfupi wa Serikali ya Awamu ya Tano, amebadilisha kabisa mkakati wake wa uwekezaji na kwa kiasi kikubwa mtaji wake sasa anauhamishia maeneo mengine ya Afrika kwa maana ya nchi nyingine za Afrika. Hatua hiyo tu inaleta ujumbe *straight* kwamba kuna ajira ambazo zimeathirika. Kuna hao mashetani sasa ambao kwa yule malaika Bakhressa kuadhibiwa na kupangiwa kodi ambazo haziko *realistic* na masharti mengine ambayo hayatekelezeki kibiashara, amepunguza wafanyakazi lakini zingatieni ndiye anayezalisha mpaka maziwa na maji ya shilingi 500 na sisi mashetani tunapata ahueni ya kunywa maji ya chupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo kama la *Breweries,* tuache malaika hawa wa *Breweries* wazalishe kwa sababu wakizalisha sisi mashetani wa kule mashambani, mazao yetu ya ngano na shairi yanapata soko la uhakika. Pia wale wanaojishughulisha na shughuli za usafirishaji na sisi vijana wetu wako kwenye kuwa madereva wa hayo magari lakini wako katika kuwa utingo wa hayo magari na kutoka hapo na sisi tunapa riziki na vijana wetu wanakwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo kwa mfano la bandari. Wakati bandari ina-*operate* katika kiwango chake ilitusaidia sana sisi tunaoitwa mashetani kupata kiasi kikubwa cha ajira na vijana wetu kutumika katika eneo la bandari ambapo kwa sasa kutokana na kiwango cha uingizaji na utoaji wa mizigo kushuka, vijana wengi sana wamepoteza ajira bandarini. Vilevile yale magari yaliyokuwa yanaondoa mizigo bandarini na kupeleka mikoani na nchi za jirani napo

palikuwa kuna kundi kubwa la Watanzania ambao walikuwa wanahudumia kama madereva, utingo lakini mama ntilie katika maeneo tofauti walikuwa wanapata riziki zao kutokana na eneo hilo. Naamini sasa nimeeleweka ninapojaribu kusema ya kwamba tuwaache malaika waendelee kuwa malaika kwa sababu sisi mashetani tunapotea kwenye karamu za meza zao, wanapodondosha na sisi ndiyo tunaishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata taarifa juzi kupitia vyombo vya habari kwamba *Private Sector Foundation* wanakuja Dodoma kwa ajili ya kuonana na Serikali, naamini taarifa hiyo mnayo. Nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, hao ndiyo watu ambao unatakiwa kuwapokea na mimi sijui niombe kama Mheshimiwa mwingine aliyesema, muache Waziri Mkuu atusikilize. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hawa watu wa *private sector* wanapokuja Dodoma kuja kuonana na Serikali wapewe fursa, wapewe usikivu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli naomba usubiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna mambo ambayo kwa kuwa hii bajeti inahusu Ofisi yake anayasikiliza, niliwaomba mumpe nafasi. Kwa hiyo, naomba tukiongea naye tuchukue muda mfupi apate muda wa kusikiliza Wabunge wanayoyaelekeza kwake. Mheshimiwa Magereli malizia dakika zako zilizobaki. *(Makofi)*

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilimaanisha kumueleza Waziri Mkuu nilisikia kupitia vyombo vya habari kwamba *The Private Sector Foundation* wanakuja Dodoma kuja kuonana na Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba uwapokee hao watu na uwasikilize kwa sababu kama nilivyosema awali makombo ya kwenye meza za karamu zao kwetu sisi ni neema. Hebu acheni *private sector* sasa ishamiri, itoe ajira kwa Watanzania, izalishe bidhaa nyingi

ili bidhaa zishuke bei lakini muwape na *access* ya ku-*import* ili bidhaa ziwe nyingi kwenye masoko na kwenye mzunguko ili na sisi tunaokuwa *referred* kama mashetani, naupenda sana huo msemo sana kwa sababu ni fahari kweli kuitwa na Rais wako kwamba wale wote ambao tuna kipato cha chini basi sisi ni mashetani na sisi tupate kuneemeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka niende kwenye suala moja la msingi ambalo nimeliona na niombe *attention.*

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, kuna suala limejitokeza ambalo naendelea kulistaajabiwa. Jambo hili ni kwamba, Mheshimiwa Rais ametoa kibali kwa mwekezaji mmoja wa hapa Tanzania, Dangote, achukue mgodi wetu wa makaa ya mawe, achimbe mwenyewe, asafirishe mwenyewe, atumie mwenyewe, huu ni utaratibu gani? Huu ni wizi wa namna gani wa wazi na hadharani? Sasa leo tunahangaika na mchanga wa *ACACIA* bandarini nimeona mpaka leo Tume imeundwa wakati kuna mahali tumemfungia fisi buchani halafu tutamuuliza umekula kilo ngapi? Hivi uwezekano huo kweli upo?

**MBUNGE FULANI:** Haupo.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshmiwa Naibu Spika, kati ya mambo sasa ambayo Bunge hili linatakiwa liisimamie Serikali na kulitazama upya ni hili suala la Mgodi wa Makaa ya Mawe. Haya ni kati ya makosa makubwa kabisa ambayo tumeyafanya hata kama lengo ni kumbembeleza mwekezaji basi hapa tumekwenda kinyume kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo lingine la wawekezaji na mitaji yao. Kauli za Mheshimiwa Rais zimeendelea kuwa tata kila mara na kusababisha wawekezaji wengi kupata mashaka kuhusu mitaji yao wanayoiwekeza ndani ya nchi hii lakini na wanaotaka kuja sasa na wao wanaongeza mashaka ya kwamba wawekeze ama la.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru ingawa naona muda umekuwa mfupi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Magereli. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, lakini kabla hajasimama kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa, mashetani haimanishi maskini na kila mtu mwenye dini yake anajua maana yake. Nalisema hili ili kumbukumbu tu zikae sawa maana wengine hatupendi kuitwa mashetani na wale walioko nje pia hawapendi kuitwa mashetani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ni kauli ya Rais.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani ajiandae.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuwa miongoni mwa wachangiaji katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wachangaiaji waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa *speed* tunayokwenda nayo sasa hivi. Niwatie moyo kwamba endeleeni kukaza uzi mambo yanakwenda barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia upande wa kilimo. Sisi wote tunatambua kwamba asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo kwa zaidi ya asilimia 85. Hata hivyo, ukiangalia hali halisi ya Serikali kutilia maanani suala hili sijaona. Serikali haijazama kwa undani zaidi kuona kwamba kilimo ndiyo kinachoweza kuwasadia Watanzania hawa wengi na mtiririko wa vijana wengi wanaomaliza vyuo

vikuu hatutaweza kuwaajiri wote wangeweza kukimbilia kwenye kilimo kama tungeweka mipango yetu vizuri. Kilimo kinalipa kwa mtu ambaye atakuwa amejipanga vizuri na Serikali imeweka mazingira mazuri. Kwa hiyo, naiomba Serikali itilie maanani sana upande wa kilimo ambacho ndiyo kinaweza kuokoa Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu mbolea na pembejeo. Toka nimeingia katika Bunge hili sijawahi kuona mwaka ambao pembejeo kwa maana ya mbolea na mbegu imewahi msimu wa kilimo hata siku moja. Ni miaka yote imekuwa ikichelewa na sijajua ni kwa sababu gani. Kama tuna dhamira thabiti ya kuwasaidia wananchi tupeleke pembejeo kabla ya msimu kuanza. Ningefurahi mwaka huu jambo hili iwe ni mara ya kwanza Serikali kuwahisha pembejeo kwa wakulima kabla ya msimu kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine la kupeleka mbegu *fake* na dawa *fake* za palizi. Yapo maeneo ambayo yanatengeneza mbegu *fake* na dawa *fake* za palizi wakulima wetu wananunua na kwenda kuyatumia yanatia hasara kubwa sana. Naomba vyombo vinavyohusika vijaribu kufuatilia makampuni haya ambayo yanapeleka mbegu *fake* na dawa *fake* za palizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado lipo tatizo kubwa la upungufu wa ardhi katika maeneo mbalimbali. Vijana wengi wanapenda kulima, lakini lazima tukubali baadhi ya maeneo ardhi haitoshi. Hii ni kutokana na watu wachache kukumbatia ardhi. Vilevile Serikali ijaribu kuangalia yale maeneo ambayo tulitenga kwa kazi nyingine iyatoe kwa vijana hawa waweze kujiendeleza kwa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni umwagiliaji. Sisi wote lazima tukubali kwamba kilimo ni sahihi kisicho na *risk* ni kilimo cha umwagiliaji. Huwezi ukalinganisha kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha mvua. Kilimo cha mvua kina *risk* nyingi sana, unaweza ukapata mafuriko, upepo mvua au kukosekana kwa mvua. Ndiyo maana hata benki ukienda kuomba mradi wa kilimo kwa kutegemea kilimo

cha mvua hupati mkopo. Ukienda na kilimo cha umwagiliaji utapata mkopo kwa sababu wanajua kwamba ni kilimo cha uhakika.

Naomba Serikali izame kwa undani zaidi kuhakikisha inainua kilimo cha umwagiliaji. Tunayo mito mingi, mabonde mengi, maziwa mengi, kuna tatizo gani la Serikali kutozama katika kilimo cha umwagiliaji ambacho tunajua kwamba ni kilimo cha uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri yangu iliweza kuomba miradi ya umwagiliaji katika vijiji kadhaa vya Uzia, Ilemba, Msia, Milepa hatujawahi kupewa hata mwaka mmoja. Naomba safari hii tuweze kupewa angalau hata kwa mradi mmoja hasa ule mradi wa Mareza ambao una hekta 7,000 ambazo zinaweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao upungufu wa maghala kwa baadhi ya mikoa inayozalisha sana kwa mfano Mkoa wa Rukwa. Ukienda pale kwenye maghala ya Serikali utakuta mahindi yamepangwa nje jambo ambalo ni *risk* mvua zitakapokuwa nyingi. Tungeomba Serikali iweze kujenga maghala ya kutosha katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende Wizara ya Afya, katika ukurasa wa 40, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea vizuri sana kwamba kumekuwa na ongezeko la fedha za kununua dawa kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 kwenda shilingi bilioni 251 mwaka 2016/2017. Tunapongeza kitendo hicho na tunaomba Serikali iendelee kuongeza fedha mwaka hadi mwaka kwa suala la ununuzi wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima tukubali, sera yetu ya Serikali kupitia Chama cha Mapinduzi iliji-*commit* kwamba lazima kuwe na zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kijiji na Wilaya kuwa na Hospitali ya Wilaya. Sera hiyo ilieleweka vizuri sana kwa wananchi na ndiyo maana wamejitoa kujenga maboma mengi sana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kwa sababu wanajua ingeweza

kuwasaidia. Cha ajabu maboma hayo hayajamalizika kutokana na Serikali kutopeleka fedha kwenye halmashauri. Ni nguvu za wananchi na wakati mwingine unakuta Mbunge anajitolea kupitia Mfuko wake wa Jimbo lakini Serikali kama Serikali tungeomba ipeleke fedha ili miradi hiyo iweze kumalizika mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye Jimbo langu kuna maboma karibu 13 ambayo wananchi wamejenga, mengine yamefikia hatua nzuri mengine bado katika vijiji vya Ilambo, Maleza, Kirando, Kiryamatundu, Mtapenda, Kasekela, Lyapoo, Nakazi, Mumba, Jangwani, Kizumbi, Kawila na kasekela. Wananchi wamejitoa kujenga majengo haya, naomba Serikali iweze kupeleka pesa kwenye halmashauri zetu ili iweze kukamilisha majengo haya. Kadhalika, vituo vya afya wananchi wamejitoa michango yao, nguvu zao, wamejenga majengo kwenye Kata za Mfinga, Muza, Ilemba, Kaoze, Kipeta na kalambazite. Tunaomba Serikali ipeleke fedha ili iweze kumalizia majengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ukosefu wa magari ya kubeba wagonjwa katika vituo vya afya. Ninavyo vituo vya afya vinne ambavyo havina magari vya Milepa, Lahela, Mpui na Msandamugano lakini sanasana nizungumzie Kituo cha Afya Milepa ambacho kimejengwa kwenye mazingira magumu kulingana na jiografia ilivyo. Kile kituo kimepoteza akina mama wengi na watoto. Mheshimiwa Waziri Ummy nimekueleza mara kadhaa hata Naibu Waziri nimewaeleza athari kubwa inayotokea ya vifo vya akina mama kutokana na kituo hiki kukosa usafiri. Nina imani kwa maelezo ya leo kwa huruma yako tungeomba uwapatie gari la wagonjwa katika kituo hiki cha afya cha Milepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao upungufu mkubwa sana wa watumishi kwenye zahanati zetu hasa mikoa ya pembezoni. Unakuta zahanati inaongozwa na Mhudumu Muuguzi sasa unategemea nini katika mazingira ya namna

hiyo? Tunaomba Serikali iweze kuliangalia hilo na ikiwezekana kutoa ajira kwa watumishi wenye sifa wa kuweza kuongoza hizo zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nikumbushie maombi ya Halmashauri ya kuomba halmashauri, wilaya na jimbo. Jambo hili wengine wamekuwa wakiona kwamba labda tunafanya mzaha. Mimi nataka nieleze ukweli, kama Watanzania tuna huduma, Mheshimiwa Waziri Mkuu umefika katika maeneo yale, tena nikushukuru sana, hukupangiwa kwenda, mimi ndiye niliyekuomba na ukafika. Hata hivyo, nakuambia, sehemu uliyofika ni moja ya nane ya eneo langu. Ulijionea hali halisi ilivyo, jiografia ilivyo na ukubwa wa jimbo ulivyo. Pamoja na Serikali kuweka msimamo wa kutoongeza maeneo, myaangalie maeneo nyeti kama haya. Mimi nazungumza kwa niaba ya wananchi. Wananchi ndiyo wamenituma nizungumze jambo hili isionekane mimi ndiye ninayezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi wapiga kura zaidi ya 200,000 na idadi ya wananchi karibu 400,000...

**MBUNGE FULANI:** Waaminifu.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** ...waaminifu kwa Chama cha Mapinduzi inakuwaje hawa watu msiwaangalie? Kama tulifanya makosa ya kutoa halmashauri kwenye maeneo ambayo hayana sifa basi yavunjeni hayo mtoe haki kwa wale ambao wanastahili kupewa haki kuliko kuweka kizuizi watu wengine wasiweze kuomba. Mimi nadhani hili ni tatizo kubwa sana katika eneo langu. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uweze kulibeba kama ulivyokuwa umelibeba toka siku ile wala siyo jambo la kupuuza. Wananchi ndiyo kilio chao kikubwa kutokana na mazingira na huduma mbovu wanayoipata kutokana na mazingira yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nililotaka kuzungumzia ni upande wa elimu. Tuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa sayansi kwa shule zetu za sekondari hata

shule za msingi. Vilevile umaliziaji wa maabara ambazo wananchi wameshajenga, tungeomba Serikali iweze kumalizia hizo maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni uanzishwaji wa shule mpya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema kwa kunijalia kusimama kwa mara nyingine ndani ya Bunge hili Tukufu. Haikuwa kazi rahisi lakini Mungu ni muweza wa mambo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wana CCM wenzangu, lakini nikimshukuru Mwenyekiti wa chama changu na viongozi wakubwa wa chama kwa kuniombea. Mimi naomba niseme nitaendelea kuwa mwana CCM mwaminifu, muadilifu kwa kukipigania na kukitetea chama changu mpaka tone la mwisho la damu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu kilimo. Asilimia kubwa ya Watanzania na hasa wanawake, wengi ni wakulima. Ukifanya sensa utawakuta wanawake wa Tanzania wanaongoza katika shughuli za kilimo. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba mvua za kwanza ni za

kupandia. Ukichelewa kupeleka mbegu wakati mvua zinaanza kunyesha wananchi hawawezi kupata mazao mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi wananchi walipanda bila pembejeo kwa sababu zilichelewa kwa maana ya mbegu, dawa na mbolea kwa ujumla. Hata wakati mwingine waliweza kupanda kwa kutumia mbegu ambazo ni tofauti na mbegu walizotegemea kupata, kwa hiyo, sehemu nyingine mazao yao hayakuweza kuwa mazuri. Naomba basi Serikali ijitahidi kuwahisha kupeleka pembejeo. Vilevile kutokana na ufinyu wa bajeti ya Wizara ya Kilimo, mwaka huu wananchi wengi hawakuweza kupata mbolea, walipata mbolea kiasi kidogo sana ambayo haikuweza kuwatosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hekima yake. Namshukuru sana kwa sababu leo hii ameweza kukutana na mawakala wa Tanzania walioweza kuwawakilisha wenzao akakaa na kuzungumza nao. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usikivu wako. Kutokana na kazi ulizonazo isingeweza kuwa rahisi kuweza kuwakubalia kukaa nao, lakini umetumia nafasi yako kuweza kuwasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kutokana na jinsi ulivyowaahidi, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, watakapokuwa wamefanya utafiti, najua wako mawakala wengine sio waaminifu, tunafahamu wapo wengine ni waaminifu na wengine sio waaminifu. Kwa hiyo, wale ambao ni waaminifu watendewe haki na wale ambao sio waaminifu, wachakachuaji wasiwaponze wenzao, wale ambao watakutwa wamefanya vizuri, hawakuweza kuliibia taifa hili waweze kulipwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitumie nafasi hii Mheshimiwa Waziri Mkuu kueleza kwamba wananchi wengi walikopa wakati wanafanya kazi ya uwakala. Naomba muwasaidie kuwaombea kule kwenye mabenki wakati wanasubiri kulipwa haki zao mabenki yale yaweze kusitisha

kuuza mali zao ili watakapopata pesa zao waweze kwenda kulipa mikopo yao. Mheshimiwa Waziri Mkuu, chonde chonde kupitia Waziri wa Fedha, tunaomba aongee na mameneja wa mabenki mbalimbali ambako wananchi walikopa mikopo, waweze kusubiri. Wananchi watakapokuwa wamelipwa madeni yao waweze kwenda kulipa madeni yale kwenye mabenki, watu wengi wanapoteza maisha kwa sababu mtu akiuziwa nyumba yake na hana njia nyingine, hana nyumba nyingine anapoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu vituo vya afya na zahanati. Tuliahidi kujenga zahanati na vituo vya afya katika kila kijiji na kila kata. Kwa bahati mbaya yapo majengo ambayo tayari yalishajengwa hayajaweza kukamilika na ili yakamilike Halmashauri ndizo zinazotakiwa kujenga yale majengo na Halmashauri hazina pesa. Naomba Serikali isaidie Wizara ya Afya ili Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Halmashauri waweze kupeleka pesa kumalizia vituo vile vya afya na zahanati zilizoko kule kwenye vijiji na kata zetu ilia kina mama na watoto waendelee kupata huduma bora kutokana na vituo vitakapokuwa vimefunguliwa katika Wilaya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wanawake wa Tanzania. Wanawake wa Tanzania wameweza kuungana pamoja wakaanzisha vikundi mbalimbali, wakaanzisha vikundi vya *SACCOS* na *SACAS.* Naomba niseme vikundi vilivyo vingi havina elimu, vinaishia kukopeshana vyenyewe kwa vyenyewe kwa sababu havijaungana pamoja na hakuna sheria ambayo imeshaundwa kwa ajili ya kuvilinda vikundi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi Serikali iweze kutunga sheria mahsusi ili vikundi hivyo viweze kuendeshwa kitaalam na viungane pamoja kusudi viweze kutambulika katika mabenki hatimaye viweze kukopesheka kwa sababu mabenki siyo rafiki wa maskini. Wale wenye vikundi hawajaweza kwenda kufungua akaunti kwenye benki, wanakopeshana wao wenyewe huko mitaani kila baada ya mwaka wanafanya sherehe, wananunua nguo mpya,

wanapika wali, wanavunja vikundi wanagawana na benki kama hawana sehemu ambayo wataenda kuangalia vikundi vinafanyaje hawawezi kukopesha wanawake hao na vikundi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia kuhusu maliasili na utalii pamoja na Wizara ya Ardhi. Waliahidi kuunda Tume, Tume iliundwa kwenda kutembelea maeneo yenye migogoro, lakini kabla ya matokeo ya ile Tume iliyoundwa baadhi ya watu wamefukuzwa. Tunaomba basi Serikali iweze kufanya haraka kutoa matokeo ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji na kuweza kusogeza mipaka baadhi ya maeneo ili wananchi waweze kupata maeneo ya kulima kwa sababu watu wanaongezeka, ardhi haiongezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia maji kwa sababu mimi ni mama nafahamu adha wanayokutana nayo akina mama vijijini na hata mijini. Mwaka jana Mkoa wa Kigoma tulitengewa fedha za kutosha, lakini mpaka sasa hivi bado tuna tatizo la maji hasa Wilaya ya Kasulu ninayoishi mimi yako maeneo ambayo maji hayajaweza kufika. Katika eneo la Kibondo maji bado ni tatizo pamoja na Kakonko. Kwa hiyo, naomba zile pesa zilizotengwa, zisiondoshwe mahali pale ziweze kurudishwa Kigoma zikafanye kazi kuwaondolea adha wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho nataka kuzungumzia kuhusu barabara. Mara nyingi pesa za kutengeneza barabara zimekuwa zikipangwa lakini wakati mwingine hazipelekwi jinsi zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi pesa zinazopangwa kwa ajili ya barabara za Kigoma ziende jinsi zilivyo ili tuweze kukamilisha barabara ambazo zimeshaanza kujengwa na hasa kipande cha kutoka Uvinza kwenda Malagarasi, Malagarasi kwenda mpaka Kaliua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa John Peter Kadutu ajiandae.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa taarifa yake na hotuba yake ya bajeti hii ambapo angalau tunaona mwelekeo kidogo ukisimamiwa mambo yataweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niwashukuru Mawaziri ambao wamo ndani ya Wizara hii Ofisi ya Waziri Mkuu, swahiba yangu pale dada Mheshimiwa Jenista, lakini vilevile na kaka Mheshimiwa Mavunde kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujielekeza kwenye mambo matatu makubwa ambayo nahisi kama nchi tunaweza tukaleta mabadiliko. La mwanzo niombe ofisi yako na tuiombe Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ujumla ili nchi hii kuinusuru na janga kubwa la njaa ambalo linatokea katika maeneo mbalimbali ambalo hasa linasababishwa na tatizo la hali ya hewa lazima tuwe na kilimo cha umwagiliaji maji, hatuna njia ya mkato. Mataifa yote ya wenzetu wengine mkakati uliokuwepo ni kuwa na kilimo cha umwagiliaji maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Novemba mwaka jana tulishiriki kwenye *Agriculture Council* ya *SADC* nchi zote zinazotuzunguka tamko lao limejielekeza kwenye umwagiliaji maji. Napenda kutoa rai tufanyaje katika hili ili tuweze kupata mlango wa kutokea. Niombe Serikali kwa ujumla iridhie kuufufua Mfuko wa Umwagiliaji Maji uwe unachangiwa kama inavyochangiwa mifuko mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko huu ni muhimu na ndiyo dawa ya kuweza kukomboka na kuwa na miundombinu ya umwagiliaji maji. Hesabu ya haraka haraka

kama tutakuwa na wachangiaji wa shilingi 50 tu, tukiwa na wapiga simu au wamiliki wa simu milioni 20 ambao kwa Tanzania tunafika idadi hiyo, pesa ile kwa mitandao mitano iliyokuweko ndani ya nchi tunaweza kuwa na zaidi ya shilingi bilioni 144. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi tunaweza kuwa na maeneo maalum ya kimkakati na mazao ya kimkakati, kila eneo tukaweza kuchimba visima vinane, tukaweza kuwa na zaidi ya hekta 1200, tayari tuna uhakika wa *reserve* ya tani 300,000 za chakula kwa mwaka. Hivyo, tishio la *NFRA* na mazao yale mchanganyiko ya kusema tutanunua wapi chakula, wale watanunua kwa hawa ambao wamewekeza kwenye umwagiliaji maji hivyo Taifa litakuwa na uhakika wa akiba ya chakula na tatizo kubwa la njaa litakuwa halipo katika maeneo yetu, hiyo ni rai yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka kumuomba Waziri Mkuu, kazi nzuri aliyoifanya kwenye Bodi ya Korosho ahamishie kazi ile kwenye bodi nyingine za Wizara ya Kilimo. Kuna matatizo na hakuendi vizuri kwenye Bodi ya Pamba, kuna matatizo na hakuendi vizuri kwenye Bodi ya Kahawa, kuna matatizo kwenye Bodi ya Chai, chai kama kaachiwa limekuwa shamba la bibi tu hamna anayemuuliza mtu. Tulikuwa na Bodi ya Pareto, leo hii tumeanzisha vilevile Bodi ya Maziwa, bodi hizi zinatakiwa zipitiwe, zifuatiliwe, utendaji wao wa kazi ujulikane lakini vilevile yale makato wanayowakata lazima yajulikane yanatumika vipi. Hali ilivyo sasa hivi kama hakuna anayesimamia bodi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Waziri Mkuu mkakati zaidi ulioufanya kwenye Bodi ya Korosho ambapo umewakomboa wakulima na wamerudisha imani wakulima wa korosho tuhamishie kwenye bodi nyingine hizi ili kurejesha imani ya wakulima wa kahawa ambao wengi wao wameacha kulima kahawa kutokana na makato na mazingira mabaya yaliyokuweko kwenye kahawa. Hali kadhalika, tuangalie pamba inakuwaje, chai inakuwaje lakini tusisahau na pareto vilevile. Tulikuwa ba Bodi ya Pareto ambayo sasa hivi hata haizungumzwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa linalotukabili kwenye kilimo ni kutokutilia maanani suala zima la upatikanaji wa pembejeo. Kilimo bila pembejeo hatuna kilimo, ardhi yetu tumeshaitumia imechoka. Serikali kadri tunavyoishauri kuhusiana na pembejeo linaonekana suala lile kwamba ni jepesi na halina uzito wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka juzi nchi ilitenga zaidi ya shilingi bilioni 250 kwa ajili ya pembejeo, zikapatikana zaidi ya shilingi bilioni 120, mwaka jana tumekwenda na shilingi bilioni 20, hali imekuwa tete. Tumetoka kwenye wakulima waliopewa ruzuku ya pembejeo 99,000 sasa hivi tumekuja kwenye wakulima karibu 350, hali ni ngumu. Niiombe Serikali hili suala iliangalie kwa jicho la maana, bila pembejeo utazalishaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito wangu kwamba, Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha hili jambo iliangalie kwa jicho la huruma. Wakulima hawa wana nia ya kuzalisha, pamoja na ukata na hali ngumu ya hali ya hewa lakini ukosefu wa pembejeo nao vilevile unachangia kudumaza maendeleo yao. Hili tulitilie maanani na tuweze kuwasaidia wakulima katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumza ni la mifugo. Nikushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu umeshughulikia vizuri suala zima la mifugo hasa maeneo ya Loliondo. Wafugaji wale wa Loliondo bila Kamati ile wangefikia pabaya, sasa hivi wangekuwa wameshafukuzwa na hawaelewi pa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wafugaji kule wako zaidi ya 64,000 ukiwaondoa pale wana ng'ombe zaidi ya 500,000 wale wanakwenda maeneo ya Morogoro na wanakwenda maeneo ya Kusini kitu ambacho kinakwenda kuchochea machafuko baina ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu, suala hili tuweze kuli-*handle* vizuri kwa sababu bado Wamasai wale wana uwezo wa kufuga ng'ombe na wakatunza zile rasilimali zilizokuwapo pale za hifadhi bila kuathiri na maisha yakaweza kuendelea baina ya wanyama wa porini na wanyama wa kufugwa. Wito wangu, Kamati iendelee na uchunguzi na mkakati wake, lakini ifike mahali uwekwe utaratibu mzuri wa kufuga pasiwe na wazo la kuwafukuza watu wale. Kwa sababu kuondoka kwao sio kama watachinja wale ng'ombe wao, watahama maeneo na hivyo tutaongeza tatizo la ugomvi baina ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia Bodi ya Maziwa. Bodi hii ina malengo mazuri, imesema mwaka huu inataka kuimarisha ng'ombe wa maziwa angalau wafike milioni moja na laki tano. Ushauri wangu tuanzishe *cowshed* au vijiji vya ufugaji ili kuweza kuwapelekea huduma hawa wafugaji ambao watapewa hawa ng'ombe wa maziwa. Tutakapoanzisha *cowshed* hizi itakuwa rahisi kuweza kuwapelekea elimu ya ugani kwa wale wafugaji ambao wataanzisha mabanda haya kwa pamoja lakini vilevile tutaweza kuweka zile *collection centre.* Bado Tanzania inaathirika na maziwa ambayo yanatoka nje, ni aibu jamani! Tanzania hatuna kiwanda cha maziwa ya unga tunashindwa na Zimbabwe walau wana kiwanda cha maziwa ya unga. Tatizo letu ni kwamba maziwa yetu hayana viwango na ng'ombe tulionao hawana uwezo wa kutoa maziwa ya kutosha tukaweza kuanzisha hivyo viwanda tulivyokusudia. Kwa hiyo, kama hatukujipanga kuweza kusambaza ng'ombe wa kutosha katika nchi hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehani muda wako umekwisha.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima James Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa John Peter Kadutu na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nianze na jambo ambalo nisingelianza, lakini kwa sababu kuna mtu amegusa inabidi niseme. Kuna mchangiaji mmoja alizungumzia Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kuzungumza ni kwa namna gani bajeti za Serikali hii zimekuwa hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa bahati mbaya akatolea mifano ya hela ndogo wakati sisi tulikuwa tunaongelea mambo mazito, tulikuwa hatuongelei mambo *peanut*. Sasa nimuoneshe tu ni kwa nini Kiongozi wa Upinzani Bungeni amesema ni hewa, nitanukuu hotuba yetu. Mosi, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilipewa shilingi bilioni 2.2 kwenye Wizara ya Kilimo ambayo ni sawa na asilimia 2.2 ya bilioni 101 ilizotakiwa ipewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Mifugo na Uvuvi ilitengewa shilingi bilioni 1.2 sawa na asilimia 7.9 kati ya shilingi bilioni 15.8. Amekiri mwenyewe muongeaji kwamba kilimo kwa mwaka huu kimekuwa kwa asilimia 2.9 badala ya asilimia sita iliyokuwa ikitarajiwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani akaenda mbele zaidi, akasema tunashangaa kwamba asilimia 70 ambayo inaajiri Watanzania wengi wamepewa asilimia 2.2 wakati eti tumenunua ndege ama kupeleka *advance payment* ya bilioni 128 ambayo inahudumia watu 10,000 tu. Sasa naona kuna Wabunge wanakaa wanalalamika hapa halafu wanashindwa kuiambia Serikali ukweli. *(Makofi)*

Wizara ya Viwanda na Biashara tunaambiwa huu ni mwaka wa viwanda, hii ni Serikali ya viwanda, hii Wizara inatakiwa iratibu wawekezaji waweze kuja, hivi viwanda viweze kupatikana, wawekezaji waweze kuwekeza nchini, imepewa shilingi bilioni 7.2 sawa na asilimia nane ya shilingi bilioni 40 zilizoidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Miundombinu ilipewa shilingi trilioni 1.7 sawa na asilimia 58.7 ya shilingi trilioni 2.1 ambayo Bunge hili lilipitisha; Wizara ya Uchukuzi asilimia 30; Wizara ya Nishati na Madini asilimia 36 na Wizara ya Afya asilimia 25. Hivi mkiambiwa hewa ndugu zangu siyo kweli kwa bajeti nzima ya maendeleo kwa wastani kwa mwaka huu unaoisha ni asilimia kati ya 26 na 34 ambazo zimetolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndugu zangu kama kweli zaidi ya asilimia 70 ya fedha za maendeleo hazijapatikana, mkiambiwa bajeti yenu ni hewa mnakasirika nini? Kupanga ni kuchagua, tujue uwezo wetu ni upi, tujipange kutokana na uwezo wetu ili tujue tunaendaje mbele kama Taifa. Ndugu zangu niwaombe wanaopitapita huko mbele wanaambiwa nenda katetee ni hivi, hapa hakuna cha kutetea, hatetei mtu hapa, yaani huu mwaka mmoja wa Mheshimiwa Magufuli na Serikali yake kwenye bajeti ya maendeleo mmechemka, tukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Halmashauri zetu, tukiacha kuwa wanafiki hapa ni vilio, mwaka jana Serikali ilikuja kwa mbwembwe hapa tunachukua *property tax,* tumejipanga vizuri wakijua kwenye Halmashauri nyingi za miji hicho ndio moja ya vyanzo wanavyovitegemea, kwa mbwembwe nyingi huu mwaka umeisha. Mimi nimetoka juzi kwenye Baraza letu la Madiwani, tunapoenda bajeti nyingine ya mwaka huu hakuna hata shilingi moja iliyotoka Serikali Kuu *kwa property tax.* Wakati wenyewe tulikuwa tuna uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 10, tulikusanya mwaka mmoja ule uliopita, tumepanga kukusanya mwaka huu Serikali imechukua pato hamjaturudishia pato, shughuli za maendeleo zinakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi ni wa Mjini ambao japo tuna vyanzo vingine, sasa wenzangu na mimi wa vijijini mkikaa hapa mnapiga makelele, mnapiga makofi, oyaoya hatutawanyoosha hawa Mawaziri ili waweze kuwajibika vizuri kwa Bunge. Kwa hiyo, mimi niombe kati ya kipindi ambacho Wabunge tunatakiwa tuwe wamoja kuisaidia nchi yetu na

siyo kulinda Serikali yetu, kuisaidia nchi yetu ni kipindi cha bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, suala la mauaji na utekaji unaoendelea. Asubuhi ilitolewa hoja hapa na Mheshimiwa Hussein Bashe, ukaikatiza hoja, mimi ninaamini kwamba Spika wetu huko anasikiliza. Ninaamini mtu mwingine akija akitoa hoja hiyo hiyo Spika wetu akija ataweza kulitendea haki hili jambo. Nadhani umeona ni jambo zito sana ukasema ngoja kwanza nimsikilizie bosi wangu akija atasema nini, inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli zinapotolewa na watu wazito na ninashukuru hili suala halina chama, linatoka upande wa CCM na linatoka kwa upande wa Kambi ya Upinzani. Kwa sababu CCM wanaamini miongoni mwa watu wa Serikali hii kuna watu wana nia njema na Taifa hili, vilevile wanajua kuna watu miongoni mwa Serikali hii hii wanafikiria wao wako juu ya sheria, kwa sababu fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunasema haya mambo lazima tuyajadili, kama Bunge lisipojadili, kama Bunge linaogopa kujadili leo, nani ajadili. Nilimsikiliza Mheshimiwa Nape akiongea Mtama, alikuwa ni Waziri Mheshimiwa Nape alitoa kauli nzito, kauli ambayo inaonesha kwamba kuna watu ndani ya Serikali wanatumia genge la Usalama wa Taifa kuteka watu, kufanya mauaji. Huyu ni *former Minister,* siyo mtu mdogo, wiki mbili zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Bashe amezungumza, mimi kwangu Mbunge wa CCM akizungumza ni kama Serikali inazungumza, *that is my opinion* kwa sababu ninaamini hakuna Mbunge yeyote makini wa kutoka Chama Tawala akasema kitu ambacho hana uhakika nacho.

Mheshimiwa Bashe amerudia amesema kuna genge ndani ya Usalama wa Taifa linashirikiana na bahati mbaya anatajwa dogo sijui Bashite yule, wamekuwa wakimtajataja kwamba Bashite ndiyo anaongoza hili genge. Sasa tunajiuliza

sasa kama Bashite anaongoza genge, kama Bashite anasemwa hachukuliwi hatua, juzi ambaye alimtolea Mheshimiwa Nape silaha lile gari lililombeba limeonesha limesajiliwa kwa namba ya Ikulu, halafu watu wanakauka tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Rais anajua? Sisi hatutaki ionekane Rais anajua, ndiyo maana tunasema hili Bunge likaondoe mzizi wa fitina, kwa sababu inaoneka Mheshimiwa Mwigulu ngoma imeshamshinda na ndiyo jukumu letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaambiwa kuna Wabunge 11 ni *wanted,* hivi kweli viongozi wetu mnaambiwa kuna Wabunge 11 *wanted* na imetoka kwenye *proper authority,* hakuna mtu yeyote aliyesimama hapa akamwambia thibitisha, futa kauli yako sisi tunajuana, yaani huku ndani tunajuana, sindano ikigusa pale pahali pake inabidi kila mtu anakaa chini anatulia, hakuna mtu aliyepinga kile kilichosemwa. Kwa hiyo, je, tusubiri aanze kufa Mbunge mmoja mmoja ndiyo tuunde hii timu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ben Saanane kijana wetu amepotea, zikaanza kupigwa propaganda eti CHADEMA tunajua alipo. Sasa kama mnajua sisi wauaji kwa nini msitukamate mtuweke ndani? Kwa nini maisha ya watu tunachukulia *simple?*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ben Saanane aliandika waraka tarehe 8 Septemba, 2016 naomba ninukuu, kaandikiwa na namba ifuatayo; “Ben Saanane unachokitafuta ndani ya Serikali hii utakipata kwa elimu na uwezo wako hatukutarajia ungefikia hatua ya ajabu kwa namna uliyofikia hujiulizi kwa nini upo huru hadi muda huu, *your too young to die.* Tunajua utaandika na hii, andika lakini *the next force* hutaandika ukiwa na uhuru wa kutosha. Andika *but your days are numbered,* unajua kuna rafiki yako alipuuza na hatutaki kuandika kuhusu yeye labda kwa kuwa alitangulia, andika Ben, andika sana, ongea sana lakini utajikuta mwenyewe.”

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji )*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu haujaisha, kengele ya kwanza sijaisikia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, mimi naongozwa na Makatibu ndiyo wanaogongesha kengele siko nayo hapa juu iko hapo chini, kwa hiyo kama wao wamegonga ya pili ndiyo maana nimeku-*alert* kwa maana ya kwamba malizia sentensi muda wako umekwisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namba iliyomwandikia ni 0768 79982 hii namba polisi wanaijua, Serikali mnaijua, mkitaka ku-*trace* watu...*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante Mheshimiwa Halima Mdee.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa John Peter Kadutu atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki ajiandae.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niseme kidogo, leo sina maneno mengi wala mapepo hatuyatoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utangulizi ninaotaka kusema nataka kuhubiri juu ya amani. Amani ni kitu muhimu ambacho hakuna mwenye dhamana zaidi ya Watanzania wote. Viongozi wa kisiasa, mwananchi mmoja mmoja tunapaswa kuilinda amani bila kujali itikadi zetu na bila misimamo ya kimihemuko na ushabiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za karibuni na hasa wanasiasa tumekuwa na matamko mbalimbali yanayoashiria kupoteza amani, vitisho mbalimbali vinatokea na matukio mbalimbali kama haya ya utekaji na mambo kadha wa kadha ambayo lazima kama Wabunge humu ndani tuyakemee kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa miaka miwili na nusu iliyobaki, nasema iliyobaki kwa sababu mwaka 2020 sitagombea Ubunge, nitaendelea kuhubiri amani na baada ya kumaliza Ubunge nitaendelea na kazi ya kuhakikisha amani inaendelea kupatikana, hiyo ni njia sahihi ya kuwakumbusha Watanzania wote juu ya amani. Watu mbalimbali tumekuwa na matamko ambayo napata taabu sana. Kwa hiyo, nilitaka kuwakumbusha wenzangu juu ya umuhimu wa amani, kila mmoja anatamka anavyoweza na kila mmoja ana uhuru wa kutamka anayoweza lakini lazima tuwe na akiba ya maneno, tuwe na vifua vipana vya kuhifadhi maneno, lakini kutafakari athari za maneno tunayoyatamka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nichangie kidogo juu ya hotuba ya Waziri Mkuu. Watu wa Tabora na Jimboni kwangu Ulyankulu, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakupongeza sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya juu ya zao letu la tumbaku, Bodi ya Tumbaku, Bodi ya *WETCU* na kwa sababu umeahidi kwamba utakuja sasa kumalizia kazi hizo tunakukaribisha kwa niaba ya wenzangu wote tunakuunga mkono kwa hatua mbalimbali unazozichukua. Huu ushirika umekuwa na shida, ushirika ulivunjwa, ukarudi lazima sasa Serikali iwe karibu sana na ushirika na hasa hawa Warajisi wa Ushirika Mikoani, ni watu ambao wakati mwingine wanasaidia kuharibu nia njema ya ushirika na tukukaribishe tena Tabora na utusimamie vizuri hasa uanzishwaji wa vyama vyetu vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani nyingine ni kwa niaba ya Wabunge wenzangu wenye ulemavu, nitoe shukrani kwa Katibu wetu wa Bunge na Sekretarieti yake kwa kuwa karibu na sisi Wabunge wenye ulemavu. Ofisi ya Katibu wa Bunge imekuwa ikiratibu mambo mbalimbali toka tukiwa na Mheshimiwa Possi na sasa tunakwenda vizuri, lakini tuombe tu Ofisi ya Katibu waweze kutekeleza ombi ambalo tulitoa kwamba Ofisi ya Utawala itengenezewe *lift* kuwawezesha Wabunge wenye ulemavu kuweza kufika kule juu kuliko na ofisi mbalimbali za Utawala, tuna imani Katibu wa Bunge atakuwa amelisikia, tunafanya kumkumbusha jambo ambalo tulilizungumza huko mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine Mheshimiwa Waziri Mkuu ni juu ya uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala. Ukiuchukua Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Tabora eneo lote lile lilikuwa Mkoa wa Tabora limeendelea kukatwa polepole na sasa bado Mkoa wa Tabora ni Mkoa mkubwa kulikuwa Mikoa yote Tanzania. Lakini hapa katikati Serikali imekuwa inatoa maeneo sisi kazi yetu tunasikiliza tu, mara mmekata Mkoa gani mmewapa, lakini Tabora hamtaki kuugawa Mkoa, kwa sababu ni Mkoa mkubwa bado tunahitaji Mkoa ugawanywe hata kama tuna azma ya kupunguza matumizi, Wilaya zetu ni kubwa, ukiichukua Wilaya ya Uyui peke yake inaweza ikakusanya Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Tanga ikawa sawa na Wilaya ya Uyui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua Wilaya ya Kaliua inaweza kuwa sawa na Mkoa pia wa Kilimanjaro na Tanga kwa pamoja. Kwa nini sasa tukazingatia tu kwamba tunataka kubana matumizi. Mheshimiwa Waziri Mkuu tuombe sana, Ulyankulu tumeomba Wilaya, tumeomba Halmashauri na jambo hili Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni aliahidi kwamba siku tatu tu zingemtosha kutoa uamuzi sasa tuna mwaka mmoja na nusu bado tu hamjatafakari kutupa Wilaya? Bila shaka ujumbe umefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu nimalizie sitaki kuwa na maneno mengi na sitaki kumaliza dakika zangu zote, kwa niaba ya *TFF* nitoe shukrani kwa Serikali pamoja na *TRA* kwa kumaliza mgogoro ambao umekuwepo hata kama haujaisha moja kwa moja lakini hatua iliyofikia kati ya Shirikisho la Soka nchini pamoja na *TRA* liko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa katikati tuliona na kusikia kwamba *TRA* iliweza kuwateremsha vijana wetu mashujaa wetu wa *Serengeti Boys* kwenye basi kisa deni, mpaka pale mamlaka zingine zilipoingilia kati. Mchana huu nilikuwa nawasiliana na Ndugu Malinzi, Rais wa *TFF* ameniambia kwamba tuko vizuri pamoja na Serikali pamoja na *TRA* juu ya jambo hili. Kwa niaba ya wadau wote wa

mpira na michezo kwa ujumla Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru kuweza kulirahisisha jambo hili ili watu wafanye kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kumaliza dakika zangu na inanitosha. Wengine kwenye Wizara na Taasisi nyingine tutakutana mbele ya safari. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mheshimiwa Antropia Theonest ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi siku ya leo kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza naunga mkono kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono nataka nianzie kwenye jambo la vijana, Serikali imeagiza Halmashauri zetu kutoa asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa akinamama, jambo hili kiutekelezaji bado linaendelea kuwa gumu, maeneo mengi Halmashauri zetu hawatekelezi ipasavyo kwa hiyo, inasababisha kudumaa kwa maendeleo katika maeneo yetu ambayo tunatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wazee kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tulihubiri sana. Suala la posho ya wazee zaidi ya miaka 65, lakini mpaka leo utekelezaji wake bado haujaonesha dalili kwamba jambo hili litafuatiliwa na wazee wetu kuanza kupewa posho kama tulivyoahidi kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la elimu katika maeneo mengi tunashukuru kiasi ambacho kinatolewa na Serikali kwa ajili ya kuwapinguzia mzigo wazazi, lakini changamoto kubwa tunayopambana nayo katika maeneo yaliyokuwa mengi, hasa Jimboni kwangu, ni juu ya uchakavu wa majengo ya madarasa ya shule za msingi na sekondari katika maeneo karibu yote yaliyopo katika maeneo ya Jimbo langu. Shule hizi zilijengwa miaka ya 1975, 1970, 1980, zilizo

nyingi zina umri mkubwa, pengine Wabunge wengine humu ndani walikuwa bado hawajazaliwa, kama ilivyo mdogo wangu Mheshimiwa Goodluck.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa majengo yale yamechakaa, yanapaswa tena kutokana na ongezeko la wanafunzi lilivyo, tuongeze mapya na haya ya zamani yaweze kukarabatiwa ili yawe na hadhi ya kuweza kusomesha watoto wetu katika madarasa yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna upungufu mkubwa sana wa walimu, hasa katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Tunduru tuna upungufu mkubwa wa zaidi ya walimu 650 ambao wanapaswa kuwepo katika madarasa kwa sababu maeneo mengi katika shule zangu za msingi walimu hawazidi wanne, watatu, shule chache zina walimu watano mpaka sita. Jambo hili linairudisha sana Halmashauri yetu ya Tunduru kielimu kwa kuwa watoto wamekuwa wengi lakini kuna upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, walimu wa awali kwa ajili ya madarasa ya awali hakuna kabisa, anachukuliwa mtu ambaye ana *idea* kidogo anaenda kufundisha, naomba Serikali ione umuhimu wa kuwafanya walimu wa awali waweze kupata mafunzo, waweze kuwafundisha watoto wetu ili waweze kuwahudumia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea zaidi ni suala la afya katika maeneo yetu. Kwa kweli kuna upungufu mkubwa wa zahanati katika Jimbo la Tunduru Kusini na Jimbo la Tunduru kwa ujumla. Jimboni kwangu kuna vijiji 67, lakini ni vijiji 24 tu ambavyo vina zahanati. Pamoja na kuwepo zahanati hizo 24 bado watumishi katika zahanati hizo ni wachache sana. Kuna watumishi wasiozidi wawili kila zahanati jambo hili linatia doa sana kwa wananchi wetu kwa sababu wanashindwa kupata huduma ile kwa uhahika zaidi kwa sababu idadi ya watumishi katika zahanati hizo imekuwa ni ndogo kwa hiyo, hawapati ile huduma inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru tuna Hospitali moja ya Mbesa ambayo miaka ya nyuma, wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne, Rais aliahidi hospitali hiyo kuwa hospitali teule kwa niaba ya watu wa Tunduru Kusini. Hospitali ile inahudumia asilimia 80 ya wakazi wa Wilaya ya Tunduru na Halmshauri yake, lakini idadi ya waganga wako watatu tu. Naomba Serikali kulingana na mikataba iliyokuwepo na Hospitali ile ya *mission* basi itekelezwe kuongeza ikama ya idadi ya wafanyakazi wanaotakiwa katika hospitali ile ili waweze kuhudumia watu wetu wa Tunduru kwa ujumla na Wilaya ya jirani ambayo inategemea hospitali ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea, ni suala la kilimo. Tumepiga kelele sana ndani humu, jambo la pembejeo, katika hotuba ya Waziri wa kilimo mwaka jana, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alizungumzia suala la pembejeo kuuzwa madukani kama soda, ninaomba Serikali ituambie imekwama wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa ruzuku unatugombanisha wakulima na Serikali yao, inagombanisha wakulima na Wabunge, Unagombanisha wakulima na Madiwani, kwa sababu wale wanaochaguliwa kupewa zile ruzuku wanakuwa ni wachache kulingana na idadi ya kaya zilizopo katika kila kijiji. Naomba sana, mpango ule ulikuwa ni mzuri, kila mtu atakayekuwa na uwezo ataenda kununua pembejeo ile dukani kulingana na hali ilivyo. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikafikiria namna ya kutoa ruzuku katika viwanda vyetu vinavyozalisha pembejeo ili viweze kutoa asilimia 100 kwa pembejeo zote zinazozalishwa katika viwanda vile na kusambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukazungumzia wakulima ukaacha kuzungumza suala la ushirika. Ushirika huko vijijini ndiyo unaosaidia sana wakulima wetu katika maeneo yaliyokuwa mengi. Hata walio wengi, Wabunge na Madiwani, wametokea katika sekta hii ya ushirika, lakini bado kuna jambo ambalo linafanywa, Serikali bado haijaweza kuiimarisha Tume ya Ushirika ili iweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba Serikali ihakikishe Tume hii inapewa meno kwa kuipa viongozi wanaotakiwa kwa maana ya Mwenyekiti wa Tume na Wajumbe wake ili waweze kusimamia ushirika huu uweze kufanya kazi vizuri. Mbili, naomba Serikali ihakikishe kwamba, watumishi wa Tume wanaenea kutoka Mikoani mpaka Wilayani ili kuhakikisha kwamba wanasimamia ushirika ipasavyo, wakulima waweze kupata tija katika mazao yao wanayozalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta kwamba kwa mfano sekta ya korosho wanaushirika wengi wanajiendesha bila usimamizi wowote, hata kama ni mtoto wako umempa ndizi kila siku anaanza kuuza sokoni, anakaa mwezi mzima hujamtembelea ukajua amepata shilingi ngapi, siku ukimuuliza atakupa majibu ambayo hayataendana na wazo lako amepata kiasi gani kwa muda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili linaendana pamoja na ushirika, tunawatumia hawa kwa muda wote, lakini kwa sababu wamekosa usimamizi wa biashara yao kwa muda wa miezi mitatu, minne tunaporudi kuwahakiki tunakuta kuna matatizo mengi, wakulima wanakosa malipo yao bila maelezo ya kutosha kwa sababu Maafisa Ushirika wa kusimamia zao hili la korosho wanakuwa ni wachache kwa kipindi kile cha msimu wa korosho wanashindwa kuwasimamia kuhakikisha kwamba pesa wanayopelekewa inanunua korosho kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa sana niliongelee ni mgawo wa maeneo ya utawala. Tunduru ni kubwa sana, inalingana katika eneo la ukubwa na Mkoa wa Mtwara na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imeanza tangu 1905. Mkoa wa Ruvuma naamini ndiyo Halmashauri ya kwanza, lakini kuna Halmashauri tano, saba zimezaliwa Tunduru iko palepale. Kutoka eneo moja mpaka lingine naamini Naibu Waziri wa TAMISEMI amefika pale ameona. Kutoka mwanzo mpaka mwisho kilometa 200 unatembea mtu anatafuta huduma kwa ajili ya Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maombi yetu yafikiriwe tuhakikishe kwamba, Majimbo yote mawili yanakuwa na Halmashauri zinazojitegemea ili tuweze kuwahudumia watu wetu kwa haraka. Kwa sababu tunavyozungumza zahanati kama nilivyozungumza mwanzo ziko 24, mtu anatembea zaidi ya kilometa 30 hadi 40 kufuata huduma za afya. Utapozungumza hospitali ya Wilaya iko zaidi ya kilometa 80 hadi 100 ili kuipata hospitali hii. Mkitugawia maeneo haya mambo mengine haya zahanati, hospitali ya Wilaya itakuwa rahisi zaidi kuwahudumia wananchi wetu. Naomba sana Serikali iweze kufikiria mgawo huu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili tuweze kuwahudumia wananchi wetu kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabisa suala la barabara.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate ahsante. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Kasuku Bilago ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa uzalendo na ukweli ndani yake, kwa sababu nilipokuwa nikisoma hakuna chembechembe za *ushilawadu* ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu

kwa ukurasa namba 16 unaosema asilimia 56 ya nguvu kazi ya Taifa ni vijana, wengi wa vijana hawa wameajiriwa kwenye sekta isiyo rasmi na ni wengi kweli zaidi ya asilimia 70 katika nchi yetu na kwa wakati huu kundi hili linazidi kuongezeka maana mwanzoni lilikuwa na vijana wachache, lakini hasa ambao wana elimu ya darasa la saba, kidato cha nne na wengine kidato cha sita, lakini sasa hivi linaingiza kundi la vijana wasomi ambao pia wamemaliza hata chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi hili linaanza kuwa muhimu sana wakati huu na tusipoangalia kama Serikali basi tutakuwa tunapoteza nguvu kazi nyingi kwa sababu wanajiunga kwenye kundi la sekta isiyo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii isiyo rasmi ina changamoto nyingi. Moja ni udogo wa mtaji, mitaji yao ni kidogo sana. Pili, ni tija ndogo kwenye uzalishaji wanaohusikanao, pia wana matumizi duni sana ya teknolojia pia utaratibu wa wao kujisajili na kuwa kwenye sekta rasmi ni mrefu sana Kiserikali unawakwaza. Kodi ambazo zinatozwa kwenye kundi hili si rafiki sana kuwafanya waondoke kwenye sekta isiyo rasmi kuingia kwenye sekta iliyo rasmi, kubwa kabisa ni kwamba kundi hili lina ukosefu wa mahali pa kufanyia shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mara nyingi watu hawa wamekuwa wakiondolewa, wakikaa mahali fulani kidogo wanaondolewa, aidha inatolewa amri na Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa. Wote tumeshuhudia kipindi kilichopita namna ambavyo kundi hili la wafanyabiashara, wale wasio rasmi, walivyofurushwa kule Mwanza na Dar es Salaam mpaka Mheshimiwa Rais mwenyewe akaingilia kati. Kwa kuangalia matatizo haya waliyonayo hatujaonesha kama Taifa kwamba tunataka kulipunguza kundi hili la sekta isiyo rasmi ili liingie kwenye sekta iliyo rasmi, hivyo mchango wake katika Taifa hili kiuchumi na kimapato umekuwa mdogo sana kwa sababu siyo rahisi sana kulifuatilia kundi hili kwa mifumo rasmi iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie upya mfumo wake ili kulifanya kundi hili litoke katika sekta isiyo rasmi liingie kwenye sekta rasmi ambayo itatoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu, vinginevyo tukiliacha namna hii na kundi hili linaendelea kukua basi tutakuwa na kundi kubwa. Tunapokuwa na kundi kubwa limekaa kwenye sekta isiyo rasmi, wataalam wa uchumi wanasema bado kundi hilo litabaki kwenye hali ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naisihi Serikali ije na mkakati au sera mpya kwa sababu sera iliyopo inayolihusu kundi hili, ile ambayo nimeiona ni ile ya mwaka 1994. Sasa kama ipo nyingine labda sijaiona, lakini kama ni ya zamani kiasi hicho basi Serikali ni vizuri ije na sera mpya, sera hiyo iainishe ni kwa namna gani inalitoa kundi hili kutoka kwenye sekta isiyo rasmi kuliingiza kwenye sekta iliyo rasmi ili kundi hili pia liweze kulipa kodi kwa Serikali na liweze kutoa ajira kwa wananchi walio wengi kwa sababu likibaki kwenye kundi hili la sekta isiyo rasmi haliwezi kutoa ajira tunazozitegemea na hatuwezi kupata mapato ya kutosha kwenye kundi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka niliongelee ni suala la taarifa zinazotoka kwenye Taasisi za Serikali. Mwaka jana mwezi wa Oktoba mwanzoni au mwezi wa Septemba mwishoni, *Tanzania Meteorological Agency (TMA)* walitoa taarifa yao kuhusiana na hali ya mvua ya vuli na mwelekeo wa mvua za masika zitakavyokuwa. Taarifa hii ilitolewa kipindi kile cha Oktoba na Disemba na wakatahadharisha pia kwamba kipindi cha masika Novemba mpaka Aprili pia ni wakati wa mvua za masika lakini mvua zitakuwa ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizi sikuona kama zinaratibiwa vizuri na kutumiwa vizuri na watu walioko Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kiasi kwamba sasa tulipofika kwenye mvua za vuli, mvua za vuli kweli zilikuwa ni chache, maeneo mengi yalikuwa ni makavu na maeneo mengi yanayotumia mvua za vuli kulima walipolima hawakuotesha na wengine waliootesha mazao yalikauka

kwa sababu kipindi cha mvua kilikuwa kifupi sana. Hata hivyo, kipindi cha mvua za masika pia kilichelewa sana mvua maeneo mengine zimenyesha Februari na Januari mwishoni, matokeo yake wakulima walipopanda mvua tena zimekuja kukatika hapa katikati. Sasa matokeo yake tumekuwa na mavuno kidogo katika maeneo mengi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua na tunakumbuka kweye Bunge hili kwamba Bunge lililopita, Waziri wa Kilimo alikuja na takwimu akasema Wilaya kama 55 hivi zina upungufu mkubwa wa chakula, lakini hatukuona hatua zinazochukuliwa na Serikali kuanzia pale *TMA* walipotangaza hali za mvua kutopatikana zile za vuli na hata hizi za masika. Hatukuona hatua zinazochukuliwa na Wizara ya Kilimo ili kuwatahadharisha wakulima na kuwatayarisha waweze kujitayarisha na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona shida hapa kwamba, taarifa zinatoka hukohuko Serikalini, Taasisi ni ya Serikali, zinakuja huku upande mwingine hazitumiki vizuri. Sasa ninaiomba Serikali wawe na uratibu mzuri wa taarifa zinazotoka hasa zinazotusaidia wanyonge kama wakulima huko kijijini. Vinginevyo tusipopata tahadhari ya namna hii tunaendelea na mambo tukijua mambo yatakuwa kawaida na kumbe kule mbele tunakutana na hatari. Kwa hiyo, niiombe Serikali wawe wanaratibu vizuri taarifa zinazotoka kwenye taasisi zake ziweze kuwa za manufaa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka jana inasema fedha zilizoombwa ni shilingi bilioni 236 na kuendelea, lakini mwaka 2017/2018 fedha zilizoombwa ni shilingi bilioni 171. Fedha ya Matumizi ya Maendeleo 2016/2017 ni shilingi bilioni 165 lakini mwaka 2017/2018 ni bilioni ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaki muda wako umekwisha.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Ooh! Ahsante, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Anatropia Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Kasuku Bilago na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nitaanza kwa kum-*quote* mwanasayansi mmoja anaitwa Albert Einstein aliwahi kusema; "Dunia ni mahali hatari pa kuishi siyo kwa sababu ya watu ambao ni wabaya, bali ni kwa sababu ya watu ambao hawafanyi lolote dhidi ya uovu."

Nitarudia, dunia ni mahali hatari pa kuishi siyo kwa sababu ya watu waovu bali kwa sababu ya watu wema ambao hawawezi kukemea uovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini nasema haya? Tangu asubuhi leo tunaongelea kupotea kwa mwananchi wa Tanzania anayeitwa Ben Saanane. Wanahesabika ni watu wangapi wanasema Ben Saanane kapotea na wanaoonekana kuongelea kupotea Ben Saanane wamekaa upande fulani, lakini Ben Saanane ni mwananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ana haki ya kuishi na ambaye kwa kupitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaipa Serikali mamlaka ya kulinda uhai na usalama wa raia wake kwa mujibu wa Katiba hii. Tunapoongea kila siku hapa hatupewi jibu kutoka kwenye vyombo husika na kwa Waziri husika, huko ni kuonesha tunashindwa kutimiza wajibu wetu na ndiyo tunarudi kwenye kauli kwamba watu wema tunavyozidi kunyamaza kimya tunafanya dunia iwe siyo mahali salama pa kuishi, hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarudi kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nirudi kwenye majukumu yetu kama Wabunge hasa tukiwa kwenye Bunge la Bajeti

hasa tukiwa na wajibu mkubwa wa kuisimamia Serikali. Siku za hivi karibuni nimeona mara nyingi mtu ukiongea unaambiwa umemwongelea Rais badilisha hotuba au umemtaja Rais, nataka kujua ni lini Bunge kama Bunge inaruhusiwa kuisema au kuisimamia Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasoma kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la mwaka 1977 ibara ya 4(2) inaipa mamlaka Bunge na inasema; "...na vyombo vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma vitakuwa ni Bunge na Baraza la Wawakilishi."

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Bunge tunapewa mamlaka ya kuisimamia Serikali, kusimamia utendaji wa kazi zake za umma na tunafanya hivyo kwa niaba ya wananchi ambao ni umma. Tunapokuwa tunakuja hapa tunasema Serikali haijafanya moja, mbili, Rais katoa tamko moja, mbili na tunaambiwa tufute nini wajibu wetu kama Wabunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda mbali zaidi kifungu cha 63(2) nitasoma kinasema; "...kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii."

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge humu ndani kila mtu aliapa kuilinda Katiba hii, tunapofika hapa tunaambiwa tusiseme, tusiielekeze Serikali, tusiikosoe Serikali tuliapa nini hapa kama siyo unafiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba hiyo hiyo tuliyoapa kuilinda na kuitekeleza inakuja Ibara ya 100 kama Bunge inaongelea Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Ibara ya 100(1) na (2) "Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge..." Pia kifungu cha 46A kinaongelea ni namna gani Bunge kama muhimili linavyoweza kumshtaki na kumwajibisha Rais. Kama tunakuja hapa Bungeni tunaambiwa usimseme mtukufu ukimsema umevunja Katiba ni lini kama Bunge likiamua sijasema lifanye hivyo, lini kama

Bunge likiona inafaa linaweza kumjadili na hata kumwondoa Rais madarakani kama tunaogopa hata kusema utendaji wa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusikwepe madaraka yetu, hii nchi imeridhia utawala bora, kuna *checks and balances.* Kama Bunge tunawajibu wa ku-*oversee* Serikali inafanya nini, kama Bunge tunapaswa kuiambia Serikali ulivyofanya hivi ni sahihi au siyo sahihi. Iweje kila siku mnasema msitamke hilo neno huyo ni mtukufu, huyu ni nani, naona sasa tunavuka mipaka. Tunaendelea kupunguza uhuru wetu bila kujua kwamba kuendelea kujinyima uhuru hatuwatendei haki watu tunaowawakilisha. Tunasahau tunavyoendelea kujinyima uhuru tunashindwa kuhoji mambo kadha wa kadha ambayo yanatuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti. Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni kiongozi na msimamizi wa Serikali Bungeni, tunaongelea Serikali unayoisimamia kwa mwaka unaoisha wa fedha 2016/2017 Serikali yako tukufu ikiwa imepanga bajeti ya shilingi trilioni 11 imeweza tu kukusanya trilioni tatu sawa na asilimia 26 kama mapato ya ndani, ikaweza kupata shilingi bilioni 871 ambazo ni fedha za wahisani. Kwa hiyo, jumla ya bajeti kwa fedha tuliyonayo ya maendeleo tunaona tuna shilingi bilioni 33 ambayo ni asilimia 33 ya bajeti nzima mnayoileta tuiongelee.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninayasema haya? nasema haya kwa sababu ukisoma kwenye takwimu unaambiwa uchumi unapaa, uchumi haupai tu, uchumi ni matokeo ya fedha zilizopekewa kwenye Halmashauri. Uchumi kukua mabadiliko ya maisha ya watu ni matokeo ya fedha tulizoweza kukusanya, takwimu za *TRA* zinasema kwamba uchumi umeendelea kupaa na wamekusanya fedha nyingi. Wanaonesha mpaka Machi, 2017 wameweza kukusanya shilingi trilioni 1.34; ukilinganisha na mwezi wa Machi 2016 ambako walikusanya shilingi trilioni 1.31 ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.23. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa mwaka huu

tumekuwa na *turn over* ndogo ya fedha za maendeleo kuliko wakati mwingine wowote. Nataka nijue kama uchumi unakua kwa *TRA* mbona fedha ya maendeleo haiendi? Mimi ni mtu wa Dar es Salaama kwa takwimu za mwezi Oktoba 2016, kulikuwa na biashara 1,741 ambazo zimefungwa katika Jiji la Dar es Salaam ambayo inaonesha ni sawa na biashara 580 sawa na biashara 19 kwa siku zinafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo naona *contradiction TRA* mapato yanapanda na biashara zinashuka, lakini bajeti ya maendeleo inazidi kushuka kabisa, hapo kuna kitu hakipo *straight* Waziri Mkuu, msimamizi wa kazi za Serikali Bungeni tunaomba utuambie mbona *contradiction?* Mapato yamepanda, biashara zinafungwa na fedha ya maendeleo haiongezeki ni lazima tuangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimewasomea Waheshimiwa Wabunge kwamba Wabunge tuna jukumu la kuisimamia Serikali, Serikali ituambie kama uchumi unakua mbona hatuoni fedha za maendeleo kwenye maeneo yetu? Mmechukua hata hela yetu ambayo ni kodi ya majengo, mmeiongeza kwenye hiyo fedha ya maendeleo, kule kwetu kumedorora kule. Mimi nadhani ni heri zile fedha za kodi ya majengo tuziache kwenye Halmashauri ili kwenu yakibuma walau kwenye Halmashauri zetu mambo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliwaomba wananchi kwamba wampe muda kitambo ana hakiki watumishi hewa, aliomba miezi miwili leo tunaingia mwaka wa pili, watu wamemaliza elimu zao, watu wamepata mikopo wamesoma huu ni mwaka wa pili hawajui wataajiriwa lini, tunataka kujua hawa watu wataajiriwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabisa ambalo lipo kwenye Ofisi ya Spika ni kwamba tuliambiwa fedha zilibaki kwenye Mfuko wa Bunge takribani shilingi bilioni sita zikarudishwa Ikulu lakini hapa Wabunge wanalia

wanasema hawana Ofisi, Ofisi hazina *furniture,* tumekuwa tunajibana lakini kumbe watu wanapeleka fedha Ikulu. Tuangalie kipi kipaumbele tunaweza kufanya kama taasisi ya Bunge ni kuwapendezesha waliopo Ikulu au ni kufanya kazi kama muhimili na kujenga ofisi kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuamua tunataka kufanya nini, tunataka kufanya kama Wabunge au tunataka kufanya kama vivuli vya Serikali Dodoma? Tuamue tunaweza kufanya vipaumbele tukaamua kwamba tunataka tuisimamie Serikali, tunataka kuishauri Serikali na tunataka kuihoji Serikali ni kwa nini fedha za maendeleo hazijaja, kwa nini fedha za wahisani haziletwi? Ni kwa sababu tumeamua sisi kama Wabunge na pengine Wabunge waliokuwa wengi wameamua kunyamaza kimya. Pengine Wabunge walio wengi wanaoamua kusema wanaonekana wanasema sana na hawapaswi kusema, tuangalie tunawatendea haki Watanzania au hatuwatendei haki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitendea haki mioyo yetu na ninarudi kwenye kauli ya Albert Einstein anasema; “Dunia ni mahali hatari pa kuishi si kwa sababu ya watu ambao ni wabaya, bali ni kwa sababu ya watu ambao hawafanyi lolote dhidi ya uovu.”

Ujiulize upo kwenye upande upi wa shilingi, umeamua kunyamaza na kuacha mabaya yatamalaki au umeamua kukemea uovu ili mambo mema yatamalaki. Tukifuata kauli ya maneno hayo tutaweza kuwa Wawakilishi na Wabunge wema wenye kuisimamia Serikali na Serikali haiwezi kuleta tena asilimia 35 ya bajeti, itahakikisha itamiza hata asilimia 70 kwa sababu inajua wakija Bungeni bajeti haitapita, wakija Bungeni wataulizwa maswali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokiona hapa hata ikija asilimia tatu wanaoafiki tusemeje wanakuwa wengi inapita, lakini maendeleo hayaendi, Tanzania ya viwanda tunaweza kuisubiri na tukakesha inaweza isionekane kesho wala keshokutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kasuku Bilago atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi ajiandae.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii. Mimi najiuliza kidogo nirudi kwenye Katiba Ibara ya 63 hiyo aliyoinukuu Msemaji aliyemaliza kuongea, maneno ya kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano kazi ya Bunge.

Sasa najiuliza ili umsimamie mtu na kumshauri lazima huyo mtu awe kwanza anakubali kushaurika, awe anakubali kusimamiwa. Kusimamiwa unaweza ukalazimisha lazimisha vyovyote, lakini habari ya kushauri ni je, huyu anashaurika? Maana kama hashauriki utapata shida sana na huyo unayetaka kumsimamia*. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tujiulize je, Serikali yetu inashaurika? Kama haishauriki tunafanya kazi gani Wabunge katika Bunge hili? Hakuna kwenye Katiba hii sehemu iliposemwa ukiwa na chama chako ni tawala wewe ambae ni Mbunge wa Chama Tawala huruhusiwi kuisimamia Serikali yako. Nawaombeni Wabunge tufanye kazi yetu ya kuisimamia Serikali na kuishauri bila kujali itikadi zetu, vinginenvyo hatu-*play role* yetu kama Wabunge. Nilikuwa nawakumbusha hicho kipengele. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye bajeti na hali ya uchumi. Bajeti yetu ya maendeleo imetekelezwa kwa asilimia 34. Hivi hili linahitaji kuwa wa chama gani na chama gani? Asilimia 34 utekelezaji na asilimia 66 haijatekelezwa kwa nini tusiisimamie Serikali? Siamini kwamba hii Serikali inazo hizi fedha halafu ina roho mbaya haikuzitoa, basi tuisimamie ipate fedha na tunapotoa ushauri wa namna ya kupata fedha, vyanzo mbalimbali vya kupata fedha Serikali itusikilize, sasa isipotusikiliza halafu baadae inakwama inakosa hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa *donors* niliwahi kuongea mwaka jana nakumbuka, *donors* wetu kabla ya kuleta kwenye bajeti kuu huwa tunaweka ni mkataba gani tunafunga na *donors* kwamba hawata *default* ili fedha yote tunayoipata kwenye bajeti iweze kutoka. Tunapanga bajeti kubwa halafu baadae hatupati zile fedha na tunashindwa kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunashindwa kuitekeleza ni kwa nini tupange nyingine kubwa zaidi, tusibaki na bajeti ile ya mwaka jana na tukaweka vipaumbele vyetu ndani ya ile bajeti ya mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu haiingii akilini wewe ulitenga shilingi trilioni 29 halafu ikashindikana ukapanga shilingi trilioni 32, ni muujiza gani utakaofanyika tupate hizo fedha? Maana yake bajeti kama ni tegemezi inategemea wafadhili hatutafanya miujiza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la kilimo. Suala la kilimo tumejipanga kwamba tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, bila kuimarisha sekta ya kilimo hivi viwanda vitatoka wapi? Malighafi ya viwanda hivyo itatoka wapi? Sekta kubwa kabisa ambayo inaajiri watu wengi ambao wangeweza kumaliza umaskini katika nchi hii lakini ndiyo Wizara inayopewa fedha kidogo kabisa katika nchi hii Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana pembejeo tulipata wakati mgumu wananchi wanataka kutumaliza, mifuko 30 tunapeleka Kijiji kimoja nani apate mtoto wa Katibu Kata au mtoto wa nani? Mifuko 30 hivi wanaobaki wanakuwa ni wananchi hawatakiwi kulima katika nchi hii? Kama hawatakiwi kulima maana yake hawatainua uchumi wao.

Kuna Mheshimiwa amezungumzia habari ya pembejeo, kilimo bila pembejeo ni sawa na kuvaa nguo ambayo haikufuliwa, wewe unaona uko bomba tu unatembea kumbe hakuna kitu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo bila pembejeo unategema tuzalishe na wananchi wanatumia jembe la mkono, hili jembe la mkono maana yake wanalima kidogo wanatarajia kuvuna sana katika kidogo wanachoweza kulima. Sasa analima kidogo halafu hana pembejeo kwa hiyo hawezi kuvuna miaka nenda rudi umaskini unajirudia rudia, tunazidi kuwa na watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fulani huwa najiuliza hawa maskini wanatengenezwa ili wawe, maana yake mtu maskini kupiga kura ni lazima aelezwe namna ya kupiga. Ukiwa maskini utaambiwa tu fanya hiki, sawa, fanya na kile sawa. Kwa nini tunakubali kundi kubwa la Watanzania ambao ni wakulima waendelee kuwa ni maskini? Pembejeo haziwezi kupatikana kwa wakati kwa nini? Na pembejeo zipo humu nchini, utakuta mbolea... *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimefika kwangu kule Kakonko mwezi Disemba mbolea inakuja na mbegu inakuja tulishalima siku nyingi na tulishapanda ndiyo mbegu zinakuja. Hivi pembejeo ikija mapema ninyi mnapata hasara gani? Wakulima wakapata pembejeo mwezi wa sita, mwezi wa saba akakaa mbegu iko pale na mbolea ipo ili ajiandae kulima msimu unapoanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kuzungumza mwaka jana kwamba kuna siku tutaleta mbolea ya kuvunia sijui tutaipata wapi. Unaleta mazao karibu yanakoma kabisa wewe ndiyo unaleta mbolea, inanipa wakati mgumu sana. Wakulima hawa tuwahurumie walime kidogo, wavune sana waondoe umaskini ili wawe na uwezo wa kufikiri vizuri hata wakati wa kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la elimu. Upande wa elimu tumetoka kwenye semina ya TWAWEZA, hali ya elimu ni mbaya. Wanafunzi wa darasa la saba wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu ni asilimia 79 “K” tatu zile. Sasa walipewa mtihani wa darasa la pili wakashinda kwa asilimia 79, ndugu zangu hali ya elimu ni mbaya. Walimu wana malalamiko rundo, walimu wanaidai

Serikali shilingi trilioni moja, hawajalipwa na hakuna anayefikiria kuwalipa na kila wanapofikiria wafurukute ili waweze kulipwa ni vitisho vya kufanyiwa hili na lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeongea na mwalimu mmoja ananiambia mwalimu wakati wa mitihani siku hizi kama *mock* na nini, hatusimamii kwa kuogopa kufelisha tunawaacha, tunakaa nje waoneshane mle ndani ili *pass mark* iwe ya juu Mwalimu Mkuu asihamishwe shule hiyo au kuvuliwa madaraka, hayo ndiyo maelezo wanayoeleza shuleni. Wanachofanya tunasimamia nje kuangalia je, kuna pikipiki inakuja au gari la Afisa yeyote, tukiona ni shwari mle ndani wanaendelea kuoneshana na *pass mark* zinapanda, hiyo ndiyo elimu ya Tanzania tulipofika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tunasema, HakiElimu wamefanya utafiti juzi juu ya elimu bure, wakakuta elimu bure haijatekelezwa kikamilifu, taarifa waliyoitoa *front page* ya gazeti la Serikali likasema elimu bure imetekelezwa kwa asilimia 100. Hao waandishi wa habari wangekuwa wakati wa Mheshimiwa Nape Nnauye nadhani wangewajibika tu. Hivi asilimia 100 kweli ipo asilimia 100 na mwandishi yule yuko vizuri tu anamfurahisha nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii elimu ni mali yetu, tukiongeza wajinga hapa nchini iko siku wajinga watakaa waungane wachague mjinga mwenzao awe Rais wa nchi, tufike mahali tukatae hili, tukatae kabisa, kwamba tunataka elimu iliyo bora na sio bora elimu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishakubaliana kwenye Kamati yetu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwamba iundwe Tume ya kuchunguza elimu *in totality,* hali ya elimu ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hussein Bashe aliwahi kutoa hoja binafsi ya kuundwa kwa Tume, yaliyompata sijui ndiyo maana yuko kwenye orodha ile ya watu 11, hata sijui! Lakini hali ya elimu tunakwenda kule

ambako Marekani walipofanya utafiti waliambiwa *a nation at risk, its where we are going in this country.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bilago. Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi tutamalizia na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya, nampongeza Mheshimiwa Waziri Jenista na mdogo wangu Mheshimiwa Mavunde kwa kazi nzuri wanayomsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu, mambo yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi zangu naomba nianze kuchangia katika kilimo cha tumbaku ambacho wakazi wa Mkoa wa Tabora ndiyo zao la kiuchumi kubwa tunalolitegemea katika mkoa wetu. Baada ya malalamiko mengi ya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usikivu mkubwa sana ameanza sasa kufuatilia kero mbalimbali na kutatua changamoto zilizopo katika zao letu la tumbaku.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hongera kwa kazi kubwa unayoifanya sasa wananchi wa Tabora, kwa kuwa walikuwa wanahisi kwamba korosho na wewe unatoka huko sasa tunaamini ni mchapakazi na kero za tumbaku zitakwisha na sasa tunakoelekea mkulima wa tumbaku atapata faida ya zao hili la tumbaku ambalo analilima. Mheshimiwa Waziri Mkuu unajua tumbaku ikisimaiwa sawasawa ni zao ambalo linaingiza pato kubwa kwa nchi yetu, itasaidia katika maeneo mbalimbali ya kutatua kero za wananchi wetu kwa ujumla katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo machache ambayo

tunataka Mheshimiwa Waziri Mkuu utusaidie ili zao hili liendelee kumnufaisha mkulima wetu. Zipo tozo mbalimbali ambazo mkulima anakuwa-*charged* zinapunguza faida yake katika zao zima la tumbaku. Tunaomba tozo hizi zipungue zibakie tozo za msingi ili kumwondolea mkulima mzigo mzito aliokuwa nao. Tunataka tupate bei nzuri na ili kupata bei nzuri ni lazima sasa tuangalie pia masoko mengine ya kuweza kupata wanunuzi wa tumbaku ili zao hili sasa liweze kuleta tija kwa mwananchi wa Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala dogo pia kuhusu hawa wakulima *(independent farmers)* ambao tuliwaambia warudi kujiunga na ushirika, wamekubaliana na wazo hili wameshajiunga na vyama vya ushirika, tunaomba sasa na wenyewe wasaidiwe ili kuwasaidia katika kilimo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia wakati tunaangalia zao la tumbaku, sisi Tabora tunarina asali nzuri sana, tunarima asali nyingi, juhudi hizo zinazoelekezwa katika kutatua changamoto za mazao mengine naomba tuliangalie zao la asali pia katika kuboresha mazingira yake, kwanza katika kuliandaa zao lenyewe na kurina asali hiyo mwisho wa siku kuitafutia soko litakalomsaidia mkulima wa asali katika Mkoa wa Tabora. Asali ni dawa, asali ni kitu ambacho kinasaidia katika maeneo mengi na vilevile inaongeza mapato kwa wananchi wetu wa Mkoa wa Tabora na maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee tatizo la maji lililopo katika Mkoa wa Tabora sana katika Jimbo langu la Igalula. Tunapongeza juhudi za Serikali katika kutatua changamoto za maji katika Mkoa wetu wa Tabora, kwa sasa tunatarajia kupata maji kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema huko nyuma, mradi huu wa kuleta maji toka Ziwa Victoria katika Jimbo langu la Igalula hatumo katika programu ya kuleta maji ya Ziwa Victoria, baadhi ya maeneo mengine wanapata maji hayo sisi tumekubaliana na hilo, tunajua

Serikali itatuangalia baadae, kwa sasa tunaomba Serikali iangalie njia mbadala za kutatua kero za kupata maji katika Jimbo letu la Igalula ikiwemo kuchimbiwa visima, kuchimbiwa malambo kwa sababu mazingira yanaruhusu kuweza kuchimba mabwawa na kuweza kutatua kero za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tuliambiwa tutafanyiwa usanifu katika Kata ya Goweko tuna bwawa moja kubwa na Kata ya Loya, lakini sijaona chochote ambacho kimefanyika, tunaomba Serikali iangalie. Tumekosa mradi wa maji ya Ziwa Victoria basi tuweze kuangaliwa kupata maji katika maeneo mengine.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua bajeti mwaka huu sio nzuri sana kuweza kutekeleza miradi yote ya maji lakini nakumbuka tulijaribu kuishauri Serikali namna ya kupata pesa za kugharamia miradi ya maji katika vijiji vyetu. Tulishauri hapa kwamba tuongeze hata shilingi 100 katika bei ya petroli ili hela hizo ziende kwenye mfuko wa maji ziweze kutatua kero za maji katika vijiji vyetu, Serikali haijakubaliana na wazo hilo. Naomba sasa Serikali ikubali tuongeze shilingi 100 katika bei ya mafuta ili tuweze kutengeneza mfuko wa maji utakaosaidia kutatua kero za maji katika maeneo yetu, tumtue mama ndoo kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mama anateseka kupata maji kilometa zaidi ya 10 hadi 15, mwisho wa siku mama huyu anarudi apike chakula, mama huyu tunashindwa kumsaidia. Tunaomba tuweze kufanya hili ili kuweza kusaidia kutatua kero ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisemee kidogo suala la barabara. Wakati nataka kuchangia katika barabara naomba nitoe pongezi kwa Serikali kusikia kilio chetu cha barabara ya Itigi – Tabora, kipande cha Chaya – Nyahua cha kilometa 85 ambacho kimekuwa ni kero kubwa sana kwa wasafiri wanaokwenda Kigoma, Mpanda na Katavi, pamoja na wasafiri wanaokwenda Tabora. Kipande kile kikitengenezwa wasafiri wa Kigoma badala ya kuzungukia

Nzega na Igunga watapunguza kilometa zisizopungua 140 kufika Tabora na maeneo mengine. Tumepata pesa toka *Kuwait Fund* nina hakika kabisa tutatengenezewa barabara hii, tunashukuru sana kwa kusikia kilio cha Wanatabora na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba kipande changu cha barabara kipandishwe hadhi kutoka Buhekela kuja Miswaki kuja Loya kwenda Iyumbu. Barabara hii ni muhimu sana inaunganisha majimbo manne ya uchaguzi, Jimbo la Igunga, Jimbo la Manonga, Jimbo la Igalula na Jimbo la Singida Vijijini, inaunganisha Wilaya tatu, Wilaya ya Igunga, Wilaya ya Uyui na Wilaya ya Singida Vijijini. Pia inaunganisha mikoa miwili ya Tabora na Singida. Kuna kilimo kikubwa sana cha mpunga kule, barabara hiyo mvua ikinyesha katika kipindi cha miezi minne haipitiki, tunaomba Serikali itusaidie katika hili kama walivyosikia barabara ya Chaya nina hakika na barabara hii tutasaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la elimu. Ninaipongeze Serikali kwa namna inavyoboresha upatikanaji wa elimu sasa, elimu bure baadhi ya watu wanasema haijaleta mafanikio makubwa, lakini kila jambo lazima liwe na mwanzo, mwanzo lazima kuna changamoto nyingi, tumekutana na changamoto nyingi Serikali itazifanyia kazi. Kiukweli wananchi wetu waliokuwa wanashindwa kupeleka watoto wao shule sasa wanapeleka watoto shule na ushahidi ni kwamba shule hizo madarasa yamejaa tunaelekea kupata changamoto ya kujenga vyumba vya madarasa. Kwa hiyo, Serikali ijipange kuboresha kupata madarasa pia napongeza tumetengeneza madawati ya kutosha, mpaka sasa madawati yanawekwa nje, hili lazima tupongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuboreshe mazingira ya ufundishaji, maslahi ya walimu ni lazima tuyaboreshe, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge pale madai ya walimu ni lazima tuyaangalie. Tunapoboresha maslahi yao, mazingira ya kufundishia pia lazima tuyaboreshe kwa maana ya kujenga nyumba za kuishi walimu katika maeneo yetu,

walimu wanapata taabu pa kukaa, wanaondoka kufundisha vijijini kwa sababu hakuna nyumba za kuishi. Lazima tutengeneze mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba katika kuboresha elimu na nyumba na maslahi ya walimu ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu pia naomba niseme jambo moja, vijijini kuna maeneo ni mbali zinapopatikana shule za msingi. Tumeanza kuhamasisha kujenga *satellite schools* ambazo zinasaidia watoto badala ya kutembea kilometa zaidi ya 20 kwenda kufuata shule mama tumeamua kuzijenga ili ziweze kutatua changamoto ya elimu, lakini bahati mbaya sana Wizara ya Elimu haitusaidii, wananchi wanajenga shule hizi katika wakati mgumu sana, nyingine zimetimiza vigezo zaidi ya asilimia 70 lakini kigezo kikubwa sana ni umbali kutoka katika *satellite* kwenda kwenye shule ile mama, zaidi ya kilometa 20 mtoto anatembea, hii inasababisha mtoto anakataa tamaa ya kwenda shule, wasichana wadogo wanabakwa njiani wanakatishwa masomo, tunasema tunataka kuzuia mimba za utotoni lakini kwa kuzuia kusajili *satellite schools* hizi tunaweza tukasababisha pia mimba za utotoni kwa hawa watoto kubakwa njiani wakati wanakwenda kutafuta shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba zile shule ambazo tumesema zisajiliwe Mheshimiwa Waziri, tunatoka huko mazingira ni magumu, wananchi kutokana na hali ngumu hii tunawachangisha pesa tunajenga shule zile, zingine zimefikisha vigezo *at least* asilimia 70 na kuendelea, tunaomba zisajiliwe. Kikubwa ni kusaidia nguvu za wananchi ambazo wanazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yetu ya Uyui ni Wilaya mpya, tunajenga... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza au pili?

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nizungumze kwa uchache sana upotoshwaji ambao unafanya ndani ya Bunge na kwa Watanzania kuhusiana na suala la mgogoro wa CUF. Nashangaa sana kwa Wabunge wanaotumia muda wa Bunge kupotosha umma kumshambulia Msajili wa Vyama kwamba anaingilia migogoro ndani ya vyama wakati wao wenyewe wameshindwa kuijua, kuisimamia na kuiheshimu Katiba ya chama chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo waliodiriki kusema kwamba Msajili wa Vyama ni karani tu anayekusanya na kutunza mafaili ya vyama vya siasa, hii ni aibu kubwa kwamba Mbunge hajui hata Sheria ya Vyama vya Siasa inasemaje juu ya majukumu ya Msajili wa Vyama. Msajili wa Vyama anafanaya kazi ya kulea na kusimamia vyama vya siasa, kazi yake siyo karani, waende wakasome Sheria ya Vyama vya Siasa, majukumu na kazi za Msajili wa Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msajili wa Vyama vya Siasa hakuingilia mgogoro wa CUF peke yake, alipelekewa malalamiko na viongozi ndani ya Chama cha Wananchi CUF, chombo cha mwisho cha maamuzi ni Mkutano Mkuu wa Taifa, Wajumbe 324 walipeleka malalamiko kwa Msajili wa Vyama juu ya uhuni uliofanyika ndani ya Mkutano Mkuu wa Chama uliofanyika tarehe 21 Agosti, hakuingilia alipelekewa malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msajili wa Vyama

hajamteua Mheshimiwa Sakaya kuwa Kaimu Katibu Mkuu, Katiba ya Chama cha CUF, kipengele 93, Sura ya Tatu kinampa Naibu Katibu Mkuu wa upande wa Bara mamlaka ya kufanya kazi za Katibu Mkuu pale Katibu Mkuu anaposhindwa kutekeleza wajibu wake kama Katiba inavyomwongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wabunge wasipotoshe Umma, wasipotoshe Bunge, wasitumie muda wa Bunge kwa ajili ya kudanganya Watanzania, wafanye kazi kwa ajili ya maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Tabora kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri aliyofanya kuweza kurekebisha Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Tabora na ku-*overhaul system* nzima ya ushirika ya Mkoa wa Tabora, ni matumaini yangu kama watendaji wa Serikali watazingatia maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu na kuyafanya vizuri nina imani kabisa kwamba kilimo cha tumbaku cha Mkoa wa Tabora kitanufaisha wakulima kama tunavyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa suala linalozungumzia suala la uchumi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba, utulivu unahitajika humu ndani tafadhali, umeingia sasa hivi umelikuta Bunge likiwa limetulia.

Mheshimiwa Sakaya endelea.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uchumi. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inasema kwamba uchumi unapanda na umekua kwa asilimia saba lakini pia kwamba mfumuko wa bei umepungua. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa ku-*wind up* atuambie, uchumi unapanda wakati hali ya maisha ya Tanzania inazidi kuwa mbaya, hali ya uchumi inazidi

kuwa mbaya, pia wafanyabiashara wengi mitaji inazidi kuzama, wanafunga maduka yao, hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya maisha ya kawaida unazidi kuwa mbaya unazidi kuwa mdogo. Sasa huu uchumi unapanda, mimi sio mchumi, uchumi unaopanda wakati fedha mifukoni inazidi kupotea ni uchumi wa aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kupanda kwa bei ya gharama za vyakula, wakati tunaambiwa kwamba mfumuko wa bei unapungua lakini ukienda sokoni, leo nimekwenda sokoni na jana nimekwenda sokoni, kilo ya mchele shilingi 2,400, kilo ya unga shilingi 2,200, maharage nimenunua leo shilingi 2,400 bei zinazidi kupanda. Kwa hali ya kawaida, Watanzania wengi kwa hali ilivyo sasa hivi hawana uwezo wa kuweza kula milo miwili ya uhakika kwa siku.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali lazima iangalie namna, kama vyakula vimefichwa vitoke vije ndani ya masoko ili bei zishuke. Kuambiwa kwamba bei zinashuka mfumuko wa bei unapungua wakati hali inazidi kubana, haiendani na hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwezeshaji wa vijana. Hotuba ya Waziri Mkuu inatuambia kwamba Serikali imetoa *almost 1.5 billion* kwa ajili ya kusaidia mfuko wa vijana na akina mama pia halmashauri zetu zimetenga fedha karibu shilingi bilioni 4.6 kwa ajili ya kuwezesha vijana na akina mama, kwa Mikoa yote ya Tanzania na Wilaya zetu karibu 140 bado ni fedha kidogo sana.

Kwanza fedha inayotolewa na Serikali, shilingi bilioni 1.5 ni ndogo kwa sababu vikundi ni vingi na vingi havipati hiyo hela ya kukopeshwa. Halmashauri zetu ile asilimia tano haitengwi, wanatenga kidogo sana kwa sababu hali ya Halmashauri pia makusanyo siyo mazuri na wengine fedha zao ni kidogo, hawana uwezo wa kutenga asilimia tano kwa ukamilifu, matokeo yake vikundi vimeundwa vingi vya akina mama, vya vijana, hawapati mikopo wanafuatilia mwaka baada ya mwaka hawapati mikopo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza Serikali ihakikishe inaongeza fedha za mikopo ya vijana na akina mama za kutosha kwenda kwenye Halmashauri zetu. Pili, kuwepo ufuatiliaji wa kutosha, Halmashauri zitenge fedha za kutosha na kulipa, vikundi vinakopa zile fedha hazirejeshwi, matokeo yake inashindwa kuwa *revolving fund* ambayo kama ingekuwa inarejeshwa kwa wakati wengine wangepewa, matokeo yake Halmashauri hazirejeshi, vijana wengine wanasubiri miaka miwili hawajapata mikopo. Kwa hiyo, suala la uwezeshaji wa vijana bado ni tatizo kubwa, fedha inayotolewa ni kidogo, haitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira, bado tatizo ajira ni kubwa ndani ya nchi yetu na vijana wengi bado wanazurura, wapo kwenye vijiwe, wapo mitaani. Ni kweli kwamba asilimia karibu 57 ya Watanzania wameajiriwa kwenye sekta binafsi, lakini mazingira wanayofanyia kazi kwenye sekta binafsi ni magumu mno. Mishahara yao ni midogo, kwanza hawaingizwi kwenye mifuko ya jamii lakini wengine hawana likizo, hawana chochote, wanashindwa wafanye nini kwenye mashirika binafsi. Wengine wananyimwa mpaka haki zao za uzazi, mwanamke akipata mimba akiwa kwenye mashirika binafsi au viwanda anaachishwa kazi kwa sababu tu kapata mimba, hata ile haki ya kuzaa ananyimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali ifuatilie, ni kweli kwamba sekta binafsi zinasaidia sana kwenye ajira ya Watanzania lazima tuwapongeze, lakini lazima sheria za kazi zifuatwe. Kama Serikali imesema kima cha chini cha mshahara kwa nini kule wakatoe shilingi 100,000, 120,000 kwa mwezi. Kwa maisha ya sasa hivi kumpa mtu 120,000 kwa mwezi anaishije? Anafanya kazi zaidi hata muda wa saa za kazi wengine mpaka usiku. Pia wengine hawapewi mikataba ya kazi wanafanya kazi kama vibarua, miaka saba mpaka kumi wanaajiriwa kwa miezi mitatu, mitatu wanakosa haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, wametuambia kwamba wanatengeneza Mabaraza ya Kazi,

maeneo mengine hawaruhusiwi kutengeneza mabaraza ya kazi. Mimi nimeshuhudia kabisa makampuni yetu haya ya Kichina, hawawaruhusu kutengeneza Mabaraza ya Kazi, hata sehemu ya kupeleka malalamiko yao hakuna. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ihakikishe kwamba pamoja na kwamba wanatusaidia ni lazima pia wahakikishe kwamba wanaweza kutoa haki zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala la uzalishaji. Hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda kama hatusimamii vizuri suala la kilimo. Kilimo tusimamie kuanzia uzalishaji, utunzaji, usafirishaji mpaka kwenye masoko. Njia pekee ya kuweza kuwa na uhakika wa masoko ni kuwa na viwanda vidogo vidogo na viwanda vikubwa. Kila Mkoa Mungu ameubariki una zao la biashara, hebu Serikali iweke mkakati, nashukuru kwamba mashirika ya kijamii yameanza kuingia kwenye kutengeneza viwanda, wahakikishe kila Mkoa, tukianza na Mkoa wa Tabora, kiwanda cha tumbaku kijengwe mkoani Tabora, vijana wa Tabora wapate kazi ndani ya kiwanda cha tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Dodoma tuna zao la zabibu, tumeweka kiwanda kilichopo hapa kinachukua *concentrate* kutoka nje, tuhakikishe kila kiwanda kinachowekwa ndani ya Mkoa wowote kinatumia *materials* kutoka ndani ya mkoa wenyewe. Tukihakikisha kila Mkoa tumekuwa na kiwanda, kutumia *material* ya kilimo yanayopatikana ndani ya mkoa ule, kwanza tutazalisha ajira kwa wingi pia tutaweza kuwainua wakulima kwa sababu watalima kwa tija wana uhakika na masoko yao. Vinginevyo ni tatizo kubwa tutaimba mpaka tuchoke wakulima hatuwezi kuwainua na ukizingatia asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na wengi wako vijijini wanategemea kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tuboreshe kilimo, pembejeo ziwepo kwa wakati, tujenge maghala ya kutosha. Tukihakikisha kilimo kimekuwa na tija nina imani kabisa Watanzania walio wengi watanufaika na tutaweza kuondoa umaskini kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa jioni hii, lakini kwa upande wa Wabunge wa CCM ili kukamilisha uwiano wa idadi ya wachangiaji nitawataja majina ambao ndio watakaokamilisha kesho ili orodha mpya iweze kuanza. Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli. Kwa hiyo, hawa watachangia kesho asubuhi kwa ajili ya kukamilisha uwiano.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja na maelezo kidogo. Tangazo linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa William Ngeleja, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanaopenda michezo kuwa matokeo kutoka Mwanza timu ya Simba imeshinda mabao matatu dhidi ya *Mbao FC* ambao wamepata magoli mawili. Anawapongeza wanasimba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo nitoe maelezo kidogo na ni bahati mbaya kwamba Mheshimiwa Halima Mdee aliyetoa haya maelezo ametoka sasa, lakini naamini ataupata ujumbe.

Waheshimiwa Wabunge, yaliyotokea leo asubuhi kwa wale waliokuwepo wanafahamu kabisa tulisoma Kanuni zinataka nini, kwa hivyo majibu yalitokana na Kanuni tulizojitungia wenyewe. Sasa hoja ya watu kutekwa, hoja ya hofu ya watu kutekwa, hoja ya kuwepo kwa orodha ya watu wanaotarajiwa ama wanaojihofia kutekwa wote tunajua sheria zetu zinasemaje. Waliotekwa wanatafutwa na polisi na wenye hofu ya kutekwa wanaenda kuripoti polisi, hata aliyetishiwa pia anaenda kuripoti polisi, haji kuripoti Bungeni kwa sababu hiyo siyo kazi ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naona kuna mazingira ambayo tunajisahau na kufikiri kwamba Bunge linaweza

kufanya jambo lolote linalotokea huko nje, siyo kweli. Majukumu yako wazi Kikatiba, kazi ya Mahakama, kazi ya Bunge na kazi ya Serikali. Sasa haiwezekani Bunge likaacha kufanya kazi zake za msingi likaanza kufanya kazi za chombo kingine ni kuingilia kulekule ambako Bunge halitaki kuingiliwa basi hata lenyewe liache vyombo vingine vinavyohusika vifanye kazi yake. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, niwakumbushe tu kidogo kwa sababu hoja namna zinavyojengwa ni vizuri zijengwe, kwa sababu wote ni viongozi zijengwe kwa namna ambayo hazileti taabu kati ya viongozi tuliowachagua kwa ajili ya kutuongoza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mbunge unaposimama unatoa hoja kana kwamba wewe umeweka matabaka ya watu wanaokaa hapa mbele siyo sawasawa. Siyo sawasawa kwa sababu Kanuni zetu ndizo zinazoongoza yeyote anayekuwa amekaa hapa mbele. Sasa ninyi msitutengenezee sisi viongozi mazingira ya kuona kwamba akikaa fulani basi yeye atasoma Kanuni kwa namna fulani akikaa mwingine atasoma Kanuni tofauti, siyo sawasawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo, ndiyo maana Kanuni ya tano imeweka utaratibu ikiwa Spika ametoa maamuzi ambayo Mbunge hakubaliani nayo ama haridhiki nayo anachukua hatua kwa mujibu wa Kanuni hiyo kuonesha kutokuridhika kwake anampelekea taarifa hiyo Katibu wa Bunge, Katibu wa Bunge anampelekea Spika na Spika Kanuni zinamlazimisha kuitisha Kamati ya Kanuni.

Sasa usiweke mazingira ambayo kana kwamba Mwenyekiti ama Naibu Spika akiamua basi unakwenda kushtaki kwa Spika, aaah, Kanuni zinatuambia Kamati ya Kanuni ndiyo itakayokaa. Kwa hiyo, tuyaelewe haya mambo Waheshimiwa Wabunge tusitengeneze mazingira ambayo tunataka wenyewe kujiletea taabu hapa ndani, tutumie Kanuni zetu sawasawa.

Kwa sababu hiyo, nalazimika kurudia niliyoyasema asubuhi, kwa mujibu wa Kanuni ya 47(4) inasema Spika akiridhika, maana yake ukishatoa hoja yako lazima Spika aridhike nayo. Kwa hiyo, kama mimi sikuridhika maana yake sikuridhika na Kanuni zimeniambia hivyo, mimi ndiye ninayepaswa kuridhika, kama sikuridhika basi sikuridhika na ndiyo maamuzi nayatoa kwa namna ambayo mimi sijaridhika. Kama ingetolewa hoja hiyo kwa mwingine ambaye angeridhika atakuwa ameridhika kwa mujibu wa Kanuni, lakini usiweke mazingira kana kwamba angekuwa mtu mwingine ingekuwa namna tofauti, hapana.

Mheshimiwa John Mnyika uwe na heshima, nimesimama na ninazungumza, kwa hiyo, huwezi kuwa wewe una uwezo wa kuzungumza, Kanuni unazifahamu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo ya kumalizia jioni hii, Kanuni yetu ya 48 inaeleza kwamba jambo linaloweza kushughulikiwa na utaratibu wa kawaida wa sheria halitashughulikiwa humu ndani, unaziachia sheria zifanye kazi, kwa hiyo tusitengeneze mazingira ya kuleta mtafaruku ambao haupo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi, tarehe 11 Aprili, 2017.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 11 Aprili, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*